Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

____________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

_____________

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Novemba, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kwa Waziri Mkuu, lakini leo simwoni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Tanzania ni nchi ambayo ulimwengu wote unaiheshimu kwa sababu ya amani lakini nimeshangaa sana safari hii kila siku kukicha ni Arusha, Arusha; na kwa kuwa sasa hivi utalii na biashara za Wananchi wa Arusha zimeharibika na inasemekana kwamba Serikali yako ndiyo inazuia kumtoa Mbunge wa Arusha Mjini kwa dhamana; ni jambo gani zinazosababisha suala hili likwame?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Arusha kuna migogoro mingi kidogo ambayo imeingiliana, lakini ninaamini Mji wa Arusha bado ni tulivu kiasi cha watu kuendelea kufanya shughuli zao. Pia ni dhahiri kama ulivyosema, kama Watanzania ni lazima tuzingatie hilo ulilolisema, isije ikawa ni tatizo tena kwa upande wa Sekta yetu ya Utalii.

Tatizo ninalolipata kuhusiana na swali la Mheshimiwa Ngonyani, kwa sababu mambo mengi yamejitokeza ambayo yote yamesababisha kesi kadhaa kufunguliwa Mahakamani, pengine kwa hiki ulichokisema kwamba Serikali imekataa kumpa dhamana Mheshimiwa Lema, labda niseme kwa ufupi kwa maana ya kujaribu kujibu hilo kwamba kilichotokea hasa ni nini.

Tarehe 28 Septemba, 2011 Mheshimiwa Lema pamoja na watu kadhaa, walikamatwa Arusha kwa tuhuma kwamba wameandamana bila kibali. Kwa hiyo, wakapelekwa Polisi kwa ajili ya kuhojiwa na wakapewa dhamana siku hiyo, lakini wakaombwa tarehe 31 wafike Mahakamani. Kwa hiyo, tarehe 31 wakaenda mbele ya Hakimu wakasomewa mashtaka lakini mashtaka yale kusema kweli yalikuwa yanastahili dhamana, hakukuwa na shtaka kubwa ambalo lingeweza kumnyima mtu dhamana. Kwa hiyo, walijitokeza watu waliokuwa tayari kuweka dhamana na Mahakama ikakubali wote wapewe dhamana. Kwa hiyo, katika wale wote waliokuwa wamekamatwa kwa sababu hiyo, wote walitoka baada ya kupewa dhamana.

Sasa kilichotokea kwa Mheshimiwa Lema, kwa sababu ambazo ninashindwa kuzijua pamoja na kwamba alipewa hiyo fursa, lakini alikataa kwamba anataka kubaki gerezani. Mahakama ikajikuta haina cha kufanya, kwa hiyo, akachukuliwa akapelekwa rumande. Sasa hapo katikati kulitokea jitihada za kujaribu kushauriana naye na kadhalika. Kwa hiyo, tarehe 7 Oktoba ndiyo wakakubaliana kwamba, wapeleke maombi mbele ya Hakimu, tumsikilize Hakimu atasema nini halafu iwe ndiyo siku ambayo angeweza na yeye kutoka. Kwa hiyo, Mawakili wake wakapeleka barua kwa Hakimu naye akajibu kwamba tulishakubaliana kwamba kesi hii itatajwa

tena tarehe 14 Novemba, 2011 kwa hiyo, tusubiri mpaka tarehe hiyo na ilikuwa ni mamlaka ya Mahakama na iliona hivyo.

Kwa hiyo, tukawa hatuna la kufanya na ndiyo maana mpaka leo unamwona Mheshimiwa Lema bado yupo ndani. Kwa hiyo, tunatarajia tarehe 14 watakapokwenda mbele ya Hakimu, yatatoka maamuzi ambayo yanaweza pengine yakamsaidia kuona busara ya kutoka badala ya kuendelea kukaa ndani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nimetosheka.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika Bunge lililopita Kikao cha Bajeti, Bunge hili Tukufu lilipitisha katika *Finance Act* kuondolewa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT* katika vipuri vya kilimo hususan matrekta lakini hadi leo hii kodi hiyo inaendelea kukusanywa na inaendelea kutozwa na utekelezaji wake bado haujafanyika:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza; na je, hiyo kodi ambayo imeshakusanywa kuna uwezekano wa kuwarudishia ili bei ya vipuri iteremke ili tuendelee na Kilimo Kwanza na wakulima waendelee kunuifaka?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Jitu Soni ni kweli, Serikali ilichofanya iliamua kwamba ni vizuri tuondoe kodi na ushuru mbalimbali kwa ajili ya matrekta na matrekta yanapokuwa hasa yameambatana na vitendea kazi ambavyo ni sehemu ya trekta kwa maana ya matrekta, inaweza kuwa ni jembe na kadhalika. Kwa hiyo, hatukupata tatizo sana kwenye eneo hilo.

Tatizo limekuja kwenye vipuri, maelezo niliyopewa mimi ni kwamba, eneo la vipuri linawapa tabu Watu wa *TRA,* namna ya kuvichanganua na kuvitenganisha na vipuri kwa ajili ya magari ya aina nyingine hasa makubwa. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba, tutafute utaratibu ambao utatuwezesha mtu anapoagiza vipuri vya trekta pengine vipewe ama *code number* tofauti ambayo itakuwa ni rahisi kuweza kuwa na uhakika kwamba kinacholetwa kweli ni kipuri kwa ajili ya trekta na si vipuri mchanganyiko, yaani trekta na magari mengine. Ninadhani ni jambo la kitaalamu na pengine hofu tu kwa upande wa *TRA,* lakini tumekubaliana kwamba, wataliangalia tuone mfumo ambao unaweza ukatuwezesha tukapata matokeo ambayo tunayataka na mimi nafikiri ni jambo jema acha tuwape nafasi.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni Waziri Mkuu wa Uingereza Bwana David Cameroom amenukuliwa akitaka nchi tunazotegemea misaada kutoka kwao ikiwemo Tanzania kwamba ili tuendelee kupata misaada kutoka kwao basi ni lazima tukubaliane na sera yao ya kuingia kwenye ndoa za jinsia moja. Ninapenda kujua kauli ya Waziri Mkuu; je, kama Taifa tumeanza kujipanga sasa kukataa misaada kutoka Uingereza? *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Regia Mtema anataka msimamo wa Waziri Mkuu, mimi ninafikiri hunitendei haki, nadhani cha msingi hapa ni Serikali inasema nini. *(Makofi)*

Kama Serikali, kauli ilishatoka tayari. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alipotoa ile kauli ilikuwa ni kauli kwa niaba ya Serikali na bahati nzuri wapo Mawaziri wengine ambao nao waliongezea nguvu katika kauli yake. Kwa hiyo, Waziri Mkuu ukimtaka atoe kauli yake ni ipi tena maana kauli kama kauli ya Serikali imeshatoka! *(Makofi)*

Kama ulitaka maoni yangu mimi, ninachoweza kusema ni kwamba, ninakubaliana kabisa na msimamo wa Tanzania katika jambo hili maana mambo mengine haya lazima tukubali kwani hata wanyama hawafanyi hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kweli kwa wanadamu kama sisi ni jambo ambalo halikubaliki *morally* na ninadhani hata kwa misingi mingine yoyote.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa katika utawala wa kwanza wa nchi hii baada ya Uhuru Serikali ilitilia mkazo sana kukuza uchumi kwa kujenga viwanda vingi vya *Textiles* na kusindika matunda; na kwa kuwa Kiwanda kama *Machine Tools* na cha Magunia cha Mkoani Kilimanjaro na Viwanda kama *SUNGURATEX, KILITEX* na *MWATEX* ya Mwanza vyote vimefungwa; na kwa kuwa Kiwanda kama *TANGOLD* cha Korogwe Tanga hata zile mashine zimehamishwa; na kwa kuwa kila Wananchi wanapoulizia wanaambiwa Mikataba ya Viwanda hivi ipo kwa *CHC* yaani *Consolidated Holding Corporation:-*

Je, Serikali haioni kwamba sasa kufufua viwanda hivi kutaleta ajira kwa Wananchi na hususan vijana na wanawake ambao ni kundi kubwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kabisa na Mhesimiwa Betty Machangu kwamba, ukiweza kupanua viwanda nchini, vinatoa mchango mkubwa sana hasa kwenye ajira na ndiyo maana tulipofika miaka ya 90, Serikali iliamua kujaribu kuja na Sera ambayo ingetuwezesha viwanda vilivyokuwa vimekufa kwa muda mrefu viweze kupata fursa pengine ya wawekezaji wavifufue na viweze kufanya kazi kwa tija kama tulivyokuwa tumetarajia. Kwa hiyo, baadhi ya viwanda alivyovitaja ni sehemu ya viwanda hivyo, lakini vipo na vingine vingi ambavyo vipo katika kundi hilo.

Sasa kwa upande wa Serikali, ninaweza kusema yapo mafanikio katika baadhi ya viwanda ambavyo vimebinafsishwa au mashirika au makampuni yaliyobinafsishwa na ambayo kweli yametoa mchango mkubwa kwa upande wa Serikali baada ya kufufua. Vipo vilevile kama alivyovitaja ambavyo havijaweza kufufuka kwa kiwango tunachokitaka.

Sasa Serikali imefanya nini; kikubwa tulichokifanya ni kuona kwamba, *CHC* iendelee kuwa ndiyo chombo ambacho kitaendelea kutusaidia kusimamia maeneo haya ili kufanya uchunguzi wa kina na kuona ni kitu gani tunaweza kufanya ili tuweze kuvifufua viwanda hivyo polepole au hatua kwa hatua ili tuweze kunufaika zaidi.

Kwa hiyo, acha tuendelee na mtazamo huo na kwa sababu wameshapewa hiyo kazi, ninadhani tutafika mahali ambapo baadhi ya viwanda hivyo vinaweza vilevile vikapewa nguvu mpya na tukafaulu kupata matumaini tuliyokuwa tunayatarajia.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, takwimu kutoka *UN Commodity Trade Statistics Data Base* ya Mwaka 2010 inaonesha kuwa katika Nchi za Afrika Mashariki; Uganda inazalisha beli 125,000 kwa mwaka, Kenya beli 55,000 kwa mwaka....

**SPIKA:** Beli za nini?

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Beli za Pamba.

**SPIKA:** *Okay!*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Tanzania inazalisha beli 275 kwa mwaka. Inamaanisha kwamba Tanzania tunazalisha zaidi Pamba, lakini katika uuzaji, yaani *exports apparel* zinazouzwa Kenya zina thamani ya dola 279 milioni lakini za Tanzania ni dola 226 milioni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hizo takwimu tajwa hapo juu huoni kwamba Serikali kuna haja sasa hata kama *CHC* imeshikilia Mikataba hiyo ukawekwa Mpango Mkakati madhubuti na makini kwa sababu tumeshaanzisha *Public Private Partnership* ili kuanzisha kiwanda kimoja cha kutengeneza nguo; maana yake ni kwamba hata nguo ambazo zinaagizwa nje zitakuwa na gharama kidogo kuliko ambavyo tunafanya sasa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Betty Machangu ni sahihi na kwa kweli kama Serikali, hizo ndiyo jitihada ambazo tunajaribu kuzifanya. Ninachosema ni kwamba, kwa sababu kazi yenyewe ni kubwa lakini tutakwenda nayo na ninadhani tutafika mahali pazuri pa kufufua viwanda vingi zaidi.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kabisa mimi ninapenda niipongeze Serikali mwaka huu kwa kununua mahindi kwa bei nzuri tofauti na bei ya mwaka jana; lakini pia mimi ninapenda niipongeze Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Ludewa kwa kuongeza vituo vya kununua mahindi kutoka Kituo cha Shaurimoyo na Mlangali ambapo mwaka huu tuna Kituo cha Mawengi na Kituo cha Ludewa Kijijini.

Pamoja na haya ambayo nimeyasema, utekelezaji wa azma ya Serikali umekuwa ukisuasua, Watu wa *NFRA* walipanga kununua mahindi *metric tonnes 50,000* lakini mpaka sasa wamenunua *metric tones 10,000* na nyingine wamewakopa Wananchi.

Ninapenda kujua kwa nini sasa hivi zoezi hili limesimama na Serikali hainunui tena mahindi kutoka kwa wakulima?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mwaka huu Serikali ilikuwa imedhamiria kwamba itanunua tani 200,000 za mahindi na polepole tuweze kufika tani 400,000 mpaka kufikia mwaka 2015 kwa nyongeza ya tani 50,000 kila mwaka. Kwa hiyo, dhamira hiyo ilikuwa hasa lengo la mwaka huu.

Tulianza ununuzi mwezi Agosti mwanzoni, lakini tulianza tukijua tunakabiliwa na uhaba wa fedha kwa upande wa *NFRA*, wameweza kutumia fedha zile ambazo wametengewa kwenye bajeti na kuweza kununua kiasi cha mahindi yaliyokuwa yapo mikononi mwa wakulima. Wakati huo huo Serikali ikawa inafanya jitihada za kupata fedha ya ziada, kwa hiyo, tulichofanya ni kuomba benki na kimsingi Benki ya *NMB* ndiyo wamekubali kuwakopesha kiasi cha shilingi bilioni 20.

Wakati huo huo pia tumeona tutumie njia nyingine za ziada, kwa hiyo, tumeruhusu mahindi tani 10,000 kutoka kwenye maghala yetu yauzwe kupitia Wafanyabiashara wa Tanzania na Kenya kwa utaratibu ambao tumewekeana. Ninadhani muda si mrefu zoezi hilo litakuwa limeanza na kitakachopatikana tutaweza kukirejesha kwenda kununua na kulipa madeni kwa wakulima.

Tumeweza vilevile kuwaomba *World Food Program* na wao wanunue, wamekubali kununua tani 10,000 kwanza na tunavyozungumza, ninadhani karibu zote wameshanunua na kiasi cha fedha zitakazopatikana nazo tunataka tuzitumie kulipa madeni na kuendelea kununua mahindi. Hivi karibuni Rais amefanya uamuzi wa ziada kwamba, *World Food Program* tuwaongezee tani nyingine 30,000 kwa utaratibu huo huo na amekubali vilevile kwamba upande wa wafanyabiashara na wao tuwaongeze tani 30,000 kwa ajili ya shughuli hiyo ya kununua mahindi kutoka kwenye maghala yetu na alichosema ni kwamba turuhusu Wafanyabiashara wa Tanzania wanunue tani zote 30,000 kutoka kwenye maghala ilimradi bei itakayowekwa isiwe chini ya shilingi 350 kwa kilo.

Kwa hiyo, tunatarajia zoezi hilo linaweza likasaidia kuongeza kasi ya ununuzi lakini vilevile kulipa madeni. Matumaini yangu ni hayo na ninaomba wakulima wenzangu huko Njombe, Rukwa, Ruvuma, Manyara na sehemu nyingine zote, mtuvumilie kidogo wakati tunalikamilisha zoezi hili. Ninadhani ndani ya wiki moja, mbili, tutakuwa tumeshalikamilisha.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera yetu kwa wanyonge na wakulima imekuwa ni Kilimo Kwanza hasa zaidi kwa maneno lakini utekelezaji wake kwa vitendo umekuwa ni taratibu na umekuwa ukisuasua. Hivi unavyozungumza Wananchi wa Ludewa wanakusikiliza, wamekata tamaa kwa sababu mvua zinanyesha na mahindi yananyeshewa. *(Makofi)*

Kwa kuwa taratibu za kwenda kukopa benki zitachukua muda mrefu; unaawaambia nini Wananchi hawa wa Ludewa na maeneo mengine ambayo wamekwishakata tamaa kuhusu mazao yao ambayo sisi wenyewe tunawahamasisha walime halafu ununuzi umekuwa wa kusuasua na mara nyingine tunawakopa? Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Kama nilivyosema, ule mchakato wa kupata mkopo kutoka benki tayari umeshakamilika. Kwa hiyo, wakati wowote fedha hizo zitapatikana na tutakwenda kuzilipa na nyingine tutaendelea kununua mahindi, siyo kwamba ndiyo tunaanza sasa, hapana; sasa hivi tupo kwenye hatua ya mwisho kabisa na fedha hizo zitapatikana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, utaratibu wa vocha za mbolea na mbegu za ruzuku kwa mwaka huu unaonekana utakuwa tofauti kidogo. Jana asubuhi nilikuwa ninazungumza na DC wangu wa Mbozi akasema kwamba, badala ya kupeleka vocha za mbolea pamoja na mbegu za ruzuku, Serikali imepeleka Waraka unaozitaka Kamati za Pembejeo za Wilaya ziziandikie mamlaka za ununuzi wa vocha kule chini kwamba, Mawakala wapeleke mbolea ili kuwapa Wananchi.

Sasa mimi ninajiuliza; utaratibu huu utawahakikishia Wananchi kwamba mbolea na mbegu zitapatikana kwa wakati mwafaka hasa huu mwezi Novemba ambao tayari wameanza kulima? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tangu tumeanza zoezi hili la ruzuku ya pembejeo kwa mfumo huu wa vocha, kumekuwa na matatizo mengi na tumepata changamoto nyingi sana ambazo mpaka sasa bado tunakabiliana nazo. Katika kujaribu sasa kutafuta suluhu ya matatizo haya, tunajaribu kutumia mbinu mbalimbali tukiamini kwamba, zitatuondoa katika tatizo hili. Ninaelewa jihitada hizi mpya ambazo tumejaribu kufanya, lakini nikuombe tu Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba, kwa sababu hivi sasa sina maelezo kuhusiana na huo Waraka, ni vizuri nikapata nafasi na mimi nikauona, nione unasema nini. Ninajua tulikubaliana tutafute kila mbinu itakayotuwezesha kusimamia mfumo huu vizuri zaidi. Nikiuona pengine na mimi ninaweza nikakupa maelezo ya ziada.

**SPIKA:** Eeeh! Mheshimiwa si anasema hajasoma Waraka au unauliza nini?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza linalofuatia swali la msingi.

**SPIKA:** Mmh!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na utaratibu wa vocha ambao bado haujaeleweka wakati tunakwenda kwenye msimu wa kilimo, lakini pia zipo taarifa kwamba vocha zenyewe hizi zimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Je, tunataka kwenda mbele na dhana ya Kilimo Kwanza au kurudi nyuma? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Azma bado ipo pale pale, lazima twende mbele. Sasa anaposema zimepungua sana, sidhani kama ni kweli zimepungua sana, hapana! Kwa sababu tulianza na laki saba na nusu, tukaenda milioni moja na nusu, tukaenda milioni milioni mbili, azma yetu ilikuwa kwamba, tutoke kwenye milioni mbili twende mbele zaidi kidogo kulingana na uwezo wa fedha ambao tutakuwa tunauongeza kila mwaka. Kwa hiyo, ninadhani azma haijabadilika, bado mtazamo ni ule ule. Kunaweza kuwa na *constraints* za hapa na pale, lakini bado dhamira ni ya dhati kabisa, tuelekee na kuwapa nguvu kubwa zaidi wakulima wadogo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumwuliza swali Waziri Mkuu. Tanzania tunaamini haiwezi kwenda mbele bila uwekezaji na kwa bahati nzuri Sera hii inakwenda kwa upana mzuri zaidi kwa ajili ya kuhakikisha Mwananchi wa Tanzania anapata fursa ya maendeleo. Wilaya ya Kisarawe kuna Mwekezaji anaitwa *Sun Biofuels,* amekuja kuwekeza Zao la Jatropha ambalo hata Kitaifa hatuna hata Sera yake. Kwa bahati mbaya zaidi, ilionekana kwamba, Wananchi watapata fursa ya ajira, wataletewa miundombinu ya huduma za kijamii ikiwemo hospitali, shule na barabara lakini mpaka sasa mwekezaji yule hajafanya lolote.

Kwa bahati mbaya sana vijana karibu 750 ambao aliwachukua kwenda kung'oa visiki wote amewafukuza kazi na mwekezaji ameuza hisa zote kwa *Thirty Degree East,* kampuni nyingine mpya hata Halmashauri haina taarifa.

Je, Serikali inaeleza nini kuhusu ku-*revoke* hiyo kwa sababu Wananchi wa Kisarawe hawajui hatma ya watoto na vizazi vyao hapo baadaye? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Selemani Jafo, kwa kuleta hoja hii. Wapo baadhi ya wawekezaji makini, lakini wapo vilevile wawekezaji wengine ambao ninaona siyo makini sana.

Kubwa na ninaomba niwaeleze Watanzania wenzangu, Halmashauri zetu hizi nazo wakati mwingine zinakuwa hazifahamu wajibu wake ni nini kwa watu wake. Kwa sababu huwezi kuwa na Mwekezaji kama huyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, wakati Wilaya yenyewe imekaa haitaki kufuatilia kujua kuna nini na kuchukua hatua stahiki mapema kadiri inavyowezekana ili kuweza kudhibiti matatizo yanayoweza kujitokeza. Sasa hiyo ni dhahiri kabisa kwamba, Halmashauri yetu pale haikuweza kutimiza wajibu wake vizuri. Ninataka nikushukuru, maadamu umetuarifu, basi nitatumia mbinu zangu nyingine kujaribu kufuatilia jambo hilo, tuone namna tunavyoweza kulimaliza vizuri zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Nilifikiri umetosheka, eeh, Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu mazuri.

(i) Kwa kuwa vijana karibu 750 wameachishwa kazi; na kwa kuwa michango yao ya *NSSF* haijapelekwa; na kwa kuwa mikataba imekiukwa na mwekezaji amempa mwekezaji mwingine; je, Serikali ipo tayari kuunda Tume Maalum kuhakikisha maslahi ya Wananchi wale yanapatikana kwa jasho lao lililopotea?

(ii) Kwa kuwa inaonekana hata baadhi ya wanaume wanasema urijali wao umekuwa na matatizo kutokana na dawa zilizokuwa zinatumika kwenye shamba kule; je, Serikali ipo tayari kuwasaidia katika hilo? (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani tatizo la Kisarawe umelieleza limeeleweka vizuri sana. Ninakuomba utupe muda tulifanyie kazi tuweze kupata suluhu ya namna tutakavyolitatua na ndiyo maana nimesema utuachie.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliahidi hapa Bungeni kulipatia ufumbuzi tatizo la mgogoro wa Umeya Arusha, lakini maelekezo uliyoyatoa kwa barua kwa Msajili hayajatekelezwa kwa kiwango cha kutosha kwa upande wa pili, hali ambayo imechangia matatizo ya Arusha na kuendelea mpaka hivi sasa.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu utafahamu kwamba, sote tunaheshimu sana Mahakama na hatuna dhamira ya kuingilia Uhuru wa Mahakama; na kwa kuwa utafahamu kwamba matukio ya Arusha ni pamoja na Mkuu wa Mkoa kuingilia baadhi ya kazi za Kimahakama; ningependa kupata kauli kutoka kwako; kwa kuwa Viongozi wa Jeshi la Polisi jana usiku wamekubaliana na Viongozi wa Kitaifa wa Chama ili tusitishe maandamano kwa lengo la kukaa nao mezani; na kwa kuwa sisi tumeshatoa kauli ya kusitisha maandamano nchini:-

Je, upo tayari kama Waziri Mkuu kwa *spirit* ile ile ya ahadi yako ya awali kuongeza nguvu kwenye majadiliano haya yaliyokwama ili kuinusuru hii hali ambayo imeanza kusambaa nchi nzima sasa ya udhalilishaji na uvunjaji wa haki za msingi? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Ndugu Mnyika anazo taarifa ambazo mimi kwa bahati mbaya sina; kwamba Viongozi pale Mkoani wamekubaliana na Viongozi ngazi ya Taifa kwa haya maelezo uliyoyasema. Kwa bahati mbaya sina na kwa hiyo, sina la kusema katika eneo hilo. (*Makofi*)

Kwa upande wa pili ni kweli nilichofanya nilidhani kingesaidia kupata ufumbuzi wa tatizo la Arusha. Siyo la Kiserikali kwa sehemu kubwa, nilidhani zaidi ilikuwa ni masuala ya kichama, ndiyo maana nikamwambia Msajili awasiliane na Vyama vinavyohusika, waone mgogoro uo katika sura gani, wakiafikiana kwamba upo mgogoro, wakutane wazungumze kwa lengo la kupata suluhu ya kisiasa. Sasa nimeona nakala ya barua ambayo imetoka upande wa Chama cha Mapinduzi kwenda kwa Msajili kwamba, katika hili hawaoni la kuzungumza, lakini kama yapo maeneo mengine ambayo bado upande wa CHADEMA wanaona ni vizuri yakazungumzwa, wapo tayari, lakini yawasilishwe yaelezwe ili waweze kuona mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, ninaamini dhamira bado ipo kwa maana hiyo. Kama yapo maeneo ambayo yanaonekana dhahiri kisiasa, ninafikiri ni vizuri Vyama vikakaa pamoja na kuzungumza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa suala hili sasa limevuka mipaka ya Vyama na kuwa suala la Kitaifa ambalo limeanza kusambaa maeneo mbalimbali ya nchi; na kwa kuwa ulilitambua hilo ndiyo maana ukaandika barua ya maelekezo uliyoyatoa; je, baada ya kupokea majibu kutoka kwa Chama cha Mapinduzi upo tayari sasa kutoa maelekezo ama ushauri mwingine ili upande wa pili ujue hatma ya suala hili na tujue hatua za kuchukua?

**WAZIRI MKUU:** Aaah, kwanza, tusikuze sana jambo hili kwamba, limesambaa nchi nzima; wapi Mnyinka? Siyo kweli, mmh! (*Makofi*)

Kikubwa hapa ninachokiona mimi katika mazingira ambayo ninayaona wenzangu ninyi wa CHADEMA mnafanya, unajua kinachohitajika hapa ni *goodwill* pande zote mbili. Kwa namna mambo yenu mnavyoyafanya, huoni dhamira kwamba watu hawa kweli mkae na kupata suluhu, maana ninyi staili yenu ya maandamano kila mahali, unajua sisi tulioko serikalini tunapata taabu sana; tunataka tufanye kazi nyingine ambazo tunahitajika, lakini muda wote unakaa unafikiria maandamano. *(Makofi)*

Mimi ninadhani kinachohitajika ni kujaribu kuteremka chini kidogo, tuanze kuona maslahi mapana ya nchi, tuone ni mambo gani ya msingi yanahitajika ili kwa pamoja tuweze kwenda mbele. Mimi kweli kabisa hii hali ya uanaharakati inanipa tabu sana, lakini kama umakini utakuwepo, sioni tatizo hata kidogo watu kukaa na kuzungumza masuala. Katika hali ninayoiona, *people's power* kila kukicha, *it doesn't give us a solution at all.* Haiwezekani! *(Makofi*)

Kwa hiyo, ninadhani kwa sehemu kubwa ni changamoto. Changamoto kwenu kwa upande huo na changamoto kwa Chama cha Mapinduzi kuona sasa hivi unapokuwa na hali hiyo hivi unafanyaje! Ninadhani mtihani mkubwa tu, lakini ukiniuliza mimi ninasema kwa kweli tunahitaji kubadilika kidogo ili muweze kutupa na sisi wenzenu imani kwamba, chama hiki makini sasa kipo tayari kwa ajili ya kutatua matatizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ninapenda nitumie nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna ulivyojibu maswali. Ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, kwa namna mlivyouliza maswali. Ninasikitika sana, Mheshimiwa Diana Chilolo, amekosa nafasi lakini atapata siku nyingine.

Ahsante sana. Katibu kwa hatua inayofuata. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 31

**Wabunge wa Viti Maalum Kuwezeshwa**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI)** aliuliza:-

Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa ni wadau wakubwa katika kuunda vikundi vya Wajasiriamali na kuviendeleza vilivyopo na kwamba Wabunge hawa hawana nyenzo za kutosha kama vile Mfuko wa Jimbo *(CDCF)* ambao ungewasaidia kuendeleza kazi hiyo:-

(a) Je, kwa nini Serikali haiwatumii Wabunge hawa kwa kuwapatia fungu maalum la kuendeleza kazi wanayofanya?

(b) Je, Serikali inasemaje kuhusu fungu la Wajasiriamali linalokwenda kwenye Halmashauri chini ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ambalo halitumiki ipasavyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote wana wajibu wa kuwahamasisha Wananchi kutumia fursa zilizopo ili wajikwamue kiuchumi. Fedha za Mfuko wa Jimbo zimetungiwa Sheria yake na zimesaidia kuongeza ari na hamasa katika Miradi ya Maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi ambayo sisi sote tunaishi.

Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum, watumie nyenzo zilizopo katika kuhakikisha wanawafikia Wanavikundi na Wajasiriamali popote walipo. Ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge hawa kwa kazi hii kubwa wanayoifanya wakishirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na Madiwani.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna fungu la fedha linalotolewa na Serikali kwenda kwenye Halmashauri chini ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kutoa mikopo ya Wajasiriamali, isipokuwa upo Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ambao unaratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwenye Halmashauri zote nchini na Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati ya Mikopo. Mfuko huo umetumika vizuri, ambapo umewawezesha Wanawake wengi wenye kipato cha chini kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kupanua biashara zao. Aidha, Serikali imeweka utaratibu wa kuziachia Halmashauri zote asilimia kumi ya riba inayotozwa kwa wakopaji zitumike kufuatilia utendaji na uboreshaji wa shughuli za Mfuko huo kwa maslahi ya Wanawake na Wajasiriamali nchini.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nina- *declare* kwamba, swali hili lilivyokaa nitakavyouliza pengine si kwa matakwa ya aliyeliandika, lakini hata hivyo, nina swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Jimbo upo kwa mujibu wa Sheria na maelezo ya namna ya matumizi ya Mfuko ule yaliwekwa wazi; na kwa kuwa sasa umekuwa ukitumika kwa ajili ya kuwezesha vikundi tu; Serikali inasema nini juu ya jambo hilo kwa sababu haiwekwi vizuri kuonekana kwamba ni kwa ajili ya ku-*support* vikundi na si Miradi ya Maendeleo kama ambavyo imeelezwa katika Sheria; na je, Serikali ina *position* gani katika ufafanuzi wa jambo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Sheria inasema nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Sheria hii ukiisoma vizuri, kazi yake hasa ni kuamsha ari au kuunga mkono jitihada za maendeleo za Wananchi. Kwa hiyo, Sheria inaruhusu ku-*support* Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi unaweza ukachangia Miradi ya Maendeleo inayoendelezwa katika maeneo ya Jimbo na Wananchi. Kamati ya Wilaya inayohusika inaweza ikaona busara ya kuchangia Miradi ya Maendeleo. Hakuna kizuizi, fedha hizi hasa ni kichocheo cha maendeleo. Hii ndiyo hasa nia ya Mfuko na nia ya fedha hizi ni kichocheo cha maendeleo na siyo vinginevyo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Serikali inatambua juhudi za Wabunge wa Viti Maalum huko mikoani; na kwa kuwa Wabunga hawa hawana Mfuko wa Jimbo na Serikali ilikiri kwamba itaendelea kulifanyia kazi

jambo hili; je, kwa wakati tulionao hawaoni kwamba sasa kuna kila sababu ile asilimia kumi inayotoka kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto sasa Wabunge wa Viti Maalum wawe Wenyeviti wa kugawa zile fedha badala ya Mkurugenzi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, angalau leo ninashukuru Mheshimiwa Diana Chilolo, amefahamu kwamba Mfuko huu ni Mfuko wa Jimbo, maana amemjibu mwuliza swali la msingi kwamba Mfuko huu kwa Sheria yake ni Mfuko wa Jimbo. Kwa sheria hii maana yake unahusika na Wabunge wa Majimbo.

La pili ni kwamba; Kamati zinazohusika na fedha hizi za Maendeleo ya Jamii katika Wilaya, sisi Waheshimiwa Madiwani na wala siyo ninyi akinamama peke yenu, hata sisi, wote ni Wajumbe wa Kamati hizi. Mheshimiwa Diana Chilolo ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa hiyo, kama unashiriki vizuri katika Kamati inayohusika, bahati mbaya pengine inakuwa ngumu kwako kwa sababu mnazo Wilaya nyingi, maana ninyi wenzetu mnafanya kimkoa. Pale kwenye Wilaya ambayo umeamua kushiriki, wewe ni Mjumbe na una uwezo wa kusimamia zile fedha kikamilifu, kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ile.

Na. 32

**Shule za Kata Nchini**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

(a) Je, kuna Shule ngapi za Kata zilizojengwa mwaka 2006 – 2010?

(b) Je, kati ya Shule hizo ni ngapi zenye walimu wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imeendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuendeleza ujenzi wa Shule za Sekondari katika Kata zetu kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau mbalimbali. Mafaniko yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za kujiunga na Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi waliohitimu Elimu ya Msingi. Aidha, mwaka 2006 zilikuwepo Shule za Sekondari za Serikali 1,690, hadi kufikia mwaka 2010 ziliongezeka shule 1,707 na kufanya jumla ya Shule zote kuwa 3,397. Mwaka huu wa 2011, Shule za Sekondari za Serikali zipo 4,325, zikiwemo za Kitaifa 88 na za Wananchi 3,337.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwepo kwa upungufu wa walimu katika Shule za Sekondari nchini, zikiwemo Shule za Kata hususan zilizopo maeneo ya pembezoni. Mwaka 2006, Shule za Sekondari nchini zilikuwa na jumla ya walimu 13,448 na mahitaji halisi ya walimu kwa sasa ni walimu 81,800. Waliopo katika Shule za Sekondari ni 44,573 na shule zote kwa ujumla zina upungufu wa walimu 37,227.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia tatizo la walimu, Serikali inaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali kuongeza udahili katika Vyuo vya Ualimu, kufungua Vyuo Vikuu, kusisitiza kila Chuo kuwa na Kitivo cha Elimu na kuajiri walimu wanaohitimu kulingana na ufaulu. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Serikali ilipanga kuajiri walimu 9,226 katika Shule zote za Sekondari nchini na mwaka 2011/2012, mwezi Desemba, Serikali inatarajia kuajiri Walimu wa Shule za

Sekondari 13,636; wa Shahada 6,649 na Stashahada 6,987; na hivyo kuwezesha kila Shule kupata walimu wanne kutoka kwenye idadi hiyo.

Serikali itaendelea kuajiri walimu ili kukidhi mahitaji kadiri wanavyohitimu na kufaulu kwao. Kwa sasa asilimia 55 ya Shule za Sekondari nchini, zina walimu wa kutosha. Serikali inaendelea na mkakati wa kutoa kipaumbele cha kupanga walimu katika maeneo ya pembezoni badala ya maeneo ya Jiji, Manispaa na Miji pamoja na kuhimiza Halmashauri kupunguza mlundikano wa shule sehemu za mijini.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Waziri ameeleza shule nyingi ambazo zimejengwa na zimeenea katika maeneo mengi; je, anayo habari kuwa katika baadhi ya hizo Shule zipo ambazo zina wanafunzi wanne tu katika darasa la kumi na mbili; katika mazingira hayo hivi hiyo shule unapaswa kuisimamia na ukaitetea kuwa ni Shule ya Sekondari na ina tija kwa Wananchi? Hilo la kwanza.

(ii) Ninapenda nikwambie kuwa medali ya dhahabu moja ina thamani kuliko shilingi 100. Tatizo kubwa linalofanya Shule hizo za Sekondari kupelekea wanafunzi wengi kufeli ni walimu. Walimu wana mambo mengi ambayo wanaidai Serikali, wana madai yao mengi ambayo Serikali kila siku inajaribu kuwapiga danadana. Hivi ni lini sasa walimu watalipwa fedha zao ili waweze kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza la suala la Mheshimiwa Khalifa ni kweli kwamba, zipo baadhi ya Shule za Sekondari zina wanafunzi wachache sana madarasani. Nimefanya ziara Wilayani Kondoa, nimekwenda kwenye shule moja nimekuta Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne wapo wanafunzi 140. Hii inadhihirisha kwamba, idadi ya wanafunzi kwenda darasa moja ni ndogo, lakini maamuzi ya ujenzi wa Shule hizi kwa wingi wake zilifanywa na Halmashauri zenyewe.

Maelekezo ya Serikali katika ujenzi wa shule hizi, ilikuwa waangalie eneo la Kata kama linatosha kuwa na wanafunzi wengi wa kutosha kulingana na Shule za Msingi zilizopo na ambazo zinaweza kutoa idadi kubwa ya wanafunzi ili kuweka Sekondari yake. Kwa sasa kwa kuwa bado tunaamini kuna vijiji vingi vinaendelea kuwepo na Vitongoji vyake na idadi ya wanafunzi ya ufaulu inaongezeka kwa Shule za Msingi, tunaamini shule hizi ambazo zina idadi ndogo ya wanafunzi, wanafunzi wake wataongezeka, lakini wajibu wetu Serikali ni kuendelea kupeleka walimu na kuendelea kuwafundisha vijana wale wapate elimu iliyokusudiwa.

Swali la pili kuhusu tatizo la madeni ya walimu; tumelieleza mara nyingi lakini ninataka nikuhakikishie kwamba, sasa tumefika mahali pazuri, kwa sababu tumeshafanya uhakiki baada ya Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Bunge la Julai kueleza matatizo ya walimu kwenye eneo la madeni. Serikali imefanya jitihada kubwa, Tume zilizoko katika kila Halmashauri zilizojumuisha Maafisa Elimu, Idara ya Utumishi, Katibu TSD na Chama cha Walimu kinachoshughulikia haki za walimu, kukaa pamoja kupitia madeni yote na tayari takwimu zimeshapatikana zitaletwa kwetu, lakini ulipaji utafanywa wakati wowote baada ya taratibu zilizokamilishwa juzi na timu ya Makatibu Wakuu wakiwemo Chama cha Walimu kukamilika. Kwa hiyo, suala la madeni ya walimu kuhusu suala la malipo yao ni wakati wowote kuanzia sasa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa miongoni mwa sababu zinazosababisha kuzorota kwa taaluma katika Shule hizi za Kata ukiachilia mbali uhaba wa walimu ni ukosefu wa maabara kwa masomo ya sayansi. Je, Serikali ipo tayari sasa katika mwaka ujao wa fedha kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa *mobile* maabara ili kuzipeleka katika Shule hizo na kunusuru wanafunzi wanaofeli hasa Masomo ya Sayansi waendelee kufaulu katika masomo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Shule zetu za Sekondari zina upungufu wa maabara, lakini kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), tumeshatenga bajeti kwa ajili ya kujenga

maabara mbili katika kila Halmashauri na tayari wataalam wameshakwenda katika kila Halmashauri kubaini ni shule zipi zitapata maabara zile mbili katika Halmashauri. Wakati huo huo, Serikali nayo inaendelea kuona umuhimu wa kuongeza maabara katika shule mbalimbali kadiri fedha zinavyopatikana.

Mpango wa *mobile laboratories* ambazo tulishaziona hapa mwezi Julai, kwa nafasi hii ninapenda niwapongeze Wabunge ambao tayari wameshaanza kununua zile maabara kwa shilingi milioni tano na kusambaza kwenye maeneo yao. Mkakati wa Serikali ni kupeleka maabara zilizokamilika, zenye vifaa thabiti na hivi sasa tunajipanga kutenga fedha tupate maabara zilizokamilika kwenye Shule zetu za Sekondari.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inafahamu kwa muda mrefu matatizo mengi katika shule zilizopo pembezoni na hii imesababisha taaluma kushuka na tofauti kubwa sana ikatokea kati ya taaluma katika miji na shule za pembezoni. Je, ni lini Serikali itanyanyua taaluma za shule zilizoko pembezoni ili wafanane na wanafunzi wa nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi, nimezungumzia mkakati wa Serikali wa kusambaza walimu na kuimarisha utoaji wa elimu kwa shule za pembezoni baada ya kupeleka walimu kwenye maeneo haya.

Tulipokuwa tunapanga ajira hii mpya ambayo itafanyika mwezi wa Desemba, kati ya mambo ambayo tumeyazingatia ni utafiti uliofanywa na wataalam wetu wa mahitaji halisi ya walimu kwenye shule za pembezoni zaidi kuliko zile za mijini. Tutakapotoa orodha yetu, utakuta kwamba, eneo kubwa ambalo tumepeleka walimu zaidi ni zile Halmashauri za Wilaya za pembeoni ukiacha zilizoko kwenye Manispaa.

Bado tumetoa maagizo kwa Maafisa Elimu wa Sekondari wahakikishe wanapeleka walimu kwenye shule za pembezoni katika kila Halmashauri badala ya kulundika katikati ya Makao Makuu ya Wilaya, ambayo sisi tunaamini yanaweza kupata walimu kwa kuhamia au kwa ugonjwa. Maeneo yote ya miji yanakuwa na walimu wengi. Kwa hiyo, tunaamini kule pembezoni sasa kutakuwa na walimu na hiyo ndiyo njia pekee itakayosaidia kuweka usawa wa kitaaluma kwa kuwa wakipata walimu watafundisha kama ambavyo walimu wengine wanafundisha.

Na. 33

**Sheria na Kanuni za Ajira Kuangaliwa Upya**

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Baadhi ya Watendaji wa Serikali na Taasisi zake wamekuwa na tabia ya kutotimiza majukumu yao kwa uaminifu:-

Je, Serikali haioni kuna umuhimu kwa kuangalia upya Sheria na Kanuni za Ajira Serikalini na kutoa adhabu kwa wanaokiuka Sheria hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi katika Utumishi wa Umma huongozwa na Sheria, Kanuni na Taratibu ambazo huweka utaratibu wa ajira ili kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kuajiriwa na kuweka utaratibu wa kupima utendaji kazi ili kuhakikisha wanatimiza majukumu yao kwa uaminifu. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002 na Kanuni

zake za Mwaka 2003, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni zake, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za Mwaka 2005, Sheria ya Utumishi wa Bunge ya Mwaka 2008, Sheria ya Utumishi ya Jeshi la Polisi na Magereza ya Mwaka 1990 na Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Sheria, Kanuni na Taratibu hizi pia zimewekewa utaratibu wa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo. Baadhi ya adhabu zinazotolewa kwa watumishi wanaothibitika kutenda hayo ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo, kushushwa mshahara, kuzuiwa nyongeza ya mshahara ya mwaka, karipio, onyo au kufunguliwa mashtaka ya jinai, kutegemeana na makosa yanayofanyika.

Mheshimiwa Spika, endapo kuna watumishi wasiotimiza wajibu bila kuchukuliwa hatua ni kasoro za usimamizi na si Sheria, Kanuni na Taratibu, kwani pale inapoonekana kuwa Sheria na Taratibu zilizopo zina kasoro, Serikali huzifanyia marekebisho ili kuleta ufanisi.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

(i) Kwa kuwa kumekuwa na mtindo wa Watendaji wengi Serikalini kutotimiza wajibu wao katika utekelezaji wa kazi zao. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwapa ajira kwa mkataba ambapo ikiwa atavunja mkataba ule kwa wakati husika na kwa kazi aliyopewa awajibike badala ya kumpa uhamisho au kumpunguzia mshahara?

(ii) Kwa kuwa Serikali imekuwa na mtindo wa Idara mbalimbali za Serikali kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi zao kwa maonesho kwenye Viwanja vya Maonesho kama Mnazi Mmoja na sehemu nyingine; na kwa kuwa ni maonesho ya uhalisia tofauti; je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuweka utaratibu mwingine wa kupima utekelezaji wa shughuli zao kwa vitendo badala ya maonesho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, suala kwa nini Watumishi wa Umma wasipewe mikataba ili waweze kuwajibika; kama nilivyotangulia kusema, Sheria na Kanuni zipo, kwa hiyo, kwa hivi sasa, hatuoni sababu ya kuwapa mikataba ndani ya Utumishi wa Umma ili waweze kuwajibika. Tunao utaratibu wa kuwapima Watumishi wa Umma kwa kuweka nao makubaliano ya kazi zipi watazifanya ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na tunawapima wametekeleza kwa kiasi gani na pale ambapo inabainika kwamba hawakufikia malengo ambayo tumewekeana, hatua za kinidhamu zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, pia hatukumia Maonesho ya Utumishi wa Umma kwa kupima utendaji kazi wa watumishi wetu. Badala yake tunatumia Maonesho yale kupata mrejesho kutoka kwa Wananchi ili watueleze kwa kiasi gani wanatuona tunatekeleza majukumu yetu. Pia tunayatumia kuelezea majukumu tunayoyafanya na kuchukua kero kutoka kwa Wananchi ili tuweze kuweka katika mipango yetu ya mwaka unaofuatia.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Watendaji wengi wa Serikali hasa katika ngazi za Halmashauri wanakaimu kutokana na sheria ambayo mtu hawezi akathibitishwa kuwa Mkurugenzi au Mkuu wa Idara mpaka ametumikia katika Halmashauri miaka saba na kupelekea Halmashauri nyingi kuzorota kwa kushindwa kufanya kazi kwa hawa watu ambao wanakaimu. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kurekebisha sheria hiyo ya kupunguza muda wa kutumikia Halmashauri kutoka miaka saba ya sasa angalau mpaka miaka miwili kwa sababu kila mwaka Halmashauri hizo zinakaguliwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, hatufikirii kubadilisha muda wa mtumishi kuchaguliwa kuwa Mkuu wa Idara au kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Kama alivyopendekeza yeye, mtumishi ametoka Chuo Kikuu au Chuo chochote, ameanza kazi, ndani ya miaka miwili unampa Ukurugenzi au Ukuu wa Idara; kwa kweli ni kutaka kuziua Halmashauri.

Suala la mtumishi kuteuliwa kuwa Mkuu wa Idara si lazima atoke kwenye Halmashauri hiyo hiyo. Kama Halmashauri husika haina mtumishi ambaye amefikisha miaka saba ambayo anaweza akapewa Ukurugenzi au Ukuu wa Idara, basi wanatakiwa watoe taarifa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ili waweze kuwatafutia watumishi ambao wana uwezo na sifa za kuweza kupewa Ukuu wa Idara. Lengo la kuweka hiyo miaka saba ni kuhakikisha kwamba, wanapata uzoefu wa kutosha kutokana na utendaji wao wa kazi wa siku hadi siku. Kwa kuwa mtumishi hawezi kupata uzoefu chuoni au mahali popote, anaupata kwa kufanya kazi na kukumbana na changamoto mbalimbali; kwa hiyo, ninapenda nikwambie Mheshimiwa Kiwanga kwamba, miaka miwili haimtoshi mtu kukomaa, hata sisi wenyewe humu ndani, ndani ya miaka miwili bado unahitaji kuendelea kujifunza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Na. 34

**Taratibu za Kuhamisha Wafanyakazi**

**MHE. DONALD K. MAX** aliuliza:-

Je, taratibu za mfanyakazi yeyote kutolewa sehemu moja kupelekwa sehemu nyingine zina vikwazo vingi kiasi gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uhamisho wa watumishi kutoka kwa mwajiri mmoja kwenda kwa mwingine umefafanuliwa katika kifungu namba 8(3)(f) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 18 ya Mwaka 2007, ikisomwa kwa pamoja na Kanuni Na. 107 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003 na aya namba 13(k) ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za Mwaka 2003, ambapo Katibu Mkuu (UTUMISHI), amepewa mamlaka ya kuhamisha watumishi yeye mwenyewe au kwa kukasimu madaraka haya kwa waajiri wengine kulingana na umuhimu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, mtumishi kutolewa sehemu moja kupelekwa sehemu nyingine, hufanyika ili kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika Utumishi wa Umma. Uhamisho wa watumishi kutoka sehemu moja kwenda nyingine, hutekelezwa kwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuwepo kwa nafasi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha husika, sehemu ambayo mtumishi husika anategemea kuhamishiwa, inaweza kutokana na kibali cha ajira mpya/mbadala au mtumishi aliyekuwepo kuhitimisha utumishi wake kwa kustaafu, kuacha kazi au kufukuzwa kazi au kufariki.

(b) Kuwepo na sababu muhimu zenye kumlazimu mtumishi kuhama kama vile kumfuata mwenzi wa ndoa au sababu za kiafya ambazo zimethibitishwa.

Hivyo, suala la mtumishi kutolewa sehemu moja kwenda nyingine, halina vikwazo. Kinachotakiwa ni kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, kuna matatizo ambayo yanajitokeza hasa kwenye Halmashauri zetu; vikwazo vipo kwa sababu kuna malalamiko mengi tumeshayawasilisha Wizarani, ambayo mpaka leo hayatatuliki. Kwa mfano, kuna watu wamehamishwa wameletwa na sasa hivi wana miaka saba hadi minane hawajalipwa mafao yao. Kwa mfano, Wilaya ya Geita mpaka leo inadai shilingi milioni 484, watu wamehamishwa tangu mwaka 2003, 2006 na 2007, sasa kidogo inatusumbua ndiyo maana ninasema kuna vikwanzo vya aina fulani ambavyo vinawafanya utendaji wa watumishi kuwa mbaya ni kwa sababu haki zao hazilipwi.

Sasa swali langu ni kwamba; nimeshaleta malalamiko hayo sasa hivi ni miezi sita hakuna hata shilingi iliyoletwa, kila ukirudi Jimboni swali ni hilo hilo. Je, Wizara ipo tayari kutusaidia kutatua matatizo haya kwenye Wilaya ya Geita?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la haki za watumishi wanaohamishwa kwenda maeneo mbalimbali, mtumishi anapohama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, sehemu anayohamia ndiyo inayowajibika kumlipa stahili zake za kuhamia pale. Kule anakotoka wao wanapaswa kumlipa stahili za usumbufu. Suala analolizungumzia Mheshimiwa Max nimeliona, amelileta kwangu lakini katika kulipitia haraka haraka, Wilaya yake ya Geita pia inao upungufu wake.

Kwa sababu ukiangalia tangu mwaka 2003, Serikali imekuwa ikipeleka pesa nyingi sana katika Halmashauri za Wilaya ambazo watumishi waliohamishwa wenye stahili mbalimbali zimekuwa zikitolewa. Kwa kuangalia tu zile za kwao, niliona niwape wataalam wangu waweze kufanyia kazi. Kwa kuwa hivi sasa tunafanya uhakiki wa madai mbalimbali ya watumishi na hilo suala lake linashughulikiwa kwa pamoja.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao tunahudhuria katika vikao mbalimbali katika Halmashauri, hebu tuwe tunauliza kila tunapokaa vikao ni pesa kiasi gani zimeletwa kama *OC* kwa ajili ya stahili mbalimbali za watumishi wetu na zimelipwa kaisi gani na kila siku tuwe tunafahamu madeni yaliyopo. Serikali imekuwa ikipeleka pesa katika maeneo yetu, lakini bado zile pesa hazitumiki kwa shughuli ile, badala yake tunaendelea kuzalisha madeni siku hadi siku.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, zamani kulikuwa na utaratibu, Serikali inapopeleka hela kwenye Halmashauri, Wabunge wanapewa nakala yake kwa vipindi fulani; kwa nini msiendelee na utaratibu huo? Mheshimiwa Mkosamali swali lingine la nyongeza liwe fupi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Ninapenda kufahamu ni utaratibu gani unaotumika kuhamisha wafanyakazi ambao wana makosa ya kinidhamu kwa sababu baadhi ya wilaya zilizoko pembezoni kama Kibondo zimekuwa zinapewa wafanyakazi wanaojifunza au wenye makosa sana waliyokosa sehemu zingine; ni taratibu gani zinatumika kufanya hivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, Serikali haina utaratibu wowote wa kumhamisha mtumishi mwenye makosa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Tumeshatoa Waraka kabisa kwamba, itakapobainika kwamba mtumishi amehamishwa na ana makosa, basi watoe taarifa ili arudishwe kule alikofanya kosa aweze kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kinachojitokeza wakati mwingine, uhamisho unapotolewa wanakuwa hawana taarifa za mtumishi kama eneo ambalo lipo kuna kosa amelifanya na hivyo hastahili kuhamishwa. Pale ambapo taarifa inatolewa, mtumishi huyo ana makosa, uhamisho huo huwa unafutwa.

Suala la kusema kwamba Kibondo wanapelekwa watumishi wanaokwenda kuanza ni kila Wilaya na kila Mkoa watumishi wanapelekwa. Mfano sasa hivi tunazungumzia walimu ambao wanatoka vyuoni ni lazima watagawiwa katika wilaya zote kwa sababu kuna watumishi wanafariki na tunaajiri kila siku. Kwa hiyo, lazima kutakuwepo watumishi wapya wanaopelekwa kufanya kazi katika maeneo yote.

Na. 35

**Maandalizi ya Sensa**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR** aliuliza:-

Taarifa kuhusu idadi ya watu na kaya ni mahitaji muhimu katika uandaaji wa mipango endelevu ya Taifa:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika maandalizi ya sensa ya watu inayotarajiwa kufanyika mwaka 2012?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepangwa kutumika kwa kazi ya sensa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi yamefanyika kama ifuatavyo:-

(i) Kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu inaendelea vizuri. Hadi sasa kazi hiyo imekamilika katika mikoa 19, ambayo ni sawa na asilimia 85 ya kazi yote. Kazi hii imepangwa kumalizika mwezi Februari, 2012.

(ii) Kazi ya kuweka ramani katika mfumo wa kidigitali inaendelea kufanyika kwa kushirikiana na wadau, kazi hii itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2012.

(iii) Kazi ya kuandaa rasimu za dodoso la sensa pamoja na miongozo ya makarani na wasimamizi imekamilika.

(iv) Sensa ya Majaribio ilifanyika tarehe 2 Oktoba, 2011 katika mikoa 11 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo kuu la sensa ya majaribio ni kupima kama uwezo wa kitaalam na mfumo wa uongozi unawezesha sensa ya watu na makazi kufanyika ifikapo Agosti, 2012.

(b) Mheshimiwa Spika, Sensa ya mwaka 2012, kiasi cha Tshs. 114.4 bilioni zitahitajika katika kipindi chote cha Sensa, kuanzia maandalizi, kuhesabu watu, uingizaji takwimu kwenye kompyuta, uchambuzi na utoaji wa taarifa zote za sensa.

(c) Mheshimiwa Spika, kimsingi, jukumu la kugharimia sensa ni la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, wadau wa maendeleo walishachangia asilimia 23 ya bajeti nzima ya sensa na asilimia 77 zilizobaki zitagharimiwa na Serikali ili kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 inafanyika kama ilivyopangwa.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa sensa ndiyo nyenzo muhimu kwa Taifa lolote na ndiyo kigezo cha kujua vipi watasaidia au kuleta maendeleo ya Wananchi wake:-

(i) Je, kwa wanafunzi watakaokuwa nje ya nchi kwa wakati huo wa sensa na wafanyabiashara watakaokuwa kwenye shughuli za kikazi nje ya nchi na hata wafanyakazi wenyewe baadhi yao watakuwa kwenye ziara au kwenye ofisi za kibalozi nje ya nchi hii; Wizara yako itachukua hatua gani ili na wao wajumuike katika sensa hii?

(ii) Sensa ambayo ili iwe na mafanikio sahihi inahitaji uelewaji mkubwa wa kazi hii na umeeleza katika maelezo yako mama. Je, wafanyakazi watakaosimamia katika sensa hiyo watakuwa na elimu ya kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kupitia kwako ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kuuliza swali ambalo litawasaidia Watanzania wote na hata Wabunge, kuwaelewesha Wananchi juu ya maandalizi ya sensa hii. Utaratibu ni kuhesabu watu wote watakaoamkia siku ya sensa na ninaomba ifahamike kwamba, tarehe iliyopangwa ni tarehe 26 Agosti, 2012. Kwa hiyo, usiku wa kuamkia tarehe hiyo

ndiyo kila mtu atahesabiwa Tanzania. Watu watakaohesabiwa ni wa Tanzania, bila kujali kwamba ni raia au si raia, mradi tu utakuwa unaamkia siku hiyo ya tarehe 26.

Watanzania wanaoishi nje ya nchi, utaratibu umepangwa kwamba, wale ndugu zao ambao wapo hapa nchini, kufuatana na dodoso la sensa, watakuwa wanaeleza kuwa wapo ndugu zao wanaishi nje ya nchi na watafahamika jinsia zao na sehemu ambazo wanatoka. Sasa hii itasaidia sana kwa wote kufahamu kwamba sensa ya mwakani imeandaliwa vizuri na tuombe kwamba ifikapo tarehe hiyo wote tushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zoezi hili kuhitaji kufanywa kwa uangalifu mkubwa; kiwango cha watumishi ambao watashiriki sensa hii ni kikubwa na wataalam wa kuanza kuandaa rasimu na wanaoandaa dodoso la sensa wapo na ni makini sana. Vilevile wataalam ambao wataweka ramani ya maeneo ya sensa wapo. Kiwango cha elimu kinachotarajiwa kwa wataalam wote hawa ni shahada na shahada za uzamili na sehemu kubwa ya sensa hii itafanywa na Walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Endapo itaonekana kwamba Walimu hawa hawatatosha, basi Watumishi wengine wa Serikali wataombwa kushiriki katika sensa hii.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Matumizi mazuri ya rasilimali watu na fedha ni jambo la msingi sana katika kupanga mipango ya maendeleo. Kwa kuwa Mradi wa Vitambulisho vya Uraia na Mradi wa Sensa taarifa zake zinawiana; kwa nini Serikali ilishindwa kuoanisha Miradi hii mikubwa ambayo inatumia rasilimali nyingi ili kupunguza gharama za uendeshaji na pia kutumia vizuri rasilimali watu na fedha kwa kuiunganisha Miradi hii miwili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, kama alivyouliza kwa nini Serikali imeshindwa kuiunganisha Miradi hii miwili; ninafikiri la msingi hapa ni kufahamu kwamba, suala la sensa lipo peke yake; na kama nilivyoeleza hapa, suala la Vitambulisho vya Uraia ambalo mpaka sasa bado linafanyiwa utaratibu halijakamilika, kwa hiyo, kwa kuunganisha Miradi hii miwili kwa hivi sasa itakuwa vigumu. Kwa hiyo, tuangalie kazi ya sensa iliyopo mezani hivi sasa na suala la vitambulisho kwa sababu halijakamilika itabidi lingoje mpaka likamilike labda tutaunganisha masuala yote mawili.

Na. 36

**Shirika la Reli Kenya Kufikisha Huduma Moshi**

**MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO** aliuliza:-

Kuna reli iliyounganisha Miji ya Mombasa – Voi – Moshi – Arusha japo kwa upande wa Tanzania huduma ya reli imesitishwa na kusababisha bidhaa zinazotoka Mombasa kusafirishwa kwa njia ya barabara ambayo ni ghali na ina usumbufu mwingi:-

Je, kwa nini Serikali isiruhusu Shirika la Reli la Kenya kusogeza huduma hiyo mpaka Moshi ambayo ni kilomita 15?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mtandao wa reli uliojengwa tangu enzi za Mkoloni, unaziunganisha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Kwa upande Kenya na Tanzania, Reli ya Kenya inaunganishwa na Reli ya Tanzania kutokea Stesheni ya Voi iliyoko Kenya kuja Stesheni ya Kahe iliyoko Tanzania. Kutoka Kahe mpaka Moshi ni kilomita 20.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Reli ya Kenya ipo huru kusogeza huduma zake mpaka Moshi hapa nchini na hakuna kizuizi chochote cha Serikali. Fursa hii ya kibiashara inatokana na Mkataba wa Oktoba, 1998 unaoitwa *Tripartite Agreement,* kati ya Mashirika ya Reli yaliyokuwa ya Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda kabla ya ubinafsishwaji unaoruhusu Kampuni ya Reli kutoka

nchi moja kupeleka treni zake kwenye reli ya nchi nyingine. Hata hivyo, ili safari hizo za treni ziweze kufanyika, yapo masuala kadhaa ya kuzingatiwa yakiwemo miundombinu ya reli kati ya Vituo vya Voi na Kahe kufanyiwa matengenezo makubwa kutokana na kuharibika sana kulikosababishwa na mvua na kutokuwepo na matengenezo ya mara kwa mara kufuatia reli hiyo kutotumika kwa muda mrefu. Sehemu ya reli ya kuanzia mpakani mwa Tanzania hadi Taveta upande wa Kenya, imeng'olewa kabisa. Ili kurejesha huduma kati ya reli hii, Serikali ipo tayari kufanya mazungumzo na Serikali ya Kenya ili kuirejesha reli hiyo iliyong'olewa. Aidha, uamuzi wa kuanzisha safari kutoka Kenya kuja Moshi, utategemea pia namna ambavyo Kampuni hiyo ya Kenya itakavyoona fursa za kibiashara na hivyo kufanya kuwepo kwa haja ya kuwekeza katika kuboresha reli hiyo.

**MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru kwa majibu mazuri ambayo nimeyapata. Kwa kuwa kwa miaka zaidi ya kumi katika Bunge hili nimekuwa nikiipigania reli hiyo ifunguliwe lakini sikuwahi kupata majibu kama ya leo, pamoja na hayo ninayo maswali mawili madogo ambayo ningeomba nipate majibu:-

(i) Kwanza ikumbukwe kuwa Moshi ndiyo Mji wa Mlima Kilimanjaro; kwa hiyo utalii wowote wa kule *Northern Region*, Moshi ndiyo Mji unaotumika kupanda Mlima wa Kilimanjaro. Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi wa reli hii pamoja na kufufua *facilities* zilizopo Moshi na Arusha?

(ii) Je, ni fursa gani nyingine zitakazopatikana kutokana na uboreshaji wa reli hii?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

(i) Wizara kwa niaba ya Serikali itafanya ukaguzi katika Reli ya Moshi – Arusha mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge hili la Novemba, 2011 na Mheshimiwa Mbunge atataarifiwa na kukaribishwa katika ukaguzi huo. Aidha, mpango wa Serikali ni kufanya maboresho makubwa ya kujenga Reli ya Tanga – Arusha – Musoma. Hivyo, *facilities* zilizopo Moshi na kwingineko, zitaboreshwa katika mpango huo.

(ii) Mheshimiwa Spika, kutokana na kuboreshwa kwa kipande kinachounganisha Kenya na Mji wa Moshi, kutafungua fursa za utalii kwani idadi ya watalii wanaotoka Moshi kuelekea Arusha na Mombasa na kurudi wataongezeka kutokana na ukweli kwamba, abiria wengi hupendelea zaidi usafiri wa treni kwani ni salama zaidi kuliko usafiri wa barabara ambapo baadhi husababisha ajali nyingi.

**SPIKA:** Ninaona limezidi kuboreshwa hilo jibu kuwa zuri zaidi. Mheshimiwa Wenje, sijui na wewe unakwenda Moshi?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa treni ni muhimu sana na unatusaidia sana kusafirisha mizigo na watu kwa gharama nafuu. Sasa ni muda mrefu sana, reli inayounganisha kutoka Dar es salaam mpaka Mwanza haifanyi kazi. Nilipokuwa ninatoka kwenye Bunge la Bajeti, Mheshimiwa Waziri, ali-*present a very ambitious budget* na aliahidi kwamba, hii treni ingeanza kufanya kazi tena mapema. Mpaka sasa usafiri wa treni kuelekea Mwanza na kutoka Mwanza kuelekea Dar es salaam haupo. Ningependa nijue kutoka kwa Waziri kwamba treni ya kwenda Mwanza itaanza lini kazi?

**SPIKA:** Ahsante. Kwa nini usiulize hivyo toka mwanzo? Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi!

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna mipango ya kufufua siyo reli ya kwenda mpaka Mwanza tu, bali reli zetu zote; na siyo kuzifufua tu na pia kuziboresha katika kipindi cha miaka mitano hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli inayokwenda Mwanza, labda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kazi za kubeba mizigo, reli hiyo inafanya kazi. Ambacho hakifanyiki kwa hivi

sasa kwenye reli ya kutoka Tabora mpaka Mwanza ambayo ndiyo inaanzia Dar es salaam ni kubeba abiria, lakini inao uwezo wa kubeba mizigo na inafanya kazi.

Pamoja na hayo, bado tunafanya bidii reli hiyo iboreshwe. Mwaka jana tulikuwa na treni moja ya kwenda mpaka Kigoma, sasa hivi zipo mbili. Tumeshawahi kuidhinishiwa pesa za bajeti za kuboresha, sasa hivi tuko katika harakati za kuboresha hasa mabehewa pamoja na *locomotives,* vitu ambavyo havipo katika kufanya kazi hizo zianze tena kwa bidii zote. Kwa hiyo, tupo katika kulishughulikia hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, kwa niaba yake swali hilo atauliza Mheshimiwa Arfi.

Na. 37

**Ukiukwaji wa Kanuni za Bodi ya Kahawa Nchini**

**MHE. SAID A. ARFI (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Kanuni za Bodi ya Kahawa nchini, ni marufuku kahawa kuondolewa kutoka Mkoa wenye kiwanda cha kukoboa ikiwa ghafi; Bodi iliagiza kahawa ibanguliwe kwenye viwanda vilivyopo kwenye Mikoa ilikozalishwa na kuhifadhiwa, lakini Bodi hiyo imekuwa ikikubali kupokea kahawa kutoka Kigoma bila kubanguliwa na hivyo kuvunja Kanuni zake:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ukiukwaji huo ambao unahujumu Ushirika Mkoani Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zitto, ninamwombea Mheshimiwa Zitto na wote wanaougulia huko India, Mwenyezi Mungu abariki dawa zinazowahudumia.

Mheshimiwa Spika, sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kilimo cha kahawa kianze Mkoani Kigoma, kahawa yao ilisafirishwa kwenda kubanguliwa Mjini Moshi kwenye Kiwanda cha *Tanganyika Coffee Curing Company (TCCCO)*. Mwaka 2004/2005, Chama cha Msingi cha Ushirika cha Kanyovu kilijenga kiwanda chake cha kubangulia kahawa huko Matiyazo, ambacho kilikidhi ubanguaji wa kahawa yote ya Kigoma. Hata hivyo, baadhi ya Wanachama wa Kanyovu walijiengua kutoka katika Ushirika huo na kuunda Umoja wao kwa jina la *KACOFA.* Wilaya ya Kigoma ilitoa kibali kwa Wakulima, Wanachama wa *KACOFA,* kusafirisha kahawa yao kwenda kubanguliwa *TCCCO* Moshi. Hali kadhalika, *TCCCO* pia *KACOFA* wanapata huduma za mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ambao haupo Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda uasili wa kahawa, Bodi ya Kahawa Tanzania inasimamia na kuhakikisha kwamba kahawa hiyo ya KACOFA inauzwa kama kahawa ya Kigoma bila kuchanganywa na kahawa ya Kilimanjaro kwa kutumia mfumo maalum wa ufuatiliaji, yaani *traceability*.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wa Kigoma wanashauriwa kuanzisha mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na kupunguza gharama za uzalishaji katika kiwanda chao ili kuwavuta *KACOFA* sasa kurudi kukoboa kahawa yao Mkoani Kigoma.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayakukidhi swali lililoulizwa; swali lilikuwa Serikali inatoa kauli gani juu ya ukiukwaji wa taratibu za Bodi ya Kahawa, lakini Waziri ametoa maelezo na hakutoa kauli ya Serikali juu ya ukiukwaji huo.

(i) Hawa Viongozi wa Serikali wa Wilaya ya Kigoma waliotoa kibali kinyume na Taratibu na Kanuni za Bodi wanachukuliwa hatua gani?

(ii) Ikiwa hivyo ndivyo, je, sasa Wizara yako ipo tayari mahala popote pale wakulima wanapotaka kujitenga na Chama Kikuu cha Ushirika wanaweza kufanya hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba majibu yawe mafupi sana kwa sababu muda umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, suala la kahawa linatawaliwa na Sheria ya Kahawa ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake na utaratibu wake ni mrefu. Wadau wanaohusika hapo ni wengi na Halmashauri za Wilaya zinahusika.

Nimeeleza katika majibu yangu kwamba, Halmashauri ya Wilaya ndiyo iliyotoa kibali, nayo ina mamlaka yake ya kufanya hivyo. Pamoja na hayo, nikijibu kwa pamoja na swali la pili la wanaotaka kujiengua; Ushirika ni hiari, hakuna kulazimishwa kwamba wewe lazima uwe Ushirika huu; Sheria ya Ushirika ndivyo inavyosema. Sasa wale wanapoona kwamba hawaridhiki katika Ushirika huu, wapo huru kabisa kwa mujibu wa Sheria kutafuta wanakoona kuna *green pasture*.

Kwa hiyo, kwa maelezo yangu hayo, ninachotaka kusema ni kwamba, ukitazama vizuri, hakuna waliokiuka hapa, hakuna makosa makubwa yaliyofanyika. Wale baada ya kuamua kujitenga, Halmashauri ilisoma Sheria ikaona hapa tunaweza tukawaruhusu wakaenda na wakakuta mambo ni mazuri kule. Sasa ninachosema ni kwamba, kule Kigoma tuboreshe utaratbu huu, tuweke utaratibu wa stakabadhi ghalani, tuwavutie *KACOFA* waweze kurudia kukoboa kahawa yao. Msimamo wetu ni huo kwamba, kahawa ikobolewe katika eneo inapozalishwa ili kuweza kuwanufaisha wakulima.

Na. 38

**Utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza**

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Serikali katika kuelekeza Mpango wa Kilimo Kwanza imekuwa ikiagiza matrekta mengi *(power tillers)* pikipiki na kadhalika:-

(a) Je, Serikali imejiandaaje kupata vipuri *(spare parts)* za vifaa hivyo hasa ikitiliwa maanani kuwa vifaa hivyo vinaagizwa kutoka nchi mbalimbali kama vile India China, Korea na kadhalika?

(b) Suala la Kilimo Kwanza linahusisha mambo mengi kama vile wataalam, mbolea, mbegu bora, skimu za umwagiliaji na kadhalika; ni lini Serikali itawatambua na kuwatumia wataalam wetu wa kilimo badala ya kuendelea kutumia wataalam kutoka nje?

(c) Je, Serikali itaendelea kuagiza mbolea na mbegu kutoka nje mpaka lini badala ya kufufua viwanda au kujenga viwanda vipya vya mbolea na kuimarisha vituo vyetu vya utafiti na uzalishaji mbegu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, inahimiza matumizi ya zana bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija, sambamba na uingizaji nchini idadi kubwa ya matrekta makubwa na madogo unaotekelezwa na wadau mbalimbali wa kilimo. Aidha, Wizara

ya Kilimo, Chakula na Ushirika, imeandaa mwongozo wa viwango vya ubora wa matrekta yanayoingizwa nchini pamoja na vipuri vyake. Mwongozo unawataka wasambazaji wa matrekta kuwa na wataalam wa kutoa mafunzo kwa watumiaji wa matrekta kufuatilia utendaji kazi wa zana hizo na kutoa *guarantee* ya mwaka mmoja au zaidi, ambayo itamlinda mnunuzi kutokana na matatizo ya kiufundi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inawatambua na inawatumia Wataalam wa Kilimo wa ndani. Kwa mfano, mwaka 2007 walikuwepo wataalam 3,379. Kufikia Juni, 2011 idadi hiyo iliongezeka na kufikia 5,181. Mwaka huu Wizara imepata kibali cha kuajiri wataalam wengine 4,499.

(c) Mheshimiwa Spika, jitihada za kujenga viwanda vya mbolea hapa nchini zinaendelea. Tayari tunacho Kiwanda cha Minjingu kinachozalisha mbolea ya *phosphate* na sasa kimeanza kutengeneza mbolea ya Minjingu Mazao, yenye virutubishi vya naitrojeni, *zinc*, shaba na *sulfur* ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao. Aidha, tunaendelea kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea hapa nchini.

Katika kuimarisha shughuli za uzalishaji wa mbegu, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seed Agency),* imeendelea kushirikiana na JKT na Magereza kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora nchini. Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa utaratibu wa kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(Quality Declared Seed),* kwa kutumia wakulima wadogo vijijini kupitia Halmashauri za Wilaya.

**MHE. KHERI KHATIB KHERI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati huu ambao tuna dhana ya Kilimo Kwanza, tunaona kwamba kuna viwanda, tunaagiza matrekta na *power tillers* na vitu vingine, lakini, tuna tatizo la *spare*. Hii moja ni kutokana na kwamba, kwanza, uagizaji wenyewe unatoka kwenye nchi mbalimbali; na pili tulikuwa tuna viwanda vya kutengeneza *spare* za matrekta hapa, mfano; ZZK – Mbeya, UFI – Dar es salaam …

**SPIKA:** Ninaomba maswali yawe mafupi, maana mnatumia muda mwingi mno!

**MHE. KHERI KHATIB KHERI:** Sawa! UFI – Dar es salaam, lakini viwanda hivyo vimekufa. Matrekta haya yatakwendaje wakati ambapo tutaendelea kuagiza *spare* kutoka nje na tutafikia vipi Kilimo Kwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, biashara ya matrekta ni biashara huria, wafanyabiashara wanaruhusiwa kuingiza matrekta, japokuwa hata sisi Serikali tunapopata nafasi kama tulivyofanya kupitia JKT, tumeingiza matrekta mengi nchini. Biashara hii bado inabaki kuwa ya wafanyabiashara. Sasa, kuhusu namna gani tunafanya kwa uagizaji wa *spare*; nimesema tumetoa miongozo kuhusu ubora; tunacho chombo chetu cha *CARMATEC*, ambacho kinasaidia kudhibiti ubora wa matrekta. Kazi kubwa inayotakiwa kufanywa hapa ni kuhakikisha kwamba, wale waagizaji tunawapa miongozo, wanapoagiza matrekta, wanakwenda sambamba na kujenga uwezo wa kuyahudumia *(after sale services)*. Hiyo ndiyo kazi tunayoifanya hivi sasa.

Kusema kwamba sisi tujenge viwanda vya kutengeneza *spares*, hata kama tungefanya hivyo, hatuwezi kuvijenga sasa hivi vikakamilika. Tunajenga uwezo wa waagizaji kutuingizia *spares* ambazo zinakidhi viwango.

Na. 39

**Mavazi ya Kike Kuvaliwa na Wanaume**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kusimamia Utamaduni na Maadili ya Kitanzania kwa kuwadhibiti wanaume wanaovaa mavazi ya kike kinyume na utamaduni wetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na baadhi ya vitendo vinavyofanywa na wanaume au wanawake kinyume na maadili ya Taifa letu. Kwa kutambua kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili miongoni mwa jamii yetu, Serikali kupitia Wizara yangu yenye dhamana ya masuala ya utamaduni, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, Mila na Maadili ya Taifa letu yanafuatwa. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na magazeti kuhusu mila na desturi zetu. Vilevile kumekuwepo na mikutano, semina na warsha mbalimbali kuzungumzia suala la mmomonyoko wa maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna kipindi kiitwacho *"Maadili ya Mtanzania"* ambacho hurushwa hewani kila Siku ya Alhamisi kuanzia saa 12.45 jioni kupitia Redio ya Taifa. Pamoja na mambo mengine, kipindi hicho huikumbusha jamii na umma kwa ujumla, kuheshimu na kuthamini Mila na Desturi za Kitanzania ikiwa ni pamoja na uvaaji wa mavazi ya heshima.

Mheshimiwa Spika, kwa vile suala la uvaaji wa mavazi linakuwa ni maamuzi ya mtu binafsi, ninapenda kutoa wito kwa Watanzania kuvaa mavazi ya heshima yanayozingatia Maadili ya Kitanzania. Aidha, ni wajibu wa kila mtu ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kuhakikisha kuwa, vijana wetu wanazingatia na kufuata Misingi ya Mila na Desturi za Kitanzania.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa wasanii ni kioo cha jamii, wamekuwa wakiielimisha jamii na kuikosoa; haoni sasa kuvaa mavazi ya kike ni kunawadhalilisha wanaume?

(ii) Kwa kuwa kuna utandawazi wa vyombo vya habari vinavyofuatilia habari za ndani na nje ya nchi; huoni sasa wasanii hawa kupaka *makeup*, rangi za midomo, wanja, kuvaa mawigi na mavazi ya kike ndiyo inapelekea sasa kuambiwa tuingie mikataba ya ndoa za jinsia moja? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Ulipenda kuchomekea tu, msingecheka bila hivyo! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Msabaha kwa swali lake la nyongeza, ambalo limetoa kidogo mtazamo na mwelekeo ambao umeniwezesha kupata swali lake la msingi hasa lilikuwa linalenga wapi. Labda nianze kwa kusema kwamba, ametuonesha kwamba, swali lake linalenga hasa wale wasanii ambao huwa wanatuburudisha.

Wanapotuburudisha, *whether,* mitaani au katika Tv zetu, wale wasanii wanaume mara nyingi huvaa nguo za kike. Kwa hiyo, anataka kutuonesha kwamba, kuna athari za wale wasanii wa kiume kujibadilisha na kuweza kuvaa nguo za kike na kudhani kwamba wanatufurahisha.

Ninataka niseme kwamba, kimsingi, Kiserikali hatuna sheria ambayo inazuia kijana wa kiume kuvaa nguo za kike au kijana wa kike kuvaa nguo za kiume. Mila zetu pamoja na desturi, ndizo zinazotupelekea kwamba ni makosa kwa kijana wetu wa kiume kuanza kuvaa nguo za kike.

Anaowazungumzia ni wasanii ambao wakati wao wa kazi huvaa nguo za kike wanapotaka kutoa ujumbe fulani au wanataka ku-*pose* kama wanawake. Sasa labda nitoe ombi tu kwa wale wasanii, kupitia Shirikisho linaloshughulikia wasanii mbalimbali hapa nchini na pia kupitia BASATA kwamba, waweze kuwaita wale wasanii na kuweza kuelimishana na kuhakikisha kwamba angalau wale wasanii wawe na wanawake katika vile vikundi vyao. Kama wanataka kutia vipodozi, wajipodoe vizuri, kama wanataka kuvaa kama wanawake, wawe ni wanawake wenye kuvaa zile nguo kusudi tusitoe picha ambayo siyo nzuri kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, suala kwamba wasanii ni kioo cha jamii; ni kweli kabisa ni kioo cha jamii. Labda tujitahidi tu kuwahimiza na sisi kama jamii pia tukatae kuwa tunafurahishwa kuona wanatokea pale vijana wa kiume wamefanya *exaggerations* makalio, wamefanya *exaggerations* nyonyo, lakini pia wamefanya *exaggerations* kwenye *lipstics* na wanja kupita kiasi, nguo zimewabana wakati tukitambua kabisa kwamba wale siyo wasichana ni wanaume.

Labda tujitahidi tu hilo kwamba, sisi kama jamii, kwanza, tukatae kwa sababu kwa kiasi kikubwa kwa mtazamo ambao ninadhani pia ni mtazamo wa Kiserikali, kwa kiasi kikubwa kwa kupitia Shirikisho, itatubidi tuwakanye na kuweza kuwapa mwelekeo mzuri. Kwa kiasi kikubwa wanadhalilisha wanawake.

**SPIKA:** Mheshimiwa inatosha.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO:**Lakini pia siyo kwamba tu inawafanya wale wanaume wanaofanya vile wanatengeneza hela lakini kwa niaba ya kudhalilisha wanawake kwa kiasi kikubwa. Na wanawake tunaweza tukakuza kizazi cha vijana ambao wakiangalia akina mama wamevaa vizuri labda wamepaka *lipstick* anaanza kukumbuka yule msanii aliyefanya *exaggerations* wakati mambo ya kujipamba ni mambo ya kawaida kabisa ya mwanamke ambayo anatakiwa kuwa nayo.

**SPIKA:** Nashukuru kwa majibu hayo. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir.

Na. 40

**Zanzibar Kujiunga na FIFA**

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR** aliuliza:-

Kwa sasa Zanzibar ni mwanachama wa *CECAFA* na *CAF*. Je, kuna uwezekano wa Zanzibar kujiunga na *FIFA*.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mbunge wa Dimani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Zanzibar kujiunga na *FIFA* limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu. Vyama vyetu vya mpira vya *ZFA* na *TFF* vimekuwa vikifanya jitihada za pamoja kuhakikisha Zanzibar inapata uanachama wa *FIFA* bila mafanikio.

Kwa kutambua umuhimu wa Zanzibar kupata uanachama wa *FIFA*, mwaka 2010 ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikiongozwa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, walikwenda Zurich-Swizerland ambako walikutana na Rais wa *FIFA*. Aidha, katika msafara huo, walikuwepo Rais wa *TFF* na viongozi wa *ZFA*. Katika mazungumzo yao, Rais wa *FIFA* aliahidi kuliwasilisha suala hili kwenye vikao husika ili kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2011 *FIFA* waliandika rasmi *ZFA* ikiwajulisha kuwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo sasa haitawezekana Zanzibar kupata uanachama kwa kuwa wanachama wa *FIFA* ni nchi zinazotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa kama inavyoelewa katika Katiba yao. Hata hivyo, *FIFA* iliahidi kuendelea kuisaidia *ZFA* kupitia *TFF* kama walivyofanya kwa kuweka nyasi bandia katika uwanja wa Gombani na mafunzo yanayosimamiwa na *FIFA*.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imekuwa ikiunga mkono jitihada za *ZFA* kupata uanachama wa *FIFA*. Ninaahidi kuwa tutaendelea kushirikiana na vyama vyetu vya *ZFA* na *TFF* kadri itakavyowezekana kufanikisha jitihada zozote zitakazosaidia kuwezesha *ZFA* kuwa mwanachama wa *FIFA*.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza;

Katika jibu lake Naibu Waziri amejibu kwamba barua ya *FIFA* ya mwezi Juni imeelezea kwamba Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa *FIFA*

**SPIKA:** Sasa uliza swali tu.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika swali, nchi ya China ni nchi kubwa kama Tanzania inahusiana na Hongkong, lakini Hongkong ni wanachama wa *FIFA* na China ni wanachama wa *FIFA*;

(a) Je Waziri ameiona hiyo barua ya *FIFA* iliyoelezea hivyo?

(b) Tanzania ina kocha wa timu ya Taifa ya Tanzania, lakini kocha huyu huyu anakuwa ni kocha wa timu ya Tanzania Bara. Je ni utaratibu au siyo utaratibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba majibu kwa kifupi sana, sina uhakika kama umeiona barua ya China hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la China na Hongkong lakini wote wakawa ni wanachama wa *FIFA* mimi nadhani hilo sisi kama Tanzania na kama Wizara hatuwezi kulisemea.

Kama nilivyosema *ZFA* kutokupewa uanachama wa *FIFA* ni uamuzi wa *FIFA* na unatokana na Katiba yao ilivyosimama na kama nilivyojibu katika swali langu la msingi ni kwamba wanatambua nchi ambayo chini ya UN ni nchi ambayo inatambulika, sasa Zanzibar inatambulika pia ndani ya Taifa letu la Tanzania, na Tanzania tayari imeshawakilishwa na TFF.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusema hayo ni lazima niseme tu kwamba kumekuwa na jitihada za dhati na jitihada za maksudi kabisa za *TFF* pamoja na Serikali yetu kuhakikisha kwamba tunajitahidi *FIFA* kwa namna yeyote ile, kama ikiwezekana hata wakati wakibadilisha Katiba yao waweze kutuingiza na sisi. Suala la Hongkong na China ni la kwao, siyo Hongkong tu na China tu yapo pia masuala ya namna hii kwa nchi za Uingereza nasikia Ireland na yenyewe pia iko namna hiyo. Lakini ninachotaka kusema hapa kwamba wale labda wakati *FIFA* inaanza kufanya shughuli hizo hizi nchi tayari zilikuwa humo kama wanachama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mimi kuwa na hiyo barua

**SPIKA:** Mheshimiwa naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Barua hiyo ipo,

**SPIKA:** Barua ya China haipo

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Ningekuwa na uwezo wa kuionesha hapa ningafanya hivyo ninayo pale kwenye kiti changu, siyo kwamba haya maneno ni

nimefanya kutunga tu ni maneno ambayo yanaeleweka na ni barua ambayo imekuja mwezi wa sita huu na sisi tumeizungumzia. Asante.

**SPIKA:** Naomba ujibu kwa kifupi sehemu ya pili hukujibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kocha kufundisha na timu ya Bara peke yake, mimi nadhani wakati anapokuwa anafundisha wapo wachezaji wanaotoka Zanzibar, ile Timu ya Taifa haiunganishi tu wachezaji wanaotoka Bara ambayo wanapata mafunzo kutoka kwa kocha huyu.

Kwa hiyo mimi nadhani kwa msingi wa mshikamano na msingi wa kushirikiana ni lazima tuungane na huyu kocha kuhakikisha kwamba tuna *train* watu wetu vizuri na hawa makocha ndiyo mafanikio mojawapo ambayo tunasema *FIFA* ikitoa msaada *TFF* hata Wazanzibar nao pia huwa wanafaidika au *ZFA* wanafaidika, Ahsante.

**SPIKA:**Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumechukua muda mwingi sana, sababu zake kubwa maswali ya kuandikwa Mawaziri wanafanya vizuri sana, maswali ya nyongeza yanachukua muda mwingi sana. Bahati nzuri mimi nimeorodhesha kila swali limechukua dakika ngapi. Wastani wa kujibu maswali ni dakika tano. Sasa unakuta inakwenda dakika kumi mpaka kumi na tano. Hivyo hivyo maswali ya nyongeza kwa Waheshimiwa Wabunge ni hotuba hili ndiyo tatizo ambalo tunalo. Kwa hiyo, maswali ya nyongeza ni marefu mno na majibu ya nyongeza ni marefu mno.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliopo mbele yetu hapa, tunao wanafunzi hamsini na walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Nzuguni. Naomba walimu na wanafunzi wasimame mahali walipo. Ahsante sana karibuni. Nzuguni nadhani ni Dodoma. Tunao wageni thelathini (30) wa Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale ambao wapo kwenye mafunzo ya kulea watoto yatima, Walimu wetu hawa wasimame mahali walipo, aah! ahsante sana, sijui mafunzo haya yanafanyika wapi lakini tunawapongeza sana na mtusaidie kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine kumi (10) wa Mheshimiwa Rose Kamil ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Arusha Education (*BED*) hawa na wenyewe wako wapi kutoka Arusha, asante sana karibuni na msome vizuri.

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo Tarehe 10 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ambacho kitafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa B; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo baada ya kipindi cha Maswali kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi Na. 231 tukimaliza kipindi cha maswali waende kwa sababu ya shughuli ile.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati hiyo kwamba leo baada ya kipindi cha maswali wakutane kwenye ukumbi wa *basement.* Agenda ni kujadili Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Biashara. Ninawaruhusu muende wakati huu. Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati tendaji ya Chama cha *APNAC* (Chama cha Wabunge wanaopambana na Rushwa Barani Afrika) kuwa leo tarehe kumi watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Msekwa C saa Saba mchana wajumbe wote wahudhurie.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo kutoka Idara ya Habari, Elimu kwa Umma na Uhusiano wa Kimataifa, Idara yetu hapa, tangazo la Mfuko wa Pension wa *LAPF.* Mfuko wa Pensheni wa *LAPF* umeweka Dawati la maelezo katika viwanja vya Bunge hadi tarehe 18 Novemba, 2011 kwa hiyo mnaombwa kufika kwenye Dawati hilo kupata maelezo kuhusu mafao yanayowafaa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, mnakaribishwa mpate maelezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu, tuendelee na *Order Paper*.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011
### *(The Public Procurement Bill, 2011)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011 *(The Public Procurement Act 2011)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wake. Vile vile nawashukuru wadau na washauri mbalimbali ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri na mapendekezo yao kwa lengo la kuuboresha Muswada huu.

Aidha, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watalaam wake kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wa maandalizi ya Muswada huu, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na mapendekezo na ushauri wa wadau wengine wote.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kufuta sheria ya Ununuzi wa Umma sura ya 410 ya mwaka 2004 na kutunga sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 ili kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria ya mwaka 2004 kwa lengo la kuuboresha usimamizi wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Bunge wa Mwezi Februari 2011. kwa mujibu wa taratibu Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeandaa na imewasilisha jedwali la Marekebisho yaani *Schedule of Amendments* kuhuisha maoni yaliyotolewa na Kamati pamoja na wadau mbalimbali kama sehemu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i)Kuainisha masuala ya kisera ya Ununuzi wa Umma katika sheria hii ambayo yatasimamiwa na Idara ya Sera ya Ununuzi wa umma kama ilivyo kwa vyombo vingine vinavyosimamia masuala ya ununuzi wa umma. Mapendekzo haya yatawezesha kueleweka kwa majukumu ya kila chombo na mipaka yake.

(ii)Kuipa uwezo PPRA kutekeleza majukumu yake ya udhibiti kwa uhuru na ufanisi.

(iii)Kuimarisha usimamizi wa masuala ya ununuzi katika Halmashauri ili kudhibiti wizi na matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Halmashauri hizo.

(iv)Kuboresha majukumu ya mamlaka ya rufani ya zabuni PPAA na kukifanya kuwa chombo huru kinachoweza kutekeleza majukumu yake ya kushughulikia malalamiko na Rufani za Zabuni kwa ufanisi pamoja na kupunguza muda katika kushughulikia malalamiko hayo.

(v) Kuongeza ufanisi katika Ununuzi wa Umma kwa kuweka utaratibu wa ununuzi wa bidhaa na huduma mtambuka ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika katika manunuzi.

(vi)Kurekebisha mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria Ununuzi wa Umma sura ya 410.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu katika Muswada huu. Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama haya yafuatayo:-

(a)Kubainisha majukumu ya kisera ambayo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atayatekeleza kupitia Idara ya usimamizi wa sera ya ununuzi wa umma.

(b)Kuipa uwezo Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma PPRA kusimamia na kutekeleza majukumu yake ya udhibiti wa uhuru na ufanisi.

(c) Kuiwezesha mamlaka ya rufani za zabuni PPAA kuwa chombo huru ambacho kitatekeleza majukumu yake ya kushughulikia migogoro inayohusu zabuni kwa ufanisi.

(d)Kuweka utaratibu wa ununuzi wa bidhaa ambazo bei zake hubadilika kutokana na msimu kama vile vyakula, mbolea na kadhalika.

(e)Kuweka utaratibu wa ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka kupitia *framework agreements*.

(f)Kubainisha mazingira na vigezo vitakavyotumika kufanya ununuzi wa dharura, mazingira hayo ni pamoja na yale yasiyoweza kuzuilika au yasipofanyika yatahatarisha amani na ustawi wa nchi au yataisababishia Serikali hasara.

(g)Kuruhusu Serikali kufanya manunuzi ya vifaa maalumu ambavyo ni Ndege, meli, mabehewa na vichwa vya treni vilivyotumika ambavyo gharama yake ni kubwa, pia ni vigumu kupatikana kwa urahisi vikiwa vipya na upatikanaji wake vikiwa vipya huchukua muda mrefu. Aidha utaratibu wa kudhibiti matumizi mabaya ya kifungu hiki utaainishwa kwenye kanuni.

(h) Kuweka utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kina *due delegence* kwa wazabuni wa ndani na nje ya nchi wanaposhiriki katika zabuni za kimataifa.

(i) Kuipa *PPRA* uwezo wa kusitisha mchakato wa zabuni yeyote kabla ya kutiwa saini endapo itathibitika kuwepo kwa ukiukwaji wa sheria na kanuni zinazosimamia Ununuzi wa Umma.

(j) Kuiwezesha *PPRA* kupata maelezo kutoka kwa mamlaka zinazohusika na ununuzi kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa wanaokiuka sheria ya Ununuzi wa Umma.

(k) Kuiwezesha *PPRA* kuzielekeza mamlaka zenye dhamana ya ununuzi zitakazopokea hoja za ukiukwaji wa sheria ya ununuzi wa umma kutoka PPRA kutoa taarifa kuhusu hoja hizo katika kipindi maalum.

(l) Kuweka sharti la kuomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au mamlaka ya kuidhinisha bajeti kabla ya kutoa zabuni ambayo imezidi Bajeti iliyoidhinishwa kwa taasisi husika.

(m) Kumuongezea uwezo Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya wazabuni kwa kuunda jopo (*Review Panel*) la kupitia malalamiko na kumshauri kuhusu hatua za kuchukua kwa mujibu wa sheria. Aidha, Afisa Masuuli kuwa na fursa ya kupata ya kupata ushauri wa kitalaam katika masuala ya ununuzi iwapo utalaam huo utakosekana ndani ya taasisi yake.

(n) Kumpa uwezo Afisa Masuuli kusimamia mchakato wa zabuni mara malalamiko kutoka kwa Mzabuni yanapowasilishwa kwake. Endapo zabuni hiyo ni ya dharura au ni muhimu kwa maslahi ya Taifa, Afisa Masuuli atalazimika kuomba kibali PPRA ili kuendelea na mchakato.

(o) Kuainisha ukomo wa viwango vya zabuni ambavyo mikataba yake itapaswa kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(p) Kuweka mfumo katika kanuni za sheria ya ununuzi wa umma wa Serikali za Mitaa utakaowezesha Madiwani kusimamia masuala ya ununuzi katika Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango ili kudhibiti wizi wa fedha za Umma katika Halmashauri.

(q) Kuainisha masuala yanayohusu mashirikiano ya Ununuzi kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Mpangilio wa Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu 10 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, yenye vifungu vya 1 hadi 4 inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada, tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika katika Muswada, pamoja na kuitambua Mikataba ya Kimataifa inayohusu masuala ya ununuzi.

Sehemu ya pili, yenye vifungu vya 5 na 6 inahusu kwanza kuitambua Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma. Pili, kuainisha majukumu ya Idara kama ilivyo kwa vyombo vingine vinavyosimamia masuala ya Ununuzi wa Umma ili kuwezesha kueleweka kwa majukumu ya kila chombo na mipaka yake.

Sehemu ya tatu ya Muswada, yenye vifungu vya 7 hadi 30 inahusu kwanza kuitambua Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma yaani PPRA itakayoweza kutekeleza majukumu yake ya udhibiti kwa uhuru. Pili, majukumu ya PPRA pamoja na Mamlaka ya PPRA ya kufanya uchunguzi wa zabuni zinazopitishwa na taasisi za ununuzi na hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa Umma watakaobainika kuhusika na ukiukwaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa Umma. Tatu, mamlaka ya PPRA kusitisha mchakato wa zabuni kabla ya kutiwa saini kutokana na ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu ya Ununuzi wa Umma na kutoa adhabu kali kwa watakaobainika kujihusisha na ukiukwaji huo. Nne, inahusu uteuzi wa wajumbe wa bodi ya Wakurugenzi wa PPRA, uteuzi wa Afisa Mtendaji Mkuu, Ajira za Watumizi, vyanzo vya mapato ya PPRA na taarifa za matumizi na ukaguzi wa hesabu za PPRA.

Sehemu ya nne, inajumuisha kifungu cha 31 hadi 46 vinavyobainisha kwanza Bodi za Zabuni na Mamlaka za kuidhinisha bajeti na kazi zake, majukumu ya Afisa Masuuli, Vitengo vya Ununuzi na kazi zake pamoja na Kamati za kutathimini zabuni. Pili, wajibu wa taasisi za ununuzi, kutoa taarifa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu ununuzi wowote utakaovuka kiwango kilichotengwa katika Bajeti. Tatu, uwezo wa Maafisa Masuuli kupata ushauri wa kitalaam katika masuala ya ununuzi iwapo utalaam huo utakosekana ndani ya taasisi zao. Nne, utaratibu wa kufanya ununuzi kwa *PPRA* na *PPAA*, tano utunzaji wa taarifa za siri za zabuni, sita jukumu la Afisa Masuuli kuidhinisha ununuzi, saba kubainisha kwamba Kamati za kutathimini zabuni si za kudumu na zitateuliwa kutegemeana na aina ya ununuzi. Nane, kuruhusu Madiwani kusimamia masuala ya ununuzi katika Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango.

Sehemu ya tano, inajumuisha vifungu vya 47 hadi 62 ambapo vifungu vya 47 hadi 48 vinahusu jukumu la mamlaka yenye dhamana ya ununuzi na Bodi za Zabuni kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Aidha, sehemu hii inabainisha jukumu la mkaguzi wa ndani kujumuisha katika taarifa yake ya robo mwaka maoni yake endapo sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake imezingatiwa na kuwasilishwa taarifa hiyo PPRA. Vifungu 49 hadi 62 pamoja na mambo mengine vimebainisha masuala yafuatayo:- Kwanza jukumu la menejimenti ya mamlaka yenye dhamana ya ununuzi, kupitisha mpango wa ununuzi wa mwaka. Pili sharti kwa Afisa Masuuli kufanya uchunguzi wa kina yaani *due diligence* kwa wazabuni wa nje na ndani wanaoshiriki katika zabuni, tatu. Ukomo wa viwango vya zabuni ambavyo mikataba yake itapaswa kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Nne, mazingira yanayoweza kusababisha kampuni au mtu kufungiwa kushiriki zabuni za Serikali. Tano, jukumu la PPRA kutunza kumbukumbu za makampuni au watu waliofungiwa. Sita, kuweka muda wa siku 30 kwa taasisi za ununuzi kuwasilisha PPRA taarifa kuhusu Mikataba iliyotolewa kwa wazabuni na viwango vya fedha vya mikataba hiyo, saba, kuweka utaratibu wa kutumia wakala wa huduma ya ununuzi Serikalini yaani GPSA katika ununuzi wa bidhaa ambazo ni mtambuka. Sehemu ya sita yenye vifungu vya 63 hadi 78 inabainisha kwanza aina mbalimbali za ununuzi na vigezo vya kuzingatiwa, pili, masharti na vigezo vya kufanya ununuzi katika mazingira ya dharura, kuandaa nyaraka za zabuni, utaratibu wa kutangaza zabuni na tathimini ya zabuni. Tatu, kuweka muda maalum wa siku 14 ambao Afisa Masuuli, atapaswa kuwasilisha maombi ya uhalalisho wa ununuzi wa dharura. Nne kuweka utaratibu wa ununuzi wa bidhaa ambazo bei zake hubadilika kutokana na msimu kama vile vyakula, mbolea na kadhalika. Tano, kuruhusu Serikali kufanya ununuzi wa vifaa maalum vilivyotumika ambavyo gharama yake ni

kubwa pia ni vigumu kupatikana kwa urahisi vikiwa vipya huchukua muda mrefu. Ununuzi wa vifaa maalum vilivyotumika utahusu tu:-

(a) Ununuzi wa ndege.

(b) Ununuzi wa meli.

(c) Ununuzi wa mabehewa na injini za treni.

Sehemu ya 7 yenye vifungu vya 79 hadi 82 inahusu mashirikiano ya kufanya ununuzi kati ya Serikali na sekta binafsi.

Sehemu ya 8 yenye vifungu vya 83 hadi 87 inaweka masharti kwa watumishi wa umma na wazabuni kutojihusisha na vitendo vya rushwa na udanganyifu. Aidha, sehemu hii inaweka adhabu kwa wale watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo. Sehemu hii pia inaweka sharti kwa wazabuni kutoa taarifa kwenye taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) endapo amepata zabuni yoyote baada ya kuahidiwa kutoa rushwa.

Sehemu ya 9 inahusu usuluhisho wa migogoro ya zabuni na inajumuisha vifungu vya 88 hadi 101. Vifungu vya 88 hadi 94 vinahusu majukumu ya PPAA ya kushughulikia malalamikia na rufaa za zabuni kwa uhuru. Vifungu vya 95 hadi 101 vinabainisha haki ya mzabuni kuwasilisha malalamiko endapo ataona hakutendewa haki na Afisa Masuuli. Aidha, sehemu hii inabainisha uteuzi wa Katibu Mtendaji wa PPAA na masharti ya ajira yake.

Sehemu ya 10 inahusu masuala ya jumla na inajumuisha vifungu 102 hadi 108. Vifungu hivi vinabainisha wajibu wa watumishi wa umma na wataalam wanaotumia sheria ya Ununuzi wa Umma kuzingatia maadili ya kazi zao.

Aidha, vinatoa kinga ya kutoshitakiwa kwa watumishi wa PPRA na PPAA pale wanapotekeleza majukumu yao kwa nia njema yaani *good faith*. Aidha sehemu hii inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutengeneza kanuni kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na hatimaye mkubali kuupitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 ili niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria husika ambao unafuta Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 kwa dhamira ya kuweka utaratibu mzuri zaidi katika kusimamia Ununuzi wa umma. Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wa Wizara yake,Taasisi zinazoratibu Ununuzi wa Umma, Wanasheria toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Wadau wa Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuwa na historia kidogo, itakumbukwa mnamo tarehe 13 Aprili, 2011 Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ilikutana mjini Dodoma kujadili Jedwali la Marekebisho la Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 pamoja na majibu ya

Serikali kuhusu ushauri uliotolewa na Kamati katika vifungu mbalimbali hasa kufuta kifungu namba 63 (3) na (4) cha Muswada kuhusu ununuzi wa mitambo na mashine zilizotumika. Wakati Kamati ikiendelea kuujadili Muswada huu, tarehe 14 Aprili, 2011, Serikali iliamua kuuondoa Muswada huu katika ratiba ya kujadiliwa katika Mkutano wa tatu wa Bunge uliokuwa ukiendelea kwa wakati huo, kwa kuwa bado kulikuwa na umuhimu wa kuendelea na mashauriano ndani ya Serikali na pia marekebisho yake yalikuwa makubwa yenye kuhitaji umakini mkubwa katika uandishi wake.

Leo hii, Serikali imeuwasilisha Muswada huu ukiwa na marekebisho yote ya msingi kwa mujibu wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati pamoja na wadau, Kamati inaipongeza Serikali kwa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kukiri kuwa Kamati imechambua kwa makini Muswada huu, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza maoni ya Wadau zaidi ya 50, pamoja na kupata maoni yao kwa maandishi. Ushauri na maoni yao yote tumeyazingatia katika kuujadili na kuuchambua Muswada husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati haina haja ya kutoa msisitizo juu ya umuhimu wa Muswada huu. Ununuzi wa Umma unagusa maeneo ya Uchumi, Siasa na uwazi katika kuendesha na kusimamia rasilimali za Umma. Inakadiriwa kuwa Ununuzi unatumia karibu asilimia 10 ya Pato la Taifa la Tanzania.

Aidha, kwa fedha zote zinazotumika asilimia 70 ya matumizi ya kawaida ni kwa ajili ya manunuzi na asilimia 100 ni kwa ajili ya manunuzi katika matumizi ya maendeleo. Kwa msingi huu Sheria ya Ununuzi haina budi kuzingatia kukuza uchumi na tija, uwazi, usawa na uwajibikaji. Kamati inafuraha kueleza kuwa sasa marekebisho mengi na ya msingi yamefanywa na Serikali katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chimbuko la kuleta Muswada huu kama nilivyosema awali ni kurekebisha mapungufu ya Sheria ya sasa ya Mwaka 2004 kama yalivyoonyeshwa na kubainishwa na Wadau, umuhimu wa kuiongezea madaraka Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA) na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni (PPAA) na hatimaye kuboresha taratibu za Ununuzi wa Umma ili kuongeza ufanisi, nidhamu na uwajibikaji katika Sekta ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo Kamati ina maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Mitambo na Mashine kubwa zilizotumika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na maoni yake ya kuondoa kwenye Muswada vipengele vya kuruhusu ununuzi wa mitambo iliyotumika badala yake kuweka vipengele ambavyo vinaruhusu ununuzi wa vifaa vilivyotumika katika maeneo maalum ambayo yanagusa maslahi ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Maeneo hayo yatahusu vyombo vya usafiri kwa maana ya ndege, meli, treni na mabehewa yake basi. Sheria hii haitoi ruhusa ya kununua mitambo na mashine iliyotumika katika maeneo mengine. Kamati iliona si vizuri kwa Serikali kujiingiza moja kwa moja katika utaratibu wa kununua vifaa vilivyotumika na kuwa liwe ni jambo la kawaida katika nyanja na ngazi zote za Serikali na ngazi zote za Serikali kuanzia Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu. Uzoefu umeonyesha utaratibu huu umekuwa ukiliingiza taifa katika hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati, kama itakavyoonekana ruhusa hii inagusa ngazi ya Taifa tu, tena mpaka kwa kibali kutolewa na Baraza la Mawaziri. Kamati haikukubaliana na mapendekezo ya mwanzo ya ununuzi wa mitambo na mashine zilizotumika kwa sababu zifutazo:-

· Wadau wote wa ununuzi katika kutoa maoni yao hawakukubaliana na utaratibu uliopendekezwa.

· Bado ni changamoto kwa Serikali katika kudhibiti uingizaji wa vifaa vilivyotumika. Hivyo ni dhahiri kuwepo na mashaka makubwa katika ununuzi makini wa mitambo na mashine zilizotumika.

· Uadilifu na uaminifu wa baadhi ya watumishi wa Serikali ni changamoto. Hivyo kuna hatari kubwa ya kununua mitambo na mashine zilizotumika ambazo hazitafaa au zitakazotumika kwa muda mfupi tu na hivyo kutokidhi lengo lililokusudiwa.

· Mitambo na mashine nyingi zinatengenezwa kutokana na teknolojia ya wakati husika, hivyo kununua mitambo au mashine zilizotumika kuna hatari ya kukosa vipuri pindi zinapoharibika.

· Kuna hatari kubwa kwa Serikali kuingia gharama mara mbili ya kununua mitambo au mashine nyingine, kwa kuwa inaweza kutopata thamani inayolingana na ubora hata kama itakuwa imefanya ukaguzi wa mitambo hiyo.

· Ununuzi wa mitambo au mashine zilizotumika unaweza kupelekea nchi yetu kuwa ni dampo (*dumping place*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Madiwani kushiriki katika Mchakato wa Zabuni, katika kujadili Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kamati ilibaini matatizo makubwa yanayojitokeza katika Halmashauri zetu katika eneo hili la Ununuzi wa Umma. Hivyo Kamati ilipendekeza umuhimu wa kuweka kipengele cha kisheria katika Muswada husika, ili kuhakikisha kuwa Madiwani katika Halmashauri nao wanahusishwa kusimamia kikamilifu masuala ya ununuzi kwenye zabuni kwa kupitia Kamati zao za Fedha na Mipango. Hapo awali taratibu zilikuwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri kusaini mikataba ya zabuni baada ya mchakato mzima kumalizwa na watendaji.

Hali hii imefanya Halmashauri nyingi kutosimamia kikamilifu taratibu za manunuzi na hivyo kushindwa kuwajibika ipasavyo katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika maeneo yao. Mapungufu haya yameleta udhaifu katika kudhibiti wizi wa fedha za umma, rushwa na hata kushindwa kupima thamani ya fedha *(value for money)* kwa miradi inayotekelezwa. Kamati inatarajia kuwa Waheshimiwa Madiwani, kupitia utaratibu huu wa kuhusishwa kwenye mchakato wa zabuni, utasaidia katika kuleta maendeleo katika maeneo yao pamoja na kupunguza kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Dharura, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu suala la ununuzi wa dharura kwa upande wa bidhaa, kazi au huduma pindi panapotokea tishio la maisha ya watu, vita, afya, usalama wa nchi, moto au majanga ya asili . Kamati inaishauri Serikali kuweka vigezo vitakavyotumika kufanya ununuzi wa dharura pamoja na kuzingatia maelekezo ya kifungu 65 (5-9) vinavyotoa utaratibu unaopaswa kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, Sera za Ununuzi wa Umma, Kamati imependekeza iongezwe sehemu katika Muswada huu itakayotoa maelekezo ya uundwaji wa Kitengo cha Usimamizi wa Sera za Ununuzi wa Umma pamoja na kazi zake ambacho kimeanzishwa ndani ya muundo wa Wizara ya Fedha. Hapo awali masuala ya usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma yalikuwa yanatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Hali hii imeondoa tatizo la *PPRA* kuwa ndio mtunga sera na hapo hapo ndio msimamizi wa utekelezaji wa sera awe huyo huyo.

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa muda wa kushughulikia Ununuzi *(Standard Procurement Processing Time),* Kamati kwa nguvu zote inaishauri Serikali kupunguza muda mrefu unaotumika katika mchakato wa ununuzi. Wadau wengi wanalalamikia mchakato mrefu wa Ununuzi wa Umma nchini ambao unagubikwa na urasimu, upotevu wa muda na hata hisia za rushwa na hivyo kuongeza gharama katika kufanya shughuli za biashara na uchumi ikilinganishwa na nchi jirani. Hili linakwaza mazingira ya kukuza uwekezaji na Uchumi wa nchi yetu.

Kamati inaunga mkono Serikali kwa kupunguza muda unaotumiwa katika kushughulikia malalamiko ya wazabuni kutoka siku zisizozidi 105 za sasa na kuwa siku zisizozidi 60. Hivyo malalamiko sasa yatawasilishwa kwanza *PPRA* ambayo itatakiwa kutoa maamuzi katika kipindi

kisichozidi siku 14, endapo mlalamikaji hataridhika na uamuzi, atawasilisha malalamiko yake moja kwa moja kwa PPAA.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kujirekebisha na ucheleweshaji unaojitokeza katika uandaaji wa nyaraka za Zabuni (*bid documents)* na uidhinishaji (*approval*); uharaka katika tathmini ya tenda; muda wa kusubiri kusaini Mikataba/Zabuni na mabadiliko yatokanayo na mabadiliko ya viwango vya gharama mara zabuni zinapopitishwa *(limit negotiations of contract variations).* Eneo hili limekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuboresha eneo la ununuzi

Mheshimiwa Spika, Mashirikiano kati ya Sekta Binafsi na Ununuzi wa Umma. Kamati inawapongeza wadau wote pamoja na Mheshimiwa Nimrod E. Nkono, (Mb) waliotoa mchango wao wa kitaalam kuhusu kuongeza masula ya mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)* na utaratibu wa udhibiti wa Ununuzi wa Umma.

Hivyo Serikali imekubali kufanyia marekebisho sehemu ya Saba kifungu cha 79-82 ili kuzingatia masuala yanayohusu *PPP* pamoja na kuahidi kufanyia marekebisho ya kanuni zitakazotungwa za Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao (E-*procurement*) Muswada huu umefanyiwa marekebisho kwa kuongeza vifungu vitakavyoiwezesha *PPRA* kuanzisha,kusimamia na kudhibiti mfumo wa ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao (E-*procurement*) ikiwemo kuruhusu matumizi ya saini za kimtandao na kuwasilisha malalamiko kwa njia ya mtandao. Aidha kanuni zitakazotungwa katika Sheria hii zitabainisha utaratibu wa jinsi ya kutumia mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, Uidhinishaji wa Zabuni (*Approval of Contracts Award*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na mawazo yake kuhusu suala la Afisa Masuuli kutokuwa muidhinishaji wa zabuni *(award contracts*) badala ya Bodi ya Wazabuni (*Tender Board*). Mantiki yake ni kuepuka kuingiliwa maamuzi kwa Afisa Masuuli pamoja na kuondoa ucheleweshaji wowote unaojitokeza. Aidha utaratibu wa kuachia maamuzi kwa Bodi ya Zabuni itaondoa hoja na hisia za rushwa. Hivyo Serikali imekubaliana na maoni ya Kamati pamoja na Wadau kuwa kazi hiyo sasa ibaki kwa Bodi ya Wazabuni kama ilivyo sasa.

Aidha Serikali imefanyia marekebisho kifungu cha 35 (4) ambapo Afisa Masuuli anatakiwa kuomba kibali kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya kufanya ununuzi ambao umezidi Bajeti aliyoidhinishiwa. Kwa upande wa taasisi zenye Bajeti zinazojitegemea, zitaomba kibali kwa vyombo vyao vinavyohusika na maamuzi kama vile Bodi za taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ununuzi kuhusisha na Bajeti. Kamati vile vile iliishauri Serikali kuanzisha Mpango wa Ununuzi kama Chombo cha Bajeti. Maandalizi ya Mipango ya Ununuzi ni lazima yakajumuishwa katika utaratibu wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali. Muswada ulipendekeza mipango ya ununuzi ifanyike miezi miwili baada ya Bajeti kuidhinishwa. Utaratibu huu unachelewesha utekelezaji wa miradi katika maeneo kadhaa nchini, hasa kwenye Halmashauri zetu na Miji yetu. Kamati ilipendekeza Mipango ya Manunuzi yatayarishwe miezi miwili kabla ya Bajeti ili hatimaye mipango hiyo iwe sehemu ya Bajeti ya Nchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na pendekezo hilo.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano ya Kamati vile vile yalitoa angalizo kwa Serikali juu ya uwepo wa majadiliano/mazungumzo na Mzabuni aliyeshinda tenda ya Bidhaa na Ujenzi; baada ya zabuni kutolewa. Utaratibu huu unaleta hisia za rushwa na hivyo basi ni bora majadiliano haya yawekwe wazi hata kabla tenda haijatolewa.

Aidha, Kamati imesisitiza umuhimu wa zabuni kuwa halali( *into force)* baada ya Mzabuni kupewa taarifa ya kushinda badala ya kusubiri mpaka kuweka saini mkataba. Hali hii itapunguza au kuondoa uwajibikaji wa PPAA. Suala la majadiliano lisiwepo baada ya kufunga Mkataba. Serikali imekubaliana na angalizo hili kwa kufuta kipengele cha 60(10) na kuweka badala yake kipengele cha 60 (9).

Mheshimiwa Spika, Wazabuni Wazalendo.Kamati vile vile iliishauri Serikali kuwa Sheria ya Ununuzi katika maeneo mengine lazima itoe upendeleo wa makusudi kwa Wazabuni Wazalendo *(Domestic Preference under National Competitive Tendering).* Hali hii si tu itawawezesha bali itajenga uimara wa Wazabuni husika katika ushindani na hatimaye kujiingiza hata katika zabuni za Kimataifa. Ushauri huu umezingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Utoaji wa uwezo na uhuru kwa PPRA na PPAA.Muswada huu unatoa uwezo na uhuru zaidi kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ununuzi wa Umma badala ya kuwa chombo cha kutoa ushauri kama ilivyokuwa sasa. Aidha, Muswada umeboresha majukumu ya Mamlaka ya Rufani za Zabuni (PPAA) kwa kukifanya chombo huru kinachoweza kutekeleza majukumu yake ya kushughulikia malalamiko kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inashauri Serikali ili PPRA na PPAA kuwa huru zaidi, wakati umefika sasa wa vyombo hivi kujitegemea kibajeti. Hivi sasa Bodi ya PPRA inawajibika kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha nae ni mdau, hapa uhuru na uwajibikaji wa PPRA unatoweka. PPRA na PPAA lazima viwe na fungu (*vote*) lake linalojitegemea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge wengine wa Kamati ni Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Oseler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu.

Waheshimiwa Wabunge wenagine wa Kamati ni Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Mheshimiwa William Augustao Mgimwa.

Waheshimiwa Wabunge wengine wa Kamati ni Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Amour Abdulla, Mheshimiwa Alhaj. Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge, na Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba nimshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Gregory G. Teu na Pereira A. Silima, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wote wa Wizara pamoja na PPRA na PPAA kwa kuandaa na kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, nimshukuru Ndugu Michael Kadebe, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati kuwasilisha maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia sana katika kuandika na kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu.

**SPIKA**: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, leo tunamwona Mheshimiwa Dkt. Magufuli akikaa pale anakaimu nafasi ya Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni akiwa safari. Kwa hiyo, tunakukaribisha katika mchakato huu.( *Makofi*)

**MHE. CHRISTINA L MUGHWAI (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Spika,Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Fedha Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge, napenda kuchukua fursa hii ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu muswada wa sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 53(6) (c).

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa pole za dhati kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Fedha, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto Mbunge ambaye yuko nje ya nchi akiendelea vizuri na matibabu, namwombea kwa Mungu apone haraka ili aweze kurudi nyumbani akiwa na afya njema na kuja kuungana nasi katika ujenzi wa Taifa. Aidha nawaombea afya njema waheshimiwa wabunge wote walioko katika matibabu nje au ndani ya nchi Mwenyezi Mungu awajalie kupona haraka ili waendelee na majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa na Waziri wa Fedha na Uchumi na vilevile Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, muswada huu unapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na kutungwa kwa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011. Sababu ya kwanza ya kutungwa kwa Sheria mpya kama ilivyoelezwa ni kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 tangu kutungwa kwa sheria hiyo. Hata hivyo, Kambi ya upinzani haijapata maelezo yoyote ya kina na ya kuridhisha ambayo yanaonyesha mapungufu ya sheria inayotumika sasa na inayotakiwa kubadilishwa. Kumekuwa na malalamiko ya jumla jumla kuhusu mapungufu ya Sheria ya manunuzi lakini malalamiko mahususi hayaelezwi ni yapi.

Kambi ya Upinzani Bungeni ingependa Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu mapungufu hayo kifungu kwa kifungu na kuonyesha ni namna gani Muswada huu unajibu mapungufu hayo. Aidha Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni hasara kiasi gani ya muda na ya kifedha imeipata kwa kutunga sheria na baada ya miaka sita tu kuifuta.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inafahamu umuhimu wa Sheria ya Manunuzi nchini. Ingawaje tunatambua Sheria inayotumika sasa kwa kiasi kikubwa sana inatokana na mashinikizo ya mikataba ya kimataifa kuhusu Biashara Duniani. Uwazi katika Manunuzi ya Umma (*Transparency in Public Procurement*) ilikuwa ni moja ya sharti katika mazungumzo ya Biashara ya Doha kwenye maeneo yanayoitwa *Singapore Issues.*

Lengo la mataifa makubwa ni kuhakikisha kuwa makampuni yao makubwa yanapata zabuni ambazo nchi zinazoendelea zinatangaza. Ndio maana katika utungaji wa sheria hii ni lazima tuwe makini sana hasa pale ambapo fedha za Umma za ndani (zisizo za wafadhili) zinatumika kununua bidhaa na huduma. Tunasisitiza kuwa manunuzi yoyote ambayo yanatokana na fedha za umma za ndani yaelekezwe kwa kampuni za ndani tu au kampuni ambazo Watanzania wanamiliki hisa nyingi zaidi kwa ubia na kampuni za nje zenye uwezo.

Mheshimiwa Spika,Ununuzi wa bidhaa na Huduma unaofanywa na vyombo vya umma unathamani ya zaidi ya asilimia 15 ya Pato la Taifa *(GDP).* Katika kipindi cha miaka mitatu ya Fedha iliyopita, Taifa letu kupitia manunuzi yaliyofanywa na serikali pekee (bila kujumuisha Mashirika ya Umma) ilitumia takribani shilingi 7.6 trilioni katika kununua bidhaa na huduma. Takwimu hizi zinaonyesha umuhimu wa muswada huu kwa Taifa na hivyo Kambi ya Upinzani Bungeni inashauri waheshimiwa Wabunge waujadili kwa umakini mkubwa sana wakitanguliza mbele maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika,Uchambuzi wetu juu ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka 2009/2010 pekee, umebaini takribani jumla ya Tsh trilioni 2.4 za fedha za umma zilitumika vibaya, ambazo ni sawa na asilimia 21% ya Bajeti yote ya mwaka huo ambayo ilikuwa na jumla ya Sh trilioni 11. Sehemu kubwa ya fedha hizi zimetumika vibaya kutokana na kutozingatiwa kwa sheria ya manunuzi ya umma hivyo muswada huu ni muhimu katika kulinda fedha za umma dhidi ya ufisadi na ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika,Mifano ya fedha zilizopotea au kutumiwa vibaya katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ni pamoja na manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka ya jumla ya

Tsh bilioni 50.6, malipo yenye shaka ya jumla ya Tsh bilioni 15.5. Hali hii inaendelea wakati watanzania wakiwa bado na kumbukumbu chungu za ufisadi uliotokana na ukiukwaji wa sheria ya manunuzi katika mkataba ulioipa zabuni ya kukodisha mitambo ya kufua umeme wa dharura kampuni ya *Richmond Development Company LLC* na hatimaye mkataba huo kurithiwa na *Dowans.*

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya upinzani inatambua pia kwamba pamoja na ufisadi katika manunuzi; kumezuka tatizo lingine kubwa la gharama kubwa za manunuzi ya umma ya bidhaa na huduma ukilinganisha na bei za manunuzi hayo hayo zinazofanywa na wanunuzi wengine katika soko. Hali hii inakwamisha kasi ya maendeleo ya nchi kwa kuwa kiwango cha fedha kinachotumiwa katika manunuzi kingeweza kufanya manunuzi mengi zaidi iwapo mifumo ingewezesha unafuu na ubora katika manunuzi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa kauli kuhusu hali hii na kueleza namna ambavyo muswada huu wa sheria umeandaliwa kukabiliana na tatizo hili ambalo limeota mizizi zaidi katika Serikali za Mitaa. Aidha, kumekuwa na kawaida kwa kandarasi nyingi katika nchi yetu kuongezeka gharama kupindukia katika ya utekelezaji kama tulivyochambua kwa kina katika hotuba za wasemaji wa kambi ya upinzani wa Wizara mbalimbali wakati wa mkutano nne wa bunge uliojadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara Mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni na sababu nyingine ya Muswada huu (tofauti na ile ya kuondoa mapungufu ya sheria iliyopo hivi sasa) ni kuipa Mamlaka ya manunuzi ya Umma (PPRA) na mamlaka ya Rufaa ya Manunuzi ya Umma *(PPAA)* ili kuwa na nguvu zaidi katika utendaji wake wa kazi.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa ujumla mapendekezo hayo hayatakuwa na tija kwa kuwa mapungufu na matatizo yote yanayotokea katika manunuzi ya umma kwa kiasi kikubwa yanatokea kwa kuwa Taasisi zinazonunua *(PEs-Procuring Entities)* ambazo hupindisha sheria ama kwa makusudi kukidhi maslahi yao binafsi au kwa kukosa wataalamu wenye taaluma ya ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2010 kwa upande wa Serikali Kuu inaonyesha kuwa kiwango cha kutofuata sheria (*compliance level*) ni takribani 55%, yaani zaidi ya nusu ya vifungu vya sheria ya manunuzi havifuatwi sawa sawa. Hili ndilo tatizo kubwa ambalo tunapaswa kulishughulikia badala ya kukimbilia tu kutunga sheria mpya ambayo pia taasisi za manunuzi zinaweza kudharau kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Katika muswada huu wa sheria neno *“specification”* halijatafsiriwa na hivyo kutoa mwanya kwa kila mzabuni kutoa “*specifications*” zake yeye na pengine zinakuwa haziendani na zile zilizothibitishwa na *TBS* na viwango vya kimataifa.

Mfano mzuri ni kwa sheria ya wenzetu wa Uganda kwa kuona umuhimu wa neno hilo na hivyo kulitolea tafsiri kama ifuatavyo:-

*“Specification means the description of an object of procurement or disposal in accordance with National and International Standards adopted and approved by the Authority, after consultation with the National Bureau of Standards, or other appropriate trade associations, the use of which shall be mandatory in all bidding documents”*. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba Sheria itamke tafsiri ya neno specification kama hii ya nchi ya Uganda. Aidha tafsiri ya maneno *“successive tender”* maneno katika kifungu kidogo cha (i) katika tafsiri hiyo bado kinasisitiza kuwa ni mzabuni ambaye gharama zake ziko chini na anauwezo wa kutekeleza mkataba, pale mtindo wa ushindani katika kumpata mzabuni utakapokuwa umetumika. Kambi ya Upinzani inaona dhana hii ya kumpatia kazi yule aliyeshindana kwa bei ya chini si sahihi kwani kunakuwepo na uwezekano wa kufanya ujanja ujanja katika kutekeleza mkataba na mwisho kuilazimu Serikali kuitisha zabuni upya. Tukumbuke kuwa siku zote rahisi huwa ni ghali.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona tafsiri hiyo ibadilishwe na kufutwa kwa maneno "*offering the lowest evaluated cost"* ili mzabuni anayeshinda awe ni yule anayekidhi vigezo na ana uwezo wa kutekeleza mkataba hata kama bei yake ni ya juu.

Mheshimiwa Spika,Kifungu cha 15(1) kinaeleza kuwa pale ambapo mamlaka ya ununuzi katika uchunguzi wake itapata uhakika au ushahidi wa matendo ambayo ni kinyume cha taratibu kufanywa na mtumishi wa umma hivyo wanapeleka suala lake kwenye chombo kinachoitwa *"competent authority".*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani hapa inaona huu ni udhaifu mwingine katika sheria hii. Kama ambavyo tumeeleza hapo juu kuwa makosa yanayofanywa na watendaji wa umma ni makosa ya kupata maslahi binafsi na yanashirikisha watendaji wa ngazi za juu katika wizara. Hivyo *PPRA* kupeleka ushahidi wake wa uchunguzi kwa chombo kingine ili kitoe uamuzi ni udhaifu wa muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema kuwa PPRA itoe uamuzi kadri itakavyoona inafaa kulingana na uchunguzi wake na pale mhusika wa uamuzi huo kama hakuridhika ndio apeleke malalamiko yake kwenye mamlaka ya rufaa ya Umma (PPAA).

Sambamba na hilo itakuwa ni bora kwa *PPRA* kutoa adhabu kwa watendaji wa Taasisi za Manunuzi na sio taasisi pekee kwani kutoa adhabu kwa taasisi maana yake ni kuendelea kuitia hasara Serikali wakati watendaji binafsi wanabaki pale pale bila ya kuguswa na maamuzi ya PPRA. Hili litawafanya watendaji kuwa na nidhamu katika utendaji wao na hivyo kupunguza au kumaliza vitendo vya kuangalia maslahi binafsi katika kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19(1) kinachounda bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Manunuzi ya Umma, kwa ujumla wake Kambi ya Upinzani haina pingamizi na kifungu hicho, isipokuwa inatilia mkazo na kukumbusha ushauri na mapendekezo yaliyokwishatolewa na Mkaguzi na Mthibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa, Waziri mwenye dhamana na sheria hii asiteue mjumbe wa bodi ambaye ni mwanasiasa wa kuchaguliwa au kuteuliwa (Mbunge, Kiongozi katika Chama chochote cha Siasa au Diwani).*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23 (1) kinachohusu uteuzi wa mtendaji mkuu wa Mamlaka, kuwa atateuliwa na Rais. Kambi ya Upinzani inaona kuwa mfumo huu wa uteuzi unaifanya bodi kuwa chini ya mtendaji mkuu, hivyo bodi kukosa meno**.**

Kambi ya Upinzani kama ambavyo imekuwa ikishauri kila mara kuwa jukumu la kumpata mtendaji mkuu liwe ni jukumu la bodi husika kwa kutumia taratibu zinazotambulika na kukubalika katika mchakato mzima wa upatikanaji wa ajira ikiwemo kwa kutangaza nafasi watu wenye uwezo wakaomba.

Kwa jinsi hii Bodi itakuwa na mamlaka juu ya namna gani Mtendaji Mkuu anavyotekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 36(1) cha muswada kinaelezea kazi na mamlaka ya *"Accounting officer".* Kambi ya Upinzani inakiona kifungu hiki kumpa *Accounting Officer* mamlaka makubwa mno na kinaweza kuwa chanzo cha rushwa kubwa, kutokana na ukweli kwamba mchakato mzima wa manunuzi unaanzia kwake na kumalizikia kwake, na ukizingatia kuwa watendaji wote wa mchakato wa manunuzi anawateua yeye. Hii ni hatari sana na kama Bunge likikubaliana na kifungu hiki maana yake tuna halalisha uwepo wa rushwa kubwa iwapo madaraka hayo yatatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 51(2) kinahusu sharti kwa Wazabuni wa ndani "*local tenderers"* wanaotaka kushiriki katika mchakato wowote wa manunuzi ni lazima wathibitishe nyaraka muhimu za usajili kwenye bodi muhimu za kitaaluma hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge itakuwaje kwa zabuni zinazotolewa lakini hazihitaji taaluma katika kutekelezeka kwake. Kwani sio kweli kwamba zabuni

zote zitahitaji taaluma. Mfano ni manunuzi ya samani za maofisini, Usafirishaji wa bidhaa za Serikali kutoka mkoa mmoja hadi mwingine, kutoa huduma za vyakula kwenye mashule ya Serikali, huduma za usafi na kadhalika..

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu cha 53 (3) Kambi ya Upinzani inakubaliana kabisa na mapendekezo ya Muswada huu kwamba iwe ni lazima kwa Taasisi yeyote ya Serikali kutafuta uhalali wa kampuni ya nje inayotaka kupewa kazi hapa nchini. Madhara ya kutokuwa na kifungu kama hiki ndiyo yaliyopolekea kupata kashfa kubwa kama ile ya Richmond ambayo iliiangusha Serikali mwezi Februari mwaka 2008. Balozi za Tanzania zilizopo nje zihusike kwa kiasi kikubwa katika kutambua uhalali wa Kampuni zinazoomba kazi hapa nchini. Vile vile Idara ya Usalama wa Taifa kitengo cha ujasusi wa kiuchumi kwa namna moja au nyingine ihusishwe katika kuhakikisha kuwa nchi au Taasisi za nchi haziingii mikataba na makampuni hewa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni wakati mwafaka sasa kuzuia Taasisi za Serikali kufanya biashara na makampuni zilizosajiliwa katika nchi ambazo hazizingatii na kufuata kanuni na sheria za uingizaji na utoaji wa fedha katika nchi zao *(offshore companies).*

Mara nyingi kampuni hizi husajiliwa huko ili kukwepa kodi na hata inakuwa vigumu mikataba inapovunjika kwa Taifa kupata haki yake kwani kampuni hizi huwa hazina mali zisizohamishika. Kadhalika nyingi za kampuni za aina hiyo hutumika kufanya biashara haramu za namna mbalimbali kama tulivyotoa mifano katika Orodha ya Mafisadi *(List of Shame).* Ni vema tukatafakari ili kuwe na kifungu katika sheria kinachokataza Serikali kutoa zabuni kwa kampuni zilizosajiliwa *offshore.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani Bungeni inapendekeza kuwepo kwa kifungu kidogo katika kifungu cha 54 kuhusiana na manunuzi yanayofanywa na Mashirika ya Umma pale ambapo Shirika hilo ni mwanahisa kwa Kampuni ambayo inazalisha Bidhaa zinazutumiwa na Mashirika hayo. Kwa mfano, Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO* linamiliki kwa niaba ya Serikali/Serikali inamiliki kwa niaba ya Watanzania hisa katika Kampuni za *TANELEC* na *EASTAFRICAN CABLES.*

Mheshimiwa Spika, Kampuni hizi zinatengeneza bidhaa ambazo Shirika la *TANESCO* linazitumia katika shughuli zake za kila siku katika kutoa huduma ya umeme, zinaajiri Watanzania, zinalipa kodi nchini na kama zikipata faida zinalipa gawio kwa serikalini. Sheria iweke vipengele ambavyo vitalinda makampuni ya namna hii ili mradi tu bidhaa zinazozalishwa ziwe zina ubora unaotakiwa na bei za kimahusiano ili kuendana na taratibu za kimataifa na bila kuathiri thamani ya fedha. Kambi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa ni vema kuweka mazingira ya kufanya manunuzi kutoka ndani ili kukuza uchumi *(multiplier effect),* kukuza ajira na hata kuongeza mapato ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 54 kinaweka mazingira ya kutoa fursa kwa makampuni ya ndani kufaidika na zabuni ambazo zinatokana na fedha za ndani. Hata hivyo kifungu hiki kitawekewa ukomo na kanuni zitakazotungwa na Waziri. Manunuzi yote yanayofanywa na Serikali na Mashirika ya Umma na ambayo yanatumia fedha za ndani yapewe kwa Kampuni za ndani na zinazomilikiwa na Watanzania.

Iwapo hakuna kampuni ya ndani yenye uwezo wa kufanya kazi zilizoainishwa kwenye zabuni basi, Kampuni ya kigeni itakayopewa kazi lazima iwe na mshirika wa ndani *(local partner)* ambaye atakuwa na hisa nyingi katika kampuni tanzu itakayoundwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani Bungeni inaamini kuwa hii ndio njia bora ya kujenga uwezo wa kampuni za ndani. Bunge na umma ufahamu kwamba kila shilingi inayonunua bidhaa au huduma kutoka nje ya Tanzania ni sawa na kupeleka nje *(export)* ajira kwa nchi za nje. Tutumie fedha zetu kukuza uchumi wetu kwa kutoa fursa kwa Kampuni zinazomilikiwa na Watanzania na sio tu kampuni za Kitanzania. Aidha, kutokana na unyeti na umuhimu wa suala hili la kuwapa kipaumbele watanzania katika zabuni za manunuzi ya umma, ni muhimu kanuni husika zikaandaliwa kwa kushirikisha wadau na mamlaka mbalimbali kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 57(1) kinaweka wazi kuwa nyaraka zote zitakazotumika kwenye mchakato wa zabuni ni sharti ziwe zimeandikwa kwa lugha ya kiingereza, Kambi ya Upinzani inaona sharti kwa njia moja au nyingine linawanyima wajasiriamali ambao wangependa kushiriki katika mchakato wa zabuni lakini haki hiyo ikapotea kutokana na kutokuielewa lugha hiyo vizuri kiasi cha kuweza kushiriki na kushindana. Hili vile vile linakwenda kinyume na kauli mbiu kuwa Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa letu. Hivyo basi, tunashauri mchakato wa zabuni uhusishe lugha ya Kiswahili na Kiingereza na itamkwe hivyo kwenye sheria kusiwepo na matakwa ya mzabuni kuchagua lugha kwa kadri atavyoona yeye inafaa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 65 kinahusu manunuzi ya dharura, Kambi ya Upinzani inakubaliana na umuhimu wa kifungu hiki katika mazingira yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha 2(a), mfano dharura zinazohatarisha uhai,afya, ustawi ama usalama wa jamii katokana na majanga ya asili, milipuko, vurugu (machafuko), vita au moto. Aidha, Kambi ya Upinzani inasisitiza kufutwa kwa kifungu cha 65 kifungu kidogo cha (3) kinachohusu kununua mitambo iliyokwishatumika kwa kisingizio cha dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina taarifa kuwa serikali inakusudia kuwasilisha jedwali la mabadiliko kufuta kifungu kidogo cha 65 (4). Kambi ya Upinzani inaona umuhimu wa kuendelea kuwepo kwa kifungu kidogo cha 65(4) kuwa chombo chenye mamlaka kumsimamia mtendaji mkuu "*accounting officer*" badala ya kumwachia mtendaji huyo mamlaka makubwa ya kuamua nini ni dharura na ni nini maslahi ya Taifa bila ya kuwepo mamlaka nyingine ya kuidhinisha maamuzi yake. Kifungu hicho kinaweza kuboreshwa kwa kuzingatia ngazi za manunuzi mathalani kuweka mfumo wa manunuzi ya dharura kwa upande wa Serikali za Mitaa na taasisi zingine.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 66 kinahusu ununuzi wa vifaa maalum vilivyokwisha tumika, kama vile ndege, mabehewa na injini za treni pamoja na meli. Jambo la kuuliza hapa ni sababu zipi zimepelekea Serikali kuchagua vifaa hivi vitatu tu, wakati dharura huwa haieleweki itatokea katika maeneo yapi. Uchaguzi huu unatia shaka na kupelekea kuamini kuwa kuna jambo tayari limekwishapangwa ili fedha zitumike katika manunuzi ya vifaa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 66(2) kinampa mamlaka Mtendaji Mkuu "*accounting Officer"* kufanya manunuzi ya Meli, Ndege pamoja na Mabehewa ya Treni na Injini zake zilizotumika chini ya mpango wa dharura bila kupata idhini ya mamlaka yeyote.

Kambi ya Upinzani inapingana na kifungu hiki kutokana na mifano iliyo hai na ambayo inawatia uchungu Watanzania kama ifuatavyo:-

1. Kampuni ya Rites katika mkataba wake na TRC walileta mabehewa na injini zilizokwishatumika na matatizo yake kila mmoja ameyaona.

2. *ATCL* ilikodi ndege iliyotumika aina ya AIRBUS lakini toka iikodishwe haijawahi kufanyakazi na badala ilipelekwa nchini MALTA kwa matengenezo na Serikali inalipa dola laki 3.5 kila mwezi kwa ajili ya ndege hiyo.

3. Serikali ilinunua helikopta kwa ajili ya kutumiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania lakini kati ya hizo helikopta 2 zimekwisha dondoka na kusababisha maafa.

4. Watanzania bado hawajasahau machungu ya hivi juzi ya ajali ya meli ya Spice Islander na ile ya Mv Bukoba ambazo maelefu ya watu walipoteza maisha yao.

5. Kivuko cha Kigamboni nacho ni mfano mwingine ambacho ufanisi wake hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, hii ni baadhi tu ya mifano, tujiulize Watanzania wataendelea kupoteza maisha hadi lini kutokana na kununua vifaa vilivyokwishatumika na visivyokidhi viwango? Kambi ya Upinzani inataka marekebisho yafanyike katika kifungu hiki ambacho pia hakielezi kiwango cha ubora kitakachotumika au muda wa matumizi uliobaki kwa kifaa husika ni asilimia ngapi? Kifungu hiki pia kinachanganya manunuzi ya kiraia na ya kijeshi wakati ambapo yana taratibu zinazotofautiana. Aidha, kifungu husika hakijaweka mchakato maalum na wa pekee wa ununuzi

wa vifaa vilivyotumika na hivyo kuweka mfumo ambao manunuzi yatakuwa kama ya kawaida. Kifungu hiki kikipitishwa bila marekebisho ya kina kitatoa mwanya kwa ufisadi na matumizi mabaya ya rasilimali ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada unazungumzia manunuzi kwa njia ya mtandao (e-*Procurement),* katika Dunia ya sasa ununuzi kwa njia ya mtandao ni jambo lisiloepukika.

Hata hivyo, Kambi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa kuna haja ya kufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuanza kwa mfumo huu kwa kutoa mafunzo kwa maafisa masuuli na hata wazabuni wa ndani ili mfumo huu uweze kulisaidia Taifa na pia kutuepusha na uhalifu wa kimtandao *(cyber crime).* Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliweka wazi suala zima la manunuzi kwa njia ya mtandao katika Sheria hii pamoja na kueleza mifumo inayoandaliwa kudhibiti hujuma katika manunuzi kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wetu kuhusu muswada wa ununuzi umebaini kwamba vifungu vingi ya muswada huu vimeacha mwanya kwa taratibu za ziada kuwekwa kwa mujibu wa kanuni *(regulations).* Kambi ya Upinzani inaona kwamba huu ni mwanya unaowekwa kisheria na watawala kwa ajili ya kutunga baadaye masharti na taratibu nyingine ambazo bunge lisingeridhia iwapo zingeingizwa katika sheria.

Ili kuepusha mianya hiyo kutumiwa vibaya, kambi rasmi ya upinzani inatoa mwito kwa bunge kuweka utaratibu wa kanuni husika *(regulations*) kupitiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kabla ya Waziri husika kuzitangaza kwenye gazeti la serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono muswada huu mpaka hapo vipengele muhimu tulivyovianisha hapo juu vitakapozingatiwa ili kudhibiti mianya ya ufisadi na ubadhirifu wakati wa ununuzi wa umma kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, ahsante. Waheshimiwa Wabunge wasemaji Wakuu katika Muswada huu wamemaliza. Kwa hiyo tunaingia kwa Waheshimiwa Wabunge kujadili Muswada huu. Kwa hiyo, atakayekuwa msemaji wa kwanza ni Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangala na Mheshimiwa David Enerst Silinde. Tuanze na hao kwanza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwe mchangiaji wa kwanza kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza nataka kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, wananchi wote wa vyama vyote wa Wilaya ya Chunya na kijiji changu cha Chalangwa kwa kunifariji wakati wa matatizo yangu ya msiba.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea Muswada wa Manunuzi upana wake ni upi. Bajeti ya Serikali mwaka huu ni trilini 13. Katika hizo trilioni 13 trilioni 8.5.6 zinaenda kwenye matumizi ya kawaida. Katika hizo trilioni 8.6 ambazo ni matumizi ya kawaida asilimia 70 inaenda kwenye manunuzi. Iliyobaki trilioni 4.5 trilioni 4.3 inaenda kwenye maendeleo. Katika hiyo asilimia mia kwa mia inaenda kwenye manunuzi. Kwa hiyo, kwenye Bajeti ya Serikali ninaposema Manunuzi ya Umma tuna maana asilimia 80 ya Bajeti nzima ya Serikali kwa Bajeti hii ya trilioni 13 maana yake ya trilioni 10 zinaenda kwenye manunuzi.

Mheshimiwa Spika, ni Muswada mzito sana ambao una maana kubwa kwenye maendeleo ya Watanzania. Pamoja na kumshukuru mtoa hoja kwa kutoa hoja yake vizuri nitaongelea mambo matatu manne kwenye Muswada huu. Kwanza napenda kuipongeza sana Serikali kwamba hatimaye imeanzisha Kitendo cha kusimamia Sera Wizarani kwenye Wizara inayosimamia Manunuzi. Serikali *eventually* imekubali kuanzisha kitengo cha kutunga na kusimamia sera za manunuzi.

Sasa naiomba Serikali kwamba Kitengo hicho baada ya kukianzisha ikiwezesha, ikiwezeshe kwa taaluma, ikiwezeshe kwa rasilimali zote kama ni fedha ili kitengo hiki kifanye kama ilivyofanya Kitengo cha Fedha Wizarani hapo hapo. Kwenye Serikali iliyopita *Accountant General* aliajiri Wahasibu wengi sana akawafundisha, akawafundisha mwaka 2006/2007 akawafundisha akawapeleka kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, naomba na kitengo hiki cha Manunuzi ya Umma ununuzi *is an art* ununuzi kwamba kila mtu anafanya ununuzi, *no, no, no*, ununuzi ni *art* ambao unasomea shuleni. Kwa hiyo, naomba Kitengo hiki kiwezeshwe, kiweze kuajiri wataalam wa ununuzi wengi tuwafundishe waende kwenye Halmashauiri ambako kuna matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa kuanzisha wakala wa manunuzi *GSPA* ambao tunasema huyu Wakala atasaidia kununua vitu ambavyo vinafanana. Naomba kwa ruhusa yako ninukuu kifungu cha 50 cha Muswada kifungu cha 50 kinasema, nanukuu. *"The procurement entity shall* maana yake ni lazima *shall for the purpouse of efficience of procurement process and reduction of procurement transaction costs within and accross public bodies engage frame aggreements".*

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Wizara na Halmashauri wanaotii kifungu hiki ni wachache sana ambao wanamruhusu huyu wakala wa ununuzi kuingia mikataba ya vitu ambavyo vinafanana ili hizi taasisi na Halmashauri ziwe zinaita kila zinapohitajika inaita, anakuwa amenunua kwa bei ndogo vitu vingi kila anapohitajika ni wachache sana wanaotii hii. Naomba Wizara inayosimamia iwakazanie Wizara zote, Taasisi zote kwenye vitu vinavyofanana, anunue huyu wakala wa ununuzi *GPSA* ili hawa wawe wanaita tu kuitwa kutoka kwenye sehemu ambazo hizo vitu vipo.

Mheshimiwa Spika, pia tunaposema ununuzi wa umma, naomba ninukuu kifungu kingine, cha pili, *section two.* Kinasema nanukuu kwa ruhusa yako. *"This Act shall apply*, imesema *shall apply* maana yake ni lazima, *shall apply to (a) to all procurement and disposal by tender undertaken by procain entity eccept where it is provided other wise in this Act shall apply. Ununuzi wa tenda, kununua na ku-dispose by tender".*

Sasa imekuwa ni kawaida taasisi zote za ununuzi Serikalini yaani kutenda ni kununua tu. Hata ku-*dispose* kama umenunua mali ya umma kwa tenda unapoiuza uiuze kwa tenda.

Sasa kumetokea kawaida siku hizi wakubwa wengi hasa hasa wenye mgari unaponunua gari ananunua kwa tenda, lakini wakati wa kuuza gari hiyo, anajiuzia. Kwa sheria inasema uuze kwa tenda, inasema uuze kwa tenda. *(Makofi)*

Utakuta bwana mkubwa sijui Mkuu wa Mkoa yuko pale, gari lake limeisha wamemnunulia lingine, halafu yeye anajiuzia kwa bei anayopanga yeye mwenyewe. Katibu Mkuu, wamemnunulia gari lake, *VX* ile aliyokuwa anatumia anajiuzia! Sheria inasema kununua na ku-*dispose by tender.* Naomba katika hili niipongeze sana Idara ya Usalama wa Taifa, peke yake, ndio yenyewe ina *yard* ambako magari yote yanayotumika yako pale, ukifika muda wa kuuza yanauzwa kwa *tender.* Naomba Wizara nyingine zote na Idara nyingine zote ziige hilo, unanunua na ku-*dispose by tender.*

Mheshimiwa Spika, katika hilo la ununuzi wa magari napenda nimpongeze sana Waziri Mkuu, narudia kumpongeza. Nilimwomba mara mbili tatu kwamba kuwe na Sera ya manunuzi, kuwe na *Car Policy,* yaani kuwe na Sera ya Magari ya Serikali, kuwe na *Car Policy.* Sasa najua ipo, bado hatujaiona kwa maandishi, lakini yeye mwenyewe ameonesha nia, amenunua gari *GX* la kutumia yeye. Ina maana watu wa chini yake watanunua gari lililo chini ya *GX.* Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba Viongozi wengine wote tuige mfano huo, kama Waziri Mkuu anatumia *GX!* pia Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na wewe nakupongeza rafiki yangu. Yeye anatumia *Land Cruiser Standard.* Ni Waziri wa Fedha anatumia *Land Cruiser Standard,* wengine muige hivyo. Kama Waziri Mkuu anatumia *GX,* wengine wote muige mtumie kama analotumia Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti fedha za umma zipo taasisi kama nne. Ipo *PPU* kitengo cha sera, ipo *PPRA,* ipo *PPAA,* upon a Wakala *GSPA.* Hizi zinahitaji *resources* nyingi sana za watu na fedha ili ziweze kudhibiti fedha za Umma hizi. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapotunga Kanuni atunge moja ya Kanuni ambayo inawalazimisha Wazabuni wakatwe asilimia fulani ambazo zitakwenda kuweka uwezo wa hizi taasisi hizi. Atunge Kanuni ambayo wazabunmi wote, hasa wa tenda kubwa, wakatwe asilimia fulani kama 2% au 1% wakatwe ziende kwenye taasisi hizi ili kuzijengea uwezo wa kuweza kudhibiti manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni hii taasisi ya *PPRA* ya Manunuzi ya Umma. Inafanya ukaguzi wa ununuzi, *procurement audits.* Inafanya vilevile *value for money audit* kwenye miradi. Naomba Bunge lako litengeneze Kanuni ambazo zinaruhusu Kamati zetu za Bunge hizi *watch dog commiitees,* zinapokwenda kuzi-*audit* Taasisi na Wizara, kwanza zipate ripoti ya *PPRA.* Zikae na *PPRA* awaambie kwamba bwana, Halmashauri kadhaa tumezikagua, tumekuta kuna ubovu huu na huu kwenye manunuzi ya umma! Basi kama ni Kamati ya Mheshimiwa Augustine Mrema, Kamati ya Mheshimiwa Zitto au Kamati ya Mheshimiwa Cheyo, ikipata ripoti ya *PPRA* ndio ianze kuzitembelea kwenda kuzikagua hizo Taasisi na Idara za Umma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Huyu ndio Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Muswada huu.

Mheshimiwa Alphoxard Kangi Lugola. Atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Hamis Kigwangalla.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya pili kuchangia katika Muswada huu wa Manunuzi ya Umma. Kwanza kabisa naishukuru Serikali yetu kwa kukubali kurekebisha maeneo flani fulani kwenye Muswada huu, hasa kuacha yale manunuzi ya mitambo ambayo imetumika. Lakini pia nishukuru Kamati zote za Upinzani na Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, kwa kuainisha yale maeneo ambayo kama yasingeondolewa yangeleta matatizo makubwa sana katika Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Spika, nianze na eneo hili la Manunuzi ya Umma ya vitu vilivyotumika. Ununuzi wa ndege, ununuzi wa treni, ununuzi wa meli zilizotumika ni kuhatarisha maisha ya Watanzania. Hatuwezi kukubali kufanya manunuzi ya vitu vilivyotumika vyenye uhusiano na maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anapotuandikia hapa katika hoja yake kwamba, hatuwezi kununua ndege mpya, meli mpya, mabehewa mapya kwa sababu gharama yake ni kubwa, pia ni vigumu kupatikana kwa urahisi vikiwa vipya! Mimi sikubaliani na hoja hii.

Huwezi ku-*compromise* maisha ya Watanzania na suala la gharama! Hata hivyo, ile *section 66* ambayo amaesema kwamba, wanaweza waka-*proceed* kufanya *procurement* kwa *normal;* akishasema kwa *normal procedure* maana yake anayakana maneno haya kwamba, ni gharama kubwa na anayakana kwamba haviwezi kupatikana kwa urahisi! Ni maneno yanayowekwa pale kama mtego. Serikali itaendelea kununua kwa *emergence* kwa sababu, tayari tumetumbukiza neno *emergency procurement. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi *whether* ni *emergency, whether* ni njia ya kawaida, sikubaliani kabisa na ununuzi wa vitu ambavyo vimetumika. Mifano imetolewa hapa, ndege zilinunuliwa zimetumika hazikuruka! Na kama ingejaribu kuruka, siku hiyo ingeweza kuleta madhara kwa watanzania. Kuna pantoni za Kigamboni ziliwahi kuharibika, zimenunuliwa ambazo zimetumika na meli nyingine!

Mheshimiwa Spika, katika hili sikubalianinalo. Lakini sababu nyingine ambayo sikubalianinalo, utakaponunua vitu vilivyotumika hununui kwa *manufacture.* Kwa hiyo, huwezi kupata *guarantee* au *warrant.* Kwa hiyo, umenunua tu kwa mashirika ambayo yamechoshwa na

zile ndege, ndege zinawasumbua na mbaya zaidi mnanunua ndege ambayo yeye anauza! Hamuendi kuchagua kwenye *yard* kwamba, tunataka hii; anawauzia ile ambayo yeye anataka kui-*phase out,* iliyomletea shida. Kwa hiyo, hatuwezi kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni *maintainance cost.* Unaweza uka-*avoid* gharama ukaenda gharama ndogo. Lakini kwa sababu vyombo hivi ni vya fedha nyingi, *maintainance cost* yake itakuwa ni kubwa mno, hakuna utakachokuwa ume-*avoid in terms of money.* Mwisho katika hilo, kuna udharura gani kwenye ndege? Kuna udharura gani kununua treni? Kuna udharura gani kununua meli? Kwamba hii ni dharura! Kwamba, leo *ATC* haina ndege kwa hiyo ni dharura, kesho tununue ndege ambayo imetumika! Ni dharura gani hiyo?

Tusikubali kutumia maneno ya dharura vibaya; tukitumia neno dharura vibaya hapa, kwa kweli Serikali yetu itatumbukia katika matatizo makubwa. Na hata walipoainisha mazingira ya dharura, hizi ndege hazihusiki pale! Treni hazihusiki wala meli! Kwa hiyo, mimi ninapinga moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu niende kwenye matumizi mabaya ya fedha, ubadhirifu, wizi, yanayotokana na ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004. Mashirika tumeyaona ambavyo yanakiuka sheria, halmashauri tumeziona zinavyokiuka sheria, pamoja na Idara za Serikali. Sio kwamba sheria hizi hazina meno! Kwamba, leo ndio kuna lugha nzuri tunazitumia kwamba, tunaboresha! Kuna lugha tunatumia, tuipe meno Serikali, tuipe meno *PPRA,* tuipe meno! Sikubaliani kwamba, chini ya Sheria hii ambayo tunaifuta, hawana meno! Meno yamo mle ndani, tatizo ni kwamba meno yao yana kigugumizi katika kung'ata. Meno ya *PPRA,* meno ya watendaji ambao wanatakiwa kuchukua hatua kwa wale ambao wanakiuka sheria za manunuzi, ndio meno ambayo tunatakiwa kuyarekebisha; ambayo tayari yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kule kwetu kule kwa jadi, watu wazee sana hasa wanaume, wanapozeeka wanasema meno yao hayawezi kutafuna nyama. Kwa hiyo, wake zao au watoto wanaanza kuponda ile nyama, halafu ndio inapikwa halafu tunaita nyama iliyopondwa. Kikwetu tunasema: *"Inyama yobhusanjage". K*wa hiyo, ndio anakuwa anakula kwa sababu meno yake yamechoka. Sasa hawa *PPRA* na wale wanaosimamia sheria hizi na wao sasa wanasema meno yao na yenyewe hayawezi kuwang'ata hawa mafisadi katika manunuzi, wezi na wabadhirifu! Wanataka tuwapondeponde ili waweze kuwang'ata.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kukubali visingizio! Hawa ni vijana kabisa meno yao bado ni mazima, hatuwezi kuwapondea nyama. Uzembe na kutowajibika, kutazama watu usoni ambao ni ma-*Chief Executive Officers* wa Mashirika, Halmashauri za Wilaya, kusiwafanye wao kuleta Sheria Bungeni kwa lugha ya kuboresha, wakati ni lugha tu zinatumika! Maneno ni yaleyale tu, hakuna tunachoboresha, maneno ni yale yale ambayo yanatumika humu siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, kama wanataka kuhakikisha kwamba Sheria ya Manunuzi inafuatwa na kunusuru fedha za Watanzania; tena ndiko ambako ziko nyingi ambazo tunaweza tukanunua meli mpya, tunaweza kununua treni mpya, tunaweza kununua ndege mpya! Wale wote ambao tayari katika hesabu ambazo zimekaguliwa na *CAG* na wamebainika kwamba wamekiuka sheria na sheria iko wazi humu kwamba *however contravince any provision of this Act,* amevunja sheria! Hao ndio nataka kusikia wanachukuliwa hatua mara moja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu, ninawaomba chonde chonde tuwahurumie Watanzania. Watanzania wamechoka na kusoma magazeti, Kamati sijui ya nani yafukuza sijui watu gani! Mahesabu gani yakataliwa! Halafu kesho yake tunaendelea! Tunawapeleka wapi Watanzania?

Wakati Sheria ambayo Bunge tulitunga hapa, Sheria ya mwaka 2004 imeainisha kila kitu, ina meno yakutosha! Lakini leo! Niliwahi kusema kwenye Kamati kule kwamba, hivi tunapokuwa tumebaini huu ubadhirifu, tunakataa mahesabu yao, *what next?* Hiyo *what next* hiyo, ndio tunataka Serikali yetu ituoneshe kuanzia kesho; ili tuwe na nidhamu ya kuhakikisha kwamba hata hii Sheria ambayo tutaipitisha hapa leo ni pale ambapo wale wote ambao tayari wameshabainika katika matumizi mabaya ya fedha, wachukuliwe hatua. Tunawafahamu kwa

majina, tunawafahamu kwa sura na hata nguo wanazopendelea kuvaa kila siku tunazifahamu. Sio suala la kuhangaika, ni suala tu la kuwachukua na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria, chini ya sheria hii hii ya 2004 ambayo ina meno ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu, tukienda vijijini wananchi wetu wameshika matama yao, tukienda vijijini nyuso zao zimekunjamana, lakini wanaamini siku ya siku wanaamini kwamba Wabunge waliotuchagua ndio tutakaowafanya watoe viganja kwenye matama yao. Ndio tutakaowafanya nyuso zao zianze kuwa na furaha. Ni pale ambapo tutahakikisha kwamba fedha za wananchi, fedha za hao zinatumika kwa nidhamu na zinawaondolea matatizo yao. *(Makofi)*

Naomba Wabunge wenzangu muniunge mkono, tusikubali kupitisha manunuzi ya vyombo ambayo ni chakavu, vitaangamiza Watanzania. Ninaomba Wabunge tukubaliane, tuseme wale wote ambao wamebainika katika ubadhirifu kwenye mashirika, kwenye Halmashauri, lazima tusikie kwamba wamechukuliwa hatua. Vinginevyo hata sheria tunazopitisha hizi hazitatufikisha mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, huyu *Accounting Officer* ambaye sheria hii tunataka kutunga kwamba, ni yeye peke yake akiamua kwamba mazingira haya ni ya *emergence. Kwa hiyo,* anaamua kunafanyika *emergency procurement!*

Mheshimiwa Spika, uzoefu wangu unaonesha kwamba, hayo mashirika tunayopitia hesabu zao na hata wale wenzetu wa Idara za Serikali na Halmashauri za Wilaya, hawa ma-*Chief Executive Officers* ndio wanaobariki ku-*by pass* sheria hizi. Hao ndio wanaotoa Baraka! Sasa leo tena ndio tunasema kwamba, katika *emergence,* huyo huyo anayetoa Baraka hizi ndio aweze kuamua kwamba tununue katika *emergence! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaingia hasara kubwa sana. Ninaomba timu yote ya *Management* kwenye Taasisi za Serikali, wao wakae waone ni mazingira gani yana-*qualify* kuwa ya *emergence procurement.* Katika mashirika tunazo Bodi, ziangalie ni mazingira gani. Halafu wakimaliza wapeleke kwa *PPRA* kwa ajili ya *approval.* Vinginevyo tumekutana kule na ma-*Chief Executive Officers,* unawauliza kwa nini mmetumia fedha vibaya hapa? Anasema ni kwa sababu tu ya makosa ya kibinadamu! Huyo leo ndio tunataka akafanye maamuzi ya *emergency procurement!*

Mheshimiwa Spika, hivi kweli mwananchi kule kijijini anapokuwa amechukua kuku wa mtu, anayo haki ya kusema kwamba aah, ilikuwa ni kwa sababu ya njaa yangu tu ni ubinadamu, halafu wamuache? Lakini leo njaa za hawa ambao wako huku wanatuambia ni kwa sabbu tu za kibinadamu! Halafu tunawaacha! Maana yake nini? Waheshimiwa Wabunge, ninaomba Bunge hili tuwatendee haki Watanzania, tusimame imara, wananchi wana imani na sisi.

Sisi ndio tutaifanya Serikali yetu iweze kuyafanya yale ambayo wananchi wanayategemea kutoka katika Serikali hii. Lakini tukikubali maeneo haya ambayo kwa kweli Serikali imeyaleta ambayo kwa kweli yatawaangamiza Watanzania, hatutawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana wenzangu wote ambao wamenitangulia, Mheshimiwa Mwambalaswa, ameongea mambo ya msingi sana. Lakini kubwa zaidi ambalo amenikonga ni katika lile eneo la *PPRA.*

*PPRA,* wamekuwa mbali mno na udhibiti wao katika manunuzi haya, wamekuwa mbali mno! Mpaka nafikia hatua nasema, tutaunda *Regulatory Authorities* ngapi katika nchi hii? Yaani ifike hatua hata hawa ambao ndio *Regulatory Body,* tuwaundie *Regulatory Body* nyingine tena i-*regulate* hawa! Tutafika wapi?

Wamekuwa mbali mno! Wanatoa visingizio kibao! Mara hatuna *PMU,* mara hatuna *Specialist* wa manunuzi! Mara hatuna nini! Na wao wanakubaliana na sababu kama hizi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba *PPRA* wa-*take charge* Sheria hii na hata hii ambayo tunasema tunaifuta, yenye meno makali kwa uelewa wangu, wana uwezo wa kuwa-*summon* hata ma-*Chief Executive Officer* na kuwahoji juu ya njia za manunuzi. Kuwahoji namna wanavyotoa tenda na hata kuhamisha! Ana uwezo kwa mujibu wa hiyo sheria kuhamisha zile kazi za Kitengo cha Manunuzi kwa sababu mara kwa mara wanarudia makosa yaleyale, akazipeleka kwenye *Agency.* Lakini *PPRA* yetu hii, imekuwa na kigugumizi!

Mheshimiwa Spika, nadhani ninapokuwa ninazungumza hapa, huyo Mtendaji Mkuu ananisikia. Ahakikishe kwamba, meno tuliyompa hata kesho tumsikie kwamba anaunguruma! Aungurumapo simba hucheza nani?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii siku hii ya leo. Lakini pili, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kwa mara nyingine tena kuhudhuria Kikao hiki, ukizingatia takribani wiki mbili zilizopita nilikuwa nimelundikwa ndani na kubambikiwa kesi.

Nashukuru Mungu kwamba, hayakunikuta ya Mheshimiwa Lema ya kukataa dhamana. Kwa hiyo, nashukuru Mungu mimi nilijidhamini mwenyewe na leo hii nimepata fursa ya kufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwanza kwa kuleta sheria hii ili tuweze kufanya maboresho katika utaratibu mzima wa kufanya manunuzi katika nchi yetu.

Mengi wameongea wenzangu lakini mimi ninaipongeza sana Serikali kwa kuweka kipengele cha 53(3), ambacho kinapelekea katika kufanya *due diligence* yakutosha ya makampuni yanayokuja kufanya mauzo ya bidhaa mbalimbali hapa nchini kwetu.

Maana kipengele kama hiki kinatoa mianya ya kampuni za kipuuzi, ya kampuni za kifisadi, kama kampuni ya *RICHMOND* ambayo ilisababisha kuanguka kwa Serikali mwaka 2008. Mimi ninaipongeza sana Serikali kwa kuliona hilo na kuamua kulifanyia kazi katika maboresho haya yanayofanyika leo hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba pia nihoji kipengele cha 51(2) ambapo inapendekezwa *Local tenderers* wathibitishe kuhusiana na *professional* zao kama kigezo kimojawapo cha kuonyesha uwezo wa kufanya manunuzi. Kwa sababu mimi nachelea kuamini kwamba si lazima kila *tender* iwe ina watu wana *professional* fulani. Hii mimi naona inaweza ikawa ni kikwazo na kigezo cha kuwafanya Watanzania ambao ni wajasariamali wanaoanza kidogo kidogo kuweza kupata uwoga wa ku-*approach application* mbalimbali za *tender* ili nao waweze kukuza mitaji na hatimaye mwisho wa siku tuwe na wataalam wa ndani ambao wanamiliki kampuni kubwa na kuendesha miradi mikubwa ya maendeleo ya kizawa hapa nchi kwetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo lakini naona kwamba tatizo la nchi yetu kubwa sana si suala la kuwa na Sheria, si suala la kuwa na sera bali ni ukosefu wa usimamizi madhubuti wa Sheria na sera ambazo zinatungwa. Kwa mfano, kuna tatizo kubwa la ukosefu wa *accountability* ambapo unakuta sheria inasema hivi, watu wanafanya vingine, lakini mwisho wa siku hakuna anayeadhibiwa, hakuna anayechukuliwa hatua za kisheria na matokeo yake wengine wanaendelea kuiga kufanya vitendo vya uozo kama vile vilivyofanywa na wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano leo hii ukisoma katika takwimu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG),* utaona *compliance level* ya masharti yote ambayo ameeleza katika Sheria ya mwaka 2004 ya Manunuzi ni takriban asilimia 55 na haijawahi kuzidi asilimia 60 toka mkaguzi aanze kufanya hizo hesabu zake. Sasa katika hali kama hiyo maana yake manunuzi yanayofanyika kwa zaidi ya asilimia 40 hayafuati masharti ambayo yamewekwa na sheria ambayo ilikuwa ina *operate* kwa muda wote huo. Sasa mimi siwezi kuona kwamba kama hili ni tatizo la kisheria au la kisera, lakini naliona zaidi ni tatizo la ukosefu wa uwajibikaji, ni tatizo la uvivu au kile anachokiita Mheshimiwa Lugola, watu kutotumia meno yao vizuri ipasavyo, kwamba mtu anafanya maamuzi

kama anavyotaka kuyafanya kwa upungufu wake, lakini mwisho wa siku huyu mtu anaachiwa, anaendelea na shughuli zake *at large* au anahamishwa anapelekwa sehemu nyingine na mwisho wa siku tutakuja kutunga sheria nyingine kuboresha, kuongeza meno zaidi kwa *PPRA*.

Mimi sioni kama hili ni la msingi sana, lakini kwa kuwa ni mapendekezo yaliyoletwa hapa mbele yetu naamini Waheshimiwa Wabunge watatumia busara kuyaangalia na kuyachuja na hatimaye kuona kama inafaa kuwa na sheria mpya kama hii ambayo imeletwa mezani kwetu leo hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sheria hii itungiwe sera na kwenye sera viwekwe vipengele ambavyo vitakuwa vinaelezea kwa uwazi kabisa na kwa umakini ni jinsi gani watakaokiuka sheria watashughulikiwa. Lakini pia pengine utengenezwe utaratibu wa jinsi gani sisi kama Bunge ambao tuna dhamana ya kusimamia Serikali tunaweza tuka-*enforce* utekelezaji wa Sheria kwa kuibana Serikali ndani ya Bunge na hata ikiwezekana kwenye vikao vya Baraza vya Halmashauri. Kwa sababu unakuta kwa mfano kuna baadhi ya Halmashauri kwa mfano kule ninakotokea mimi wanafanya maamuzi yanapitishwa, Madiwani hawakuhusishwa, Mwenyekiti anakuwa *compromised* pengine ana saini kwa niaba ya Baraza halafu mwisho wa siku mnakuja kuona kitu kimeshafanyika. Sasa sheria za namna hii, maamuzi ya namna hii kuna ya kuyatengenezea sera ya jinsi ya kuyatekeleza na jinsi ya hata ya kuyapindua kuliko kuacha mambo yawe yanakwenda tu hovyo hovyo, maamuzi yanafanyika hovyo hovyo na mwisho wa siku madhara yanajitokeza katika miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge unamaanisha itungwe sera au kanuni za utekelezaji?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** *I mean* kanuni za utekelezaji, *sorry.*

**SPIKA:** *Okay*, ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, *regulations*, naomba nisiendelee zaidi niishie hapa nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa nimuite Mheshimiwa David Silinde na nafikiri Mheshimiwa Dokta Charles Tizeba atafikiwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nasimama hapa nilikuwa nafikiria, awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa na nini la ziada ambalo lilimfanya aliweza kununua ndege mpya, mabehewa mapya, meli mpya, tofauti yake yeye ni nini na awamu ya nne? Wakati Mwalimu Nyerere anachukua nchi hii kulikuwa na wasomi wachache, walijali uzalendo wakanunua vitu vilivyo vipya. Lakini leo hii ambapo wasomi wapo wengi kuna Maprofesa na Madaktari, Bungeni tumejaa wasomi kibao, lakini tunafikia mahali mpaka sasa kuwaambia Watanzania tumewachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anajaribu kujenga hoja ili tuhakikishe kwamba Sheria hii inapita, ameelezea kwamba amejaribu kuonyesha kwamba utaratibu utafuatwa. Lakini hali ambayo inaelezea uhalisia, Sheria ya awali ya Manunuzi ambayo ilitaka tununue vitu vipya ilikuwa imeshashindwa, tuna mifano ya Halmashauri ambayo imenunua vitu chakavu, magari chakavu, mifano hiyo ipo wazi, lakini leo tunataka sasa, tunasema jamani tupitishe Sheria kwa lengo moja tu kwa sababu hii siyo Sheria tu hatuzungumzii Sheria kwa ujumla tunazungumzia kipengele cha manunuzi ya vitu vikubwa, mabehewa, *engine* za *train*, ndege pamoja na meli. Lakini ukitaka kuangalia hivi ni vyombo vya usafiri vinavyobeba mamia ya Watanzania au ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii siyo sawa na gari dogo, meli inayobeba zaidi ya watu 2,000, ndege inabeba zaidi ya watu 100 au 500 sasa hivi ndiyo vitu chakavu, tunanunua chakavu, maana yake ni nini kwamba muda wake sasa umekwisha. Wazungu wenzetu tunapokwenda kununua hivi vitu

huwa kabla havijaisha muda wake huwa wanatoa *notice* kwa wale wanaovitumia, chombo chako cha usafiri, meli, ndege, treni kufikia mwaka 2011 hatuhitaji iendelee kutumika nchini, mwisho wake ukishafika wanasema sasa nani ambao wakafe na hivi vyombo? Wao havijawaua wapelekee Watanzania. Hapa tunachotafuta ni kuunda tume tu, ndicho ambacho nakiona hapa, ni miradi ndiyo ninayoiona hapa hakuna kitu kingine. Kwa sababu mwisho wa siku tutakuja tena hapa nani alipitisha hii Sheria, CHADEMA tukichukua nchi mwaka 2015 lazima tuikatae japo na sasa hivi tunaikataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri, tujaribu kuwa na uzalendo, hata kama kweli tuna nia na Watanzania hatuhitaji kununua vitu chakavu, Watanzania ngoja niwaeleze, Watanzania hawahitaji ndege, Watanzania hawahitaji meli, Watanzania hawahitaji treni, Watanzania wanachohitaji ni maji safi na salama, huduma bora za afya, barabara zinazopitika saa 24, elimu bora kwa Watanzania wote, maisha bora kwa kila Mtanzania ndiyo Watanzania wanayoyahitaji. Haya madogo yametushinda, tunataka kubeba makubwa tunalipeleka wapi hili Taifa?

Mheshimiwa Spika, kinachoniuma mimi ni kuingia katika hili Bunge kila siku kuendelea kupitisha vitu ambavyo havina mantiki. Sisi Wabunge wa CHADEMA na CHADEMA kwa ujumla kama chama, kuna wakati tuliandamana kabla ya Bunge la Bajeti kwamba endapo mitambo ya *IPTL* na *DOWANS* itanunuliwa tutaandamanisha wananchi nchi nzima, hatuwezi tukanunua mitambo chakavu, kwa sababu Sheria ya Manunuzi hairuhusu, tuliahidi kitu kama hicho, Serikali ikasikia kwa sababu hapa nimekuja kugundua kweli maandamano yana faida na huwa mnayasikia japo huwa mnayapinga pinga lakini huwa mnayasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmejaribu kubadilisha sasa kuiondoa mitambo ya *DOWANS* na *IPTL* kuleta kwenye mauaji ya Watanzania, mimi haya naweza nikaita ni mauaji kwa sababu tunaingia kwenye *risk* yaani ni sawasawa unaingia kwenye tanuli la moto unategemea kufa ama kutokufa wakati jibu lipo wazi kwamba unapokwenda kwenye kitu chochote chakavu maana yake unaelekea kwenye hatari, *risk* ya maisha ya Watanzania tunaendelea kuiweka katika mazingira magumu, kwa hili mimi siwezi nikaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama watu wamekaa wakafikiri, tunapoleta vitu chakavu maana yake tunasema sasa Tanzania ni shimo la takataka *(damping place)*, kwamba ninyi watu wa nje mkitaka ku-*damp* vitu vyenu leteni Tanzania, Japan sasa hivi wanapanua miundombinu ya reli, sasa kwa sababu wanapanua miundombinu ya reli wanataka kuleta reli mpya za kisasa zinazotumia umeme, yale mabehewa chakavu unategemea yatakwenda wapi? Si Tanzania? *That is what we expect,* yatakuja huku wala sioni nchi nyingine. Kwa hiyo, ikija kutokea kama zile ajali za treni hapa Dodoma tusishangae ni vitu ambavyo tulivipanga, yakija yakitokea mambo ya *MV Bukoba* tusishangae ni vitu ambavyo tulivipanga, hatuwasaidii Watanzania. Ni heri tukaendelea kubaki bila ndege, tukatumia hizo wanazo wenzetu *Precision Air*, *Air 540,* na mambo mengine wanatusaidia bado. Si lazima tuwe nazo sisi kama Serikali, kama tumeshindwa kuzihudumia, tusubiri watu wengine watakaoweza kuzihudumia wao waje wafanye hiyo kazi. Kwa hiyo, mimi ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, jaribuni kuwa makini, hatuhitaji ndege, tunahitaji ajira kwa vijana, kwa watu ambao wamesoma lakini hawajapata ajira ndiyo mambo ambayo tunahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii ukisoma taarifa ya Benki ya Dunia ya leo inasema gharama za maisha zimepanda, dunia nzima gharama za maisha zimepanda na thamani ya shilingi ya Tanzania inaendelea kushuka, hili linaeleweka wazi kwa Wabunge wote na Rais naye anajua. Na kama gharama ya maisha inaendelea kupanda, taarifa inasema Tanzania inaelekea kufilisika kama ilivyo Ugiriki, kama ambako inaelekea Italia.

Sasa sisi watu wa nchi ya mwisho huku hii ni taarifa ya Benki ya Dunia inasema hivyo na kwa nini ime-*state*, kwa nini tunaelekea kufilisika kwa sababu tunaagiza zaidi nje ya nchi ndiyo haya ya kununua mabehewa yaliyooza, kununua *engine* za treni zilizokufa ndiyo haya yanayosabisha sisi tuendelee kufilisika. Sisi tulikuwa tunataka tutoe kama wito kwamba badala ya kutuwekea sheria ya kununua kila siku tuna-*import* zaidi, mnatakiwa sasa mje na sheria ambayo lazima i-*limit* yaani kwamba kama kuna vitu vinapatikana ndani ya nchi viwekewe sheria ni lazima

vinunuliwe kwanza, tununue vitu ambavyo havipo ndani ya nchi. Lakini sasa kuna vitu kama mbao zipo ndani ya nchi, Sheria ya Manunuzi tuna-*import South Africa* kwa sababu mbao za Mgololo pale ni bei kubwa, *what are we doing? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanya nini, Sheria za Manunuzi zinaruhusu kwenda kufuata kitu *South Africa,* lakini ndani ya nchi tunazo mbao zipo Iringa pale Mama Spika unafahamu hili tunashindwa kufanya hivi vitu, ni vitu vya namna gani mnategemea nchi itaendelea? Lakini si kwamba tunatafuta wenzetu wanavilivyo bora hapa mbao hizi tunazokalia wote ninyi mnajua, mbao zao tunakaa miaka miwili zimeharibika. Siyo bora kuliko za kwetu lakini kwa sababu ziko *cheaper* na kwa sababu ya *ten percent* basi tupo tayari kuangamiza watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufika kwa utaratibu huo, lazima tuwe na uzalendo, Sheria tu yenyewe ya Manunuzi Mheshimiwa Waziri hili lazima ulitambue, tulipokuwa Jimboni tunazunguka, kufanya ziara, mimi Mbozi, Mbozi Magharibi kule Jimboni kwangu, wananchi wanauliza hawajui hata mzabuni ni nani, hawajui mzabuni ni nani? Wananiuliza Mheshimiwa Mbunge mzabuni ni nani, mzabuni namjua mimi Mbunge na wewe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Spika, lakini watu wa kijiji hawajui mzabuni ni nani, wanauliza mzabuni anafanya kazi gani kwa sababu tumechangishwa fedha, mlango ambao sisi hapa kijiji kwetu Kamsamba, tunanunua shilingi 15,000 kwa mzabuni tunanunua 150,000 *who is* mzabuni? Wananiuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dirisha ambalo lilikuwa linauzwa kwa shilingi 10,000 mpaka shilingi 20,000 tunanunua kwa zaidi ya shilingi 75,000 huyu mzabuni ni nani ndiyo miradi, ndiyo utaratibu fedha ya nchi imekuwa ikiisha kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nagombana na watu kwenye suala la Mfuko wa Jimbo, umegawa Mfuko wa Jimbo unakwenda kukagua mradi wa fedha ya Mfuko wa Jimbo ulikokwenda tunaambiwa wamelipwa wazabuni kwa sababu walikuwa wanatudai, kazi imeshindwa kufanyika, mnatuambia sasa tunajenga ama tunabomoa nchi. Mara nyingine walimu wangu wa dini walinifundisha kwamba mtu anapofilisika huwa hajitambui, ila watu wa pembeni huwa wanajua kwamba anafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawajui kwenye benki ana kiasi gani lakini wanatambua kabisa kwamba huyu anafilisika na kwa sababu yeye hataki kujua kabisa kwamba ninafilikiska huwa anajenga jeuri ya kibinadamu kwamba sifilisiki, anajaribu ku-*maintain* maisha aliyonayo. Lakini siku ya mwisho shilingi ya mwisho ikishamuishia ndiyo anajua kwamba kweli leo nimefilisika na Mwenyezi Mungu aliye mkuu kuliko wote huwa anawapiga upofu watu wa namna hii, huwa hawajitambui. Unafikia mahali unachukua maamuzi bila kujijua, hatuwezi kujenga Taifa namna hii. Mimi nahisi wengi mko katika hali hii, mnafilisika bila kujitambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kufilisika huku ni kwa sababu ya jeuri ya kibinadamu kwamba chochote wanatakachokiongea hao hatuwezi kukisikiliza, mtu anakuangalia kwa dharau, lakini tunachoeleza ndiyo ukweli, haya ndiyo maamuzi ya Watanzania, hatuhitaji kuendelea na huu utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la meli, ndege, mabehewa ya treni pamoja na *engine* zake, Mheshimiwa nafikiri ulisitisha. Marehemu Mwalimu Nyerere alisema mtu anayeanza kula nyama ya mtu hawezi kuacha tena, tutatoka kama tumeweza kwenye meli kwa nini tusije kwenye magari? Kwa nini tusije kwenye viti, ningewaelewa sana mngesema Sheria ya Manunuzi ya viti, *procurement* hii tu ambayo tuipitishe tununue vitu chakavu ili tukienda kwenye ofisi yako Mkulo tukute viti chakavu uone kama wewe utakaa pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo vitu ambavyo tunavitaka, vitu ambavyo vinaonekana, kwa nini nyie msitake vitu chakavu mnataka watu tu wale Watanzania wa hali ya chini? Hatuwezi kujenga hili Taifa kwa mfumo huu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninawaomba, ninawaomba sana sheria hii tusiipitishe, hicho kipengele maeneo mengine hayana tatizo sana, ni mazuri lakini kipengele cha kununua vyombo vya usafiri vinavyobeba Watanzania wengi ni hatari, hatuna udharura na meli, hatuna udharura na ndege,

hatuna udharura na treni, hivyo vitu hatuna udharura navyo, tumekaa bila kuwa navyo kwa miaka mingi sana na Watanzania maisha bado yanaendelea. Tujengee Mheshimiwa Magufuli, tujengee barabara tutatembea kwa magari, magari ni mengi yamezidi kuliko uwezo, kwa hiyo, tujengee hivi vitu, kwa sababu meli, ndege ni *luxury, luxury goods* ambavyo mtu wa chini hawezi kupanda, watakaopanda ni wenye uwezo tu, Wabunge na Mawaziri na watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, twende tujengeni barabara, tuleteeni huduma bora za afya, tuleteeni maji, mkishindwa kufanya hivyo sisi maandamano tunaendelea na jana Mheshimiwa mmoja alikuwa tunaomba mtuwekee maeneo kabisa tuendelee tukalale vizuri zaidi kule, labda hapo mtaweza kutuelewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini hatutaki kilio hiki Watanzania tuwafikishe mahali ambapo nchi za wenzetu kama Libya, Misri wamefika tunataka kwa sababu Tanzania yetu ni nchi ambayo ilitengenezwa kwa umoja, wazee wetu akina Mwalimu Nyerere walichukua mamlaka bila kumwaga damu na tusingependa Tanzania ifikie huko, Watanzania wanachoka na wanalijua na ninyi wenyewe mnayafahamu haya, ninyi wengi ni marafiki zetu na ndugu zetu sikilizeni watu wanalia, makanisani mnakosali na misikitini mnajua Mashekhe wanakashifu, wanasema Serikali imeoza, Mapadri, Maaskofu, Wachungaji wanakashifu wanasema Serikali imeoza mnayasikia lakini mnashindwa kuyatekeleza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha tena leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakuwa na uhuru wa kusema hapa ndani, lakini naamini kabisa uhuru huo haupaswi kutumika vibaya kwa maana ya kuupotosha umma, uhuru tunatakiwa tuutumie vizuri kuelewesha umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haingii akilini kwangu kusikia kwamba treni ni *luxury* kwa Watanzania, mimi naamini zaidi kwamba barabara huenda ndiyo *luxury* kwa Watanzania na siyo treni, treni ni usafiri ambao watu wote kabisa wanaweza kumudu na kwa bei rahisi sana kuliko barabara. Bei rahisi kwa watumiaji, bei rahisi kwa Serikali na kila mtu, kwa hivyo niombe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunasema hapa tuwe waangalifu kidogo na maneno tunayowapelekea Watanzania kwa sababu yanaweza yakawapotosha na kuamini kwamba tunayoyasema kwa vile wametuchagua basi ndiyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada ulio mbele yetu unazungumzia jambo kubwa sana katika uhai wa Serikali kwa sababu kwa takwimu zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati, ukijumlisha manunuzi katika miradi ya maendeleo na manunuzi katika matumizi ya kawaida ya Serikali utaona karibu 80% ya fedha yote tunayoidhinisha Bungeni inatumika katika manunuzi ya umma. Kwa hiyo, ni jambo kubwa ambalo tunatakiwa kuli-*approach* kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo matatu, moja ni eneo la miradi mikubwa ya umma. Katika eneo hili fedha nyingi sana ya umma inatumika, nitolee mfano wa Bajeti tuliyoipitisha miezi miwili iliyopita, barabara peke yake zimetuchukulia karibu trilioni moja na nusu. Sasa hizi fedha ukizitazama zitakavyotumika karibu 90% itakwenda kwenye makampuni ya nje ya nchi yetu, na sisi hatujajiwekea utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba faida itakayopatikana kwa hayo makampuni basi angalau kwa kiasi ibakie ndani ya nchi ili kuwa kama *stimulus* ya uchumi wetu wa ndani ya nchi, faida yote itakwenda nje kwa maana kwamba tunakusanya kodi ya wananchi kuwanufaisha watu wa nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina mapendekezo, nianze kutoa mfano ili nieleweke vizuri. Leo tunapozungumza Wakala wetu wa Barabara anadaiwa na makampuni karibu shilingi bilioni 450 na kati ya hizo shilingi bilioni 450 ni shilingi bilioni 37 tu ambazo zinadaiwa na kampuni za ndani ya nchi na shilingi bilioni 413 ni fedha inayodaiwa na makampuni ya nchi za nje. Maana yake faida

yote itakayopatikana kutoka kwenye hiyo fedha shilingi bilioni 450 itakwenda nje kupitia mishahara ya watumishi, faida na manunuzi ya vifaa na mitambo ambayo kampuni hizi za nje zitanunua kutoka kwao.

Kwa hiyo, sisi katika uchumi tutakachoambulia kwa juu sana ni hizo shilingi bilioni 37 ambazo zinadaiwa na kampuni zetu za ndani, lakini hii yote ni kwa sababu Sheria hii haijaelekeza namna gani Taifa linufaike na manunuzi yanayofanywa kupitia fedha ya umma.

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo yafuatayo; kwamba kazi zote kubwa yaani *contracts* zote kubwa za Serikali au zifanywe kwa ubia kati ya kampuni za nje na kampuni za ndani ili faida inayopatikana igawanywe au kama hilo ni gumu kampuni za nje zilazimishwe kwa asilimia fulani kutoa kazi yaani sijui nisemaje, lakini ni *sub contract* kwa kampuni za ndani ili angalau sehemu ya faida ile ibakie kwa kampuni zetu. Lakini kama hilo nalo linakuwa gumu basi tuweke utaratibu ambao nchi nyingine za Afrika zimefanya kulazimisha kampuni za nje kufanya kitu kinaitwa *Management Contract* peke yake lakini *actual execution* ya hizi kazi ifanywe na kampuni za hapa ndani kwa usimamizi wa kampuni za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo faida nyingi lakini tukichukua moja ya hizi taratibu kwanza mitaji itabaki nchini lakini tutazijengea uwezo kampuni zetu za ndani sana ambalo ni jambo kubwa sana katika kuboresha na kuimarisha uchumi wetu. Lakini pia tutadhibiti mfumuko wa bei au kushuka kwa thamani ya sarafu yetu kwa maana sasa hivi kwa mfano hizi shilingi bilioni 413 zote zitakwenda nje au zitahitaji dola ili kampuni hizi ziweze kulipwa kwa sababu kampuni za nje hata wakilipwa kwa shilingi lakini kuna *amount* ambayo wanakuwa wanadai walipwe kwa fedha ya kigeni na kunapokuwa na *demand* kubwa ya fedha ya kigeni ndiyo shilingi yetu inazidi kupoteza thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi kama *South Africa* na Botswana wao walikwishaweka sera za namna hii, *South Africa* ilikuwa inaitwa *Black Empowerment Scheme* ambapo kampuni zote ambazo hazikumilikiwa na watu weusi zilikuwa zinalazimika kuwapa kazi za utekelezaji wao wakisimamia kampuni zinazomilikiwa na watu weusi angalau katika kuwainua na kuwajengea uwezo. Botswana walichofanya ni *Citizen Empowerment Scheme,* kwamba wewe mgeni ukija Botswana unalazimika kujiunga na Mswana kwanza katika kutekeleza kazi ili kumjengea uwezo na kuhakikisha kwamba faida utakayoipata kutokana na manunuzi ya umma inawanufaisha pia wananchi wa Botswana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninaomba kuchangia katika Muswada huu ni la hizi hizi kampuni kutosaidia katika kukuza ujuzi wa Watanzania wanaoajiriwa katika shughuli ambazo zimetokana na manunuzi ya umma. Uingereza nadhani wamekwishapitisha tayari Sheria hii ambayo inazilazimisha kampuni siyo zote, lakini zile ambazo zinapata mikataba mikubwa ya umma kutenga asilimia ya zile fedha katika kuendeleza ujuzi wa watu wanaoajiriwa katika kampuni hizo. Hii itatusaidia sana hasa ukizingatia kwamba miezi miwili iliyopita hapa hapa Bungeni tulikubali kuondoa sehemu ya *Skills Development Levy* kuipeleka kwenye mfuko wa mkopo katika elimu ya juu. Kwa maana hiyo, hii *cadre* ya katikati ya ujuzi na ufundi sanifu ikawa imeachwa ikizidi kupungukiwa fedha kwa ajili ya kuiendesha. Sasa mlango wa kutokea katika hilo ninauona upo hapa ambapo kampuni hizi zinapopata mikataba mikubwa basi zilazimike kwa mujibu wa Sheria kutenga fedha tuseme 1% au hata kama ni 0.5%, lakini fedha hiyo iwa-*train* watu watakaokuwa wanafanya kazi pale wasio na ujuzi kamilifu au wenye ujuzi mdogo ili kuwakweza zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala hili lina manufaa mengi sana, kampuni ikimsomesha pale kwa pale mfanyakazi wake anakuwa mwaminifu zaidi kwa hiyo, kampuni na atafanya kazi vizuri zaidi. Lakini pia itakuwa imeisaidia Serikali kupambana na kundi kubwa la vijana ambao hawana ujuzi, wanaendelea kuwa vibarua katika hizi kampuni kwa sababu tu hawana ujuzi, wangekuwa na ujuzi ukibarua ungekwisha. Katika utaratibu huu ambao huenda labda unahitaji kabisa sera na siyo kubadilisha tu kifungu katika Sheria hii, lakini nadhani ni jambo ambalo tukilitazama vizuri mbele ya safari linaweza likatusaidia sana katika kukuza ujuzi wa vijana wengi ambao wanahitimu shule za sekondari ambao hawana taaluma yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninaloomba kuchangia katika Muswada huu ni kifungu cha 66. Ukikisoma kinasema; *"Where the public interest demands that railway, machinery, civilian or military ship and civilian or military aircraft that has been used..."* hiyo ni ya zamani. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba inaishia kwa kusema; *"upon approval by the Cabinet..."*

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kabisa na hii sentensi kwa sababu kuruhusu Baraza la Mawaziri lijiingize katika michakato ya manunuzi ni kui-*expose* Serikali kwa lawama ambazo siyo za lazima, na hapa nikizungumza Serikali maana yake tunataka kumtanguliza Rais kwenye *falling line* kwamba *Cabinet* ikisha-*approve* katika utekelezaji halafu watendaji wakakosea wakanunua kitu chakavu kisicho na ubora uliotarajiwa basi lawama yote iende kwa Rais kwa sababu itakuwa inasemekana kwamba yeye ndiye aliyeidhinisha manunuzi.

Mimi ningependa sana Rais awe mtu wa mwisho kulaumiwa katika jambo lolote la *public* na siyo Sheria tuitunge leo ambayo inamtanguliza yeye kuwa katika lawama na Baraza lake la Mawaziri, tuelewe kwamba huyu ndiye Kiongozi Mkuu wa nchi, kwa hiyo, hatuwezi kumtengenezea mazingira ya kulaumiwa kila siku jambo linapoharibiwa na utendaji ulio chini yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba sana Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atafute njia nyingine ya kuliweka hili kama kifungu hiki kitapita ingawa ninaona hapa kinakataliwa, kama ikipelekea kinapita basi angalau Baraza la Mawaziri lisihusike katika ku-*approve* ununuzi wa hivi vifaa chakavu hata kama vinalazimika kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nisije nikampa mtu dakika kumi halafu akasema ananidai tano. Kwa hiyo, mimi naahirisha kikao hiki mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) alikalia Kiti*

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

***Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011***
***(The Public Procurement Act, 2011)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala kwenye Muswada uliopo mbele yetu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, ambapo hapa nina wachangiaji watakaoanza. Mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Dokta William Mgimwa.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu Na. 68(8), leo asubuhi Mbunge mmoja alipokuwa anachangia alisema kwamba Serikali ya Tanzania aidha, itafilisika au inakaribia kufilisika. Kufilisika kwa Serikali maana yake ni hali ambayo Serikali inashindwa kulipa madeni yake, aidha, kwa kuwa uwezo wake wa kukusanya mapato ni mdogo au Taifa hilo halikopesheki, wala halina heshima ya kuweza kupata wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa ya *World Bank* hapa ambayo ningependa baadaye nikukabidhi mezani kwako ambayo inaisafisha Tanzania kwamba ni moja ya nchi zinazoheshimika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilichotaka kusema ni kwamba, kauli ya wenzetu wa upinzani kuwa Tanzania ni Taifa lililokaribia kufilisika haina ukweli hata kidogo na inakosa kabisa takwimu za kudhihirisha. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kupuuza kabisa hilo. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ismail Rage, kwanza kupitia Kanuni hiyo na Mwongozo uliouomba ni sahihi. Lakini nilitaka tu niseme kwamba wakati mwingine hatuhitaji sana kuchelewesha mambo. Nitoe tu rai kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba wakati mwingine lugha tunazozitumia na hasa zile zinazoumiza heshima ya nchi yetu kwa kutumia Bunge ni jambo linalohitaji chochote unachokisema uwe na uhakika nacho, uwe umefanya utafiti na kiwe ni kitu ambacho kinaaminika na kipo katika taarifa rasmi.

Sasa kama kweli jambo hilo lililosemwa ni kinyume, kama tu kuna ushahidi, lakini hata mimi jana nilikuwa nasoma gazeti kwamba uchumi wa Tanzania uko *very stable* na kwamba unapanda. Pamoja na vurugu zote zilizopo duniani lakini sisi tuko salama, hatujaathirika sana. *(Makofi)*

Sasa kwa hili ulilolisema mimi sioni haja ya kutoa Mwongozo, labda baadaye, niseme tu Waheshimiwa Wabunge, niombe sana na Mheshimiwa Ismail Rage ukubaliane tuwe makini tunapotoa kauli ambazo zinaumiza heshima ya nchi yetu. Ukisema nchi itafilisika wewe mwenyewe hubakii salama. Sidhani kama zina uhakika. Kama Mheshimiwa David Silinde utakuwa tayari kutoa ushahidi huo labda useme, lakini napenda nitoe rai kwamba ni jambo zito na kubwa.

Sijui Mheshimiwa Silinde unasemaje?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kukirudia kusema ni kwamba, Tanzania inaelekea kufilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kutoa ushahidi kwa kupitia vidhibiti hivyo hivyo mlivyovitumia vya Benki ya Dunia. Nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Ismail Rage muda mfupi uliopita, tafsiri yake nyingi ameandika kwa Kiswahili, ni jambo ambalo nilikuwa namwambia ni la kawaida, lakini uhalisia utabaki kuwa uhalisia. Uchumi hauwezi kupanda wakati Watanzania maisha yao yanaendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika na ulinganisho unaoufanya, lakini jambo hili basi Mheshimiwa Spika, atalitolea Mwongozo muda utakaokuwa unafaa. Sisi tuendelee.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Natumia Kanuni ya 68(1) naomba ninukuu; "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu", ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokukwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia sasa kwenda kwenye Kanuni ya 64(1)(a) kwamba, "hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli." Wakati Mheshimiwa Ismail Rage ameomba Mwongozo hapa, ame-*attack* kauli za Wabunge wote wa Upinzani kwamba, tunatoa taarifa ambazo siyo sahihi. Naomba asahihishe kauli yake kwa sababu siyo Wabunge wote wa Upinzani, ni Mheshimiwa David Ernest Silinde peke yake. Atutake radhi Wabunge wengine wa Upinzani kwamba ndiyo ambao tumeweza kulipotosha Bunge na Watanzania wote wanatuangalia hivi sasa. Naomba suala hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Rage alichokifanya alimtaja kabisa, alimtaja kabisa ila…

**MBUNGE FULANI:** Hakumtaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rage, kama hukumtaja mchangiaji aliyekuwa anasema na mimi nilisikia wenzetu wa Upinzani, nadhani kuna haja ya kuweza kusahihisha ili ile hoja yako ambayo inangojea Mwongozo wa Spika iwe *specific.*

Mheshimiwa Rage, unaweza kufanya hivyo?

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Ninamaanisha ndugu yangu Mbunge wa Chama cha CHADEMA, siyo wote. Kwa hiyo, naomba radhi kama…

**MWENYEKITI:** Mtaje kama ulisikia na unamjua.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Silinde.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Nataka kumthibitishia kwamba ninayo *version* ya Kiingereza ambayo imetolewa na *World Bank* tarehe 7 Novemba, mwaka 2011. Hata akitaka yeye binafsi naweza nikampa kwa taarifa zaidi.

**MWENYEKITI:** Tumesema tutalitolea Mwongozo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Sasa kama nilivyosema ataanza Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda na baadaye Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu. Naomba kabisa kwanza ku-*declare interest,* mimi ni *Committee member* wa Fedha na Uchumi. Naomba kuchangia katika mambo manne katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nitazungumzia juu ya manunuzi ya dharura *(emergency procurement).* Jambo la pili, nitazungumza juu ya Muswada unavyozungumza kuhusiana na *procurement of used properties*, nitazungumza juu ya majukumu ya Madiwani katika shughuli hii ya manunuzi, halafu mwisho nitamalizia juu ya *e-procurement. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa sehemu ya Kamati kama alivyosema Mwenyekiti wetu asubuhi wakati anawasilisha maoni ya Kamati, Muswada huu tuliurudisha mara mbili kwa sababu nyingi ambazo zinahusiana na haja iliyokuwepo kwa ajili ya kuuwasilisha na kuufanya ulingane na matarajio ya Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, e*mergency procurement* ambayo ipo ndani ya *section 65* inazungumza kwamba, chini ya *section* hiyo atakayekuwa na mamlaka ya kutambua umuhimu wa *emergency* (dharura) atakuwa ni *Accounting Officer*. Ilituwia vigumu kufikia muafaka namna gani tunaweza tukawa pamoja na Serikali katika hilo, kwa sababu tuliona kwamba jukumu hili kumwachia *Accounting Officer* ndiye a-*determine* hali ya *emergency* ilikuwa katika hali ya hatari kidogo. Kwa sababu tunavyofahamu *Accounting Officer* ni binadamu, *is an individual*. Kwa hiyo, mawazo ya Kamati yalikuwa jukumu hili liwe katika mikono ya walio wengi, na tukapendekeza iwe *tender board* au *management team* kwa ajili ya kuondoa uwezekano wa athari zinazoweza zikatokana na wazo la mtu mmoja. Huu ulikuwa ushauri ambao tumeuweka mbele ya Serikali. *(Makofi)*

Jambo la pili, ununuzi wa vitu vilivyotumika. Wote tunafahamu Muswada wa awali ulikuwa umependekeza *used properties* kwa maana ya mitambo na mashine zilizotumika. Lakini baada ya kuwa wameenda kubadilisha tena, sasa wamelenga kununua vitu ambavyo viko *very specific* ambavyo ni meli, ndege, mabehewa na vichwa vya treni. Hoja kubwa iliyo mbele yetu ni

matumizi ya maneno, kitu gani kinazungumzwa, *used assets* kwa maana ya mali iliyotumika au mali chakavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliona kwamba kinachoweza kuwa na mantiki ni mali iliyotumika lakini yenye *specified period* ya *use*, si mali chakavu. Nimeona nichukue nafasi hii kutoa ufafanuzi wa hoja za Kamati. Tunachokiona kinaweza kuwa na msingi ni mali iliyotumika ambayo imetumika kwa kipindi fulani ambacho *due diligence* imethibitisha kwamba inaweza ikatumika, lakini si mali chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua ununuzi wa mali chakavu unaweza ukawa na athari walau nne au tatu. Kwanza, kununua mali chakavu tunaweza tukaleta athari kwa watu, kwani tukinunua ndege iliyochakaa, meli ilichokaa, behewa au kichwa cha treni kilichochakaa tunaweza tukahatarisha maisha ya watu. Wote tuliliona hilo na ndiyo maana tukazingatia neno *used* ambalo *due diligence* ita-*prove* kwamba bado kina thamani ya kuweza kutumika katika hali ambayo ni *effective.* Vilevile, ukinunua mali chakavu unaweza ukajiweka wewe mwenyewe katika matatizo ya *maintenance*. *Maintenance* ya mali chakavu ni kubwa kuliko *maintenance* ya kitu ulichonunua kikiwa kipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya tatu ukinunua kitu kilichochakaa vilevile ufanisi wa huduma ya chombo hicho ni mdogo kuliko ufanisi wa chombo kipya. Hilo tulilitambua na tukakwepa kulenga kununua mali chakavu. Tukasema kama Serikali ina hoja ya kununua kitu kilichotumika kwa sababu ambayo inaridhisha na imepitia *due diligence,* basi ilenge kununua mali iliyotumika katika *specified period of time*. Hii itamkwe kama ni miaka mitano au sita au minne kulingana na *effective use* ya aina ya chombo hicho, lakini siyo mali chakavu. Nimeona niliseme hili ili kuweka hoja vizuri kama tulivyoona wenzenu tunaotoka katika Kamati ya Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kulingana na hili lilitokana na hoja iliyoletwa na Serikali kwamba ili kuona ununuzi huo utakuwa salama, basi uidhinishwe na *cabinet.* Hoja inayokuja ni kwamba, tukiruhusu idhini itoke kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri, ambalo liko chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais, basi tutakuwa tumeleta matatizo ya ku-*manage process.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri mahitaji ya idhini yaelekezwe kwa *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA).* Kama *PPRA* itakuwa haina uwezo basi *capacity building* ielekezwe kwa *PPRA* ili iwe na uwezo wa kuwa na *all required competencies* za kuhimili kuidhinisha vitu vya namna hii, lakini siyo Ofisi ya Baraza la Mawaziri kwa sababu pale kwa kusema kweli tutaleta matatizo katika Ofisi ya Rais katika kuhoji. Sisi kama Kamati tunaona si vizuri. Kwa hiyo, ni vizuri basi ku-*empower PPRA* ichukue nafasi hiyo kwa maana ya kuipa *capacity*, kama ni *training* basi ielekezwe huko kuwa-*train* vizuri ili wawe na uwezo wa kushughulikia shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni majukumu ya Madiwani ili kusaidia kuona kwamba mchakato wa manunuzi unakuwa kama matarajio ya wananchi na sisi ambao tuna-*float* hizo *tenders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuna malalamiko mengi kama walivyosema wengine kwamba kuna wizi mkubwa sana unatokea, lakini matokeo ni kwamba tunakuja kugundua baada ya kuwa wizi umefanyika.

Sisi kama Kamati, tuliona kwamba kuna umuhimu wa kuangalia namna gani Baraza la Madiwani linaweza likawa sehemu ya kuzuia kabla athari hizi za wizi hazijafanyika. Pendekezo letu, tulipata matatizo kidogo namna gani kuliingiza katika Sheria. Lakini, pendekezo ni kwamba iwekwe *provision* ndani ya Sheria itakayoelekeza, Waziri atengeneze kanuni zinazoelekeza Baraza la Madiwani kwa kutumika Kikao cha Kamati ya Fedha, namna ya kutathmini na kuchunga athari zinazoweza kutokana na manunuzi katika ngazi za Halmashauri. Kwa hiyo, ni suala ambalo tayari na Waziri ameshalieleza, lakini na sisi tunaliunga mkono na ndiyo tuliolipendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni manunuzi kupitia *e-procurement. E-procurement* kama ilivyoelezwa ni matarajio kwamba kwa ukuaji wa *technology* duniani, na sisi kama sehemu ya dunia, hatuwezi tukakwepa matumizi ya mtandao katika manunuzi. Lakini kunahitajika maandalizi mazuri ambayo yataondoa athari zinazotokana na *cyber crime* na mambo mengine yanayotokana na utumiaji wa mitandao katika shughuli zozote zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho tumeona ni mambo mawili makubwa, *e-procurement*, kitu kikubwa ni mambo ya kuweka sahihi, na hii ni masuala ya *electronic signature*. Kwa hiyo, haya yaangaliwe kiutalaam kabla mchakato haujashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, utaratibu wa *electronic law* ambao ni muhimu uwepo kabla ya Sheria haijaanza kufanya kazi kwa sababu *e-procurement* ni *electronic law related.* Kwa hiyo, ni lazima tuwe na uhakika kwamba uwepo wa Sheria ambayo inatambua matumizi ya *electronic transactions* unaheshimiwa na unaweza ukakubalika katika Mahakama, ili jambo lolote linalotokea liweze likakingwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba nashukuru sana kupewa nafasi hii na nashukuru sana katika hilo. Naunga hoja mkono katika mabadiliko haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dokta William Mgimwa, sasa nitamwita Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa ajiandae na baadae atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Muswada uliopo mbele yetu. Nianze tu kwa kusema sipo mbali na wachangiaji waliopita na nadhani nitakalozungumza itakuwa ni kama kurudia, lakini ni kuonyesha msisitizo kwamba Muswada huu ni muhimu kwa Taifa letu, kwa hiyo, tunapoujadili hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge wote tuangalie hasa maslahi ya nchi na wananchi ambao wametuweka kuwawakilisha hapa Bungeni kama ndio njia mojawapo ya kusema mawazo yao huko walipo sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na mengi ya kuzungumza, lakini nitakwenda katika kifungu cha 66(1) na (2) kinachohusu manunuzi ya mashine zilizotumika kwa mfano ndege, meli, reli pamoja na mabehewa yake kama walivyokwishakutangulia wenzangu. Pamoja na tafsiri nzuri na tafsiri nyingi za kuweza kutuonyesha kwamba tukubaliane na Muswada huu wa kununua vitu vilivyotumika nianze kusema moja kwa moja sikubaliani na naupinga Muswada huu mpaka pale ambapo tutakubaliana kuacha kabisa kununua vitu ambavyo vimetumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana kwamba nchi za dunia ya tatu ambazo zinapenda kuitwa nchi zinazoendelea zimekuwa na *tendency* ya kuona kwamba zenyewe zifanywe kama majalala ya kutupia teknolojia za watu ambazo zimepitwa na wakati. Kwanza tujiulize wenzetu sasa hivi wanawaza teknolojia mpya za kisasa, wanatengeneza treni wameshaanza siku nyingi, wanatengeneza treni za umeme, ndege za kisasa, meli za kisasa, sasa tufikirie kitu kimoja, wao wameona kwamba hivyo vifaa vyao sasa vimepitwa na wakati kwa kupeleka ni wapi. Sisi tunajua sio kwamba hatujui, labda kwa utendaji wetu wanawaza maslahi yao binafsi wanasahau kwamba siku moja nao watakuwa huko huko kwa wenzetu wa chini kwa kuwaza *ten percent* sijui kama wamerubuniwa labda kwa kurubuniwa kuona kwamba sasa wanafanya hisani kutuuzia vile vitu walivyovitumia vimechakaa, vimepitwa na wakati, *life span* vimekwisha sasa tunakubali viletwe kuja kutumika kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa na nguo sisi wanawake huwa tuna kawaida ukishavaa nguo imepitwa na wakati unaweza kusema ngoja sasa nimpelekee shangazi kule kijijini akavae. Unaitupa kwa sababu haina tena ule muonekano mzuri na haiendani na wakati unaipeleka, kwa sababu huwezi kuichoma moto, unafikiri uliinunua kwa shilingi ngapi uende kuichoma moto. Lakini haifai, shangazi akienda kuvaa siku mbili imeshachanika kwa sababu muda wake wa kutumika umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wabunge tusikubali Tanzania kufanywa dampo la vifaa vilivyotumika. Mifano ipo tunakumbuka *MV Kigamboni* wakati wa enzi za Mheshimiwa Mustapha Nyang'anyi ilinunuliwa ikiwa chakavu iko wapi sasa hivi? Tunakumbuka *ATC* ilinunua ndege safari yake ya kwanza kuruka kule Tanzania ndiyo iliyokuwa ya mwisho haijaruka tena. Inasemekana hata ile *MV Bukoba* ambayo ilizama ilikuwa imeshafanya kazi sehemu nyingine ikatumika ikiwa imeshatumika huko imeshamaliza muda imeletwa na kitu kilichotumika udhibiti wake haufai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii *MV Spice Islanders* iliyoua ndugu zetu Wazanzibar wamesema imetumika huku na huku. Imekuja imetumika sijui siku ngapi na imeua ndugu zetu, wapo hapa ni ndugu zetu. Wengine tumepoteza mashemeji, tumepoteza wajomba hata mimi ndugu zangu wamekufa huko. Tusikubali kuleta makaburi, tusikubali kufuga nyoka kwenye nyumba yetu ambayo baadae atatung'ata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji tukumbuke kwamba siku moja na sisi tutakwenda kutumia treni kwa sababu sasa hivi Waheshimiwa Wabunge tunayo tabia moja ya kusahau tulikotoka. Sisi tumepewa mikopo tumenunua magari mazuri tunasahau treni, hatupandi treni. Kwa hiyo, hata ikiwa imechakaa hatukumbuki, lakini tuna watoto wetu wanakwenda shuleni, tuna ndugu zetu kwa nini tusiwe na huruma na nchi hii. Tamaa ya nini? Watanzania ni wavumilivu hatujafikia mahali pa kuanza kupiga kelele tununuliwe vitu ambavyo vimechakaa. Kwa uvumilivu huo huo tunaomba ndugu zetu Waheshimiwa watendaji mtuonee huruma, mtusaidie Taifa hili lisipate kuangamiza watu kwa sababu ya makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja na nadhani Waheshimiwa Wabunge wote kwa umoja wetu tusahau itikadi, tuzungumze jambo ambalo litajenga na ambalo litarudisha heshima ya nchi yetu, nchi yetu si nchi ya kupewa *scrapers.* Sasa hivi tumesikia Wizara ya Uchukuzi ina mpango wa kupanua reli na mambo mengine, lakini ni kwa sababu kwamba Japan imeshaanza kwenye teknolojia nyingine inataka kutuletea treni zake ili tuzitumie huku. Juzi tumeshuhudia *TRL* wakinunua mabehewa yamechakaa sijui yapo wapi, *engine* za treni ziko wapi sasa hivi na zinafanya nini. Treni ipo wapi ambayo ilikuwa inafanya kazi tangu enzi za Uhuru, tangu mimi nazaliwa reli ya kati ipo, lakini walipoingia ndugu zetu mambo yamechakachwa na sasa hivi tunalia. Ndugu zetu wa Kigoma wanapiga kelele kila siku hapa ni kwa sababu ya uzembe na ni kwa sababu ya tamaa ya watu wachache sasa tunataka kukimbizwa mbio mbio hata huu Muswada tunaletewa asubuhi wanatukimbiza mbio mbio ili tukubaliane na mambo ambayo hayawezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga, kama kweli tunapenda Taifa letu kwa umoja wetu tukatae hivi vitu ambavyo tutaletewa hapa. Nisiongee sana, nakushukuru na narudia tena siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa kama alivyosema mchangiaji aliyepita nianze kusema siungi mkono hoja hasa kipengele hiki cha mali chakavu. *(Makofi)*

Ningependa nianze kwa kusema *priority* namba moja ya Serikali yoyote duniani ni ku-*preserve* maisha ya wananchi wake. Pamoja na kwamba tuna *preserve nature* lakini *priority* namba moja ni kuhakikisha uhai wa watu wetu unalindwa kwa gharama yoyote. Ndugu zangu hivi vifaa chakavu ambavyo Muswada huu umeletwa ambao imelenga kuagiza vitu chakavu kama mabehewa ya treni, ndege na meli, *majority* ya watu wengi sana wanaokaa mwambao, wenzetu wa visiwani, Kigoma, Mwanza wanatumia sana huu usafiri. Kwa hiyo, kama tusipojali sana maisha yao na kutokuthamini uhai wao tutakuwa tumepotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo tu ndio nataka nijikite, ili nieleweke vizuri naomba ninukuu maneno kadhaa hapa ya hotuba ya Pick Botha aliyoitoa mwaka 1985 ambayo wengine wameidadisi kwamba ilikuwa ni *propaganda* ya *ANC,* wengine wanasema ni Pick Botha lakini *it doesn't matter* ni kwamba haya maneno alizungumza, lakini napenda wengine wanaopenda kutoa miongozo, wahubiri huwa tunasema huwezi kujengea *doctrine* kwenye *parable* hii ni

*parable.* Lakini hoja anayotaka kuijenga hapa ni mipango mibovu ambayo tuliyonayo. Pick Botha aliwahi kusema katika hotuba hiyo ambayo kwenye *google* unaweza ukaibua ukitaka. Anasema; *"Pretoria has not made by the white mind, The Republic of South Africa that we know today has not been created by wishful thinking. We have created it all at the expense of intelligent."* Anasema; *"By now everyone of us has seen it practically that blacks cannot rule themselves. Give them guns and they kill each other. They are good in nothing else but making noise, dancing, marrying many wives and indulge sex. Let us all accept that blacks man is a symbol of poverty, mental inferiority, laziness and emotional incompetence. Every black man does not plan his life beyond a year." (Makofi)*

Leo ni miaka 50 ya Uhuru, tunataka kusherehekea miaka 50 ya Uhuru, tunakaa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikiri kununua vitu vichakavu. Nimetoa mfano huyu Kaburu alikuwa anatu-*challenge* watu weusi kwamba hatuwezi kujitawala, hatuwezi kupanga mambo yetu wenyewe anasema *average black man* ana uwezo wa kupanga mambo yake mwaka mmoja tu zaidi ya hapo hawezi. Toka tumepata Uhuru tunawaza kununua vitu vichakavu leo. Haya ni masuala ya kukaa ndugu zangu tukajifikiria tuwe tuna *plan*. Watu waliotuletea Muswada huu wamechoka kufikiri, hawataki kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili tusikubaliane kuungana na watu ambao wana-*refuse* kufikiri badala ya kupanga mipango mizuri ya kuendelea mbele tunarudi nyuma. Wenzangu wamezungumza hapa Afrika imegeuka kuwa ni dampo la takataka. Tumejaza kompyuta, mafriji, redio ambavyo ni *used*, tumejaza midoli *used*, tumepata Uhuru tunavaa nguo *used, for how long you will go with these things? (Makofi)*

Mimi kama Mhubiri kuna masomo mengine pale kanisani huwa tunasema *quick fix*. Mtu akiwa na madeni anaamua kunywa pombe ili asahau madeni lakini akiamka madeni yako pale pale. Tunajaribu kuwa na *quick fix* badala ya kukaa chini na ku-*plan* tunakwenda wapi tumetoka wapi tujifunge vibwebwe kama Taifa. Kuna msemo mmoja unasema; *"an engine in the right direction is better than a mile in the wrong one."* Tukae tujihoji tumeshindwa wapi tuanze upya kama Taifa. Mbona tulinunua ndege ya Rais japokuwa tulikuwa na mipango mibovu haitumiki. Kwa nini tusikae chini tukafikiri hata bora tukope mikopo ili tusiweke rehani maisha ya Watanzania. Ningewasihi Wabunge kwa ujumla wetu, Watanzania wanatusikiliza, Watanzania wanatuona kwa ujumla wetu sisi hapa ndio *cream* ya Taifa tukae kwa pamoja tujadili vitu vya maana vyenye manufaa kwa Taifa letu, tusianze kuwaza vitu vya mitumba. Teknolojia imebadilika tunao watu wengi katika nchi hii ambao yawezekana hawako katika *system* ambayo sisi tumebahatika kuwepo. Hebu tujaribu kuwaingiza watoe mawazo yao, tunaweza kufikiri tukaweka mipango mizuri ambayo italitoa Taifa letu hapa tulipo. Tuache itikadi za vyama, tufanye mambo ya msingi ambayo Watanzania wametuamini. Leo tunawaza kununua vitu chakavu, halafu tunasema tumethubutu, tumeweza, tumesonga mbele. Tunathubutu kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunathubutu kitu gani badala ya kuwaza na kufanya mipango ya kununua vitu vikubwa na hii yote ni *poverty mentality*. Kwa sababu tunafikiri kwamba sisi ni watu wa kupewa vitu vya chini chini. Tutafute watu wenye *brain* kubwa, watu wanaoweza kufikiri tuwe na mipango endelevu kwa ujumla wetu tuwe na mipango mikubwa, tusifikiri hivi kidogo, hivi vitu vimetu-*cost.* Halafu kwa bahati mbaya mimi katika Kamati yangu tumezunguka sana kwenye maeneo ya madini, tumeenda sehemu mbalimbali. Ukienda kwa mfano Mgodi wa Bulyanhulu pale au ukienda Nyamongo au Buzwagi unapoingia tu kwenye mgodi unapokaribishwa na wale wageni ambao wanasema mipango yao hawajafanya kwa kubahatisha *they used their mind,* wame-*plan* mambo yao utakapoingia utakuta wameweka vizuri *power point* vizuri, *speaker* zinafanya kazi vizuri, *toilet* ziko nzuri, mkitoka mambo safi, unapotoka tu unaingia kwenye Ofisi ya Serikali tulienda kwenye Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hata maji kwenye choo kwenye mradi mkubwa ule hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *cement* kiwango kilichopangwa hamna, hayo ndio yanayotusumbua sio *bills* zinazokuja za ajabu ajabu watu wanataka kufanya *deal* hapa. Unapotoka pale kuna *white mind* unaona vitu viko *well organized*, unapohama tu unaingia katika Ofisi ya Serikali bahati mbaya sijaenda Ikulu, lakini mahali ambapo kuna utaratibu mzuri afadhali hapa hapa Bungeni naona vitu vinaenda vizuri. Lakini unapotoka kwenye Ofisi za Serikali kitasa

hakifungi mlango, choo tenki limekaa hivi, vitu vya ajabu kabisa wakati watu wamesoma miaka 50 ya Uhuru *I don't understand* tunasherehekea kitu gani, halafu tunakaa hapa tunapiga makofi hatutaki kuwajibika kama Wabunge kuishauri Serikali kwamba wananchi wa Tanzania wametuamini, wametupa dhamana ni lazima tufikirie afya zao. Ni lazima tu-*preserve* uhai *at any cost. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba huu Muswada kipengele hiki kitupiliwe mbali tuwe na mawazo ya kununua vitu vipya. Uwezo huo tunao, kilichokosekana hatuna *leadership*, hatuna *inspirational leaders* ambao wanaweza waka-*inspire* watu, wanaoweza waka-*motivate* Watanzania tukashikamana kwa pamoja hata kwa kuchangishana tukanunua vitu vipya. Tuna *vacuum* ya ile *schedule* na ndio maana tunakuja na Miswada hii ambayo haina kichwa wala miguu ya kuweka rehani roho za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niombe kama ndugu yangu aliyeomba asubuhi kwamba Watanzania wanatutazama, wametuamini, wanatupenda na kwa muda mrefu wamekuwa wavumilivu, wameisikiliza kweli kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini inafika mahali hawana imani. Ninyi wenzetu mmepewa dhamana ni Serikali yenu, *we need your brain to be involved* mnapoleta Miswada yenu hapa. Huu Muswada umerudishwa mara nyingi unatupwa unarudi, unakwenda unarudi, hatutaki vitu chakavu tunataka vitu vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimesema sana kipengele changu niwasihi chonde chonde Mheshimiwa Mkulo, tunaomba kipengele hiki kiondoke tuungane mkono dhana ya kufikiri kwamba hatuna pesa hiyo ni *poverty mentality* na tunatakiwa tuikatae. Sisi Watanzania sio maskini ila tuna ufahamu wa kimaskini. Tunacho kila kitu katika nchi hii tunahitaji tu-*involve brain* kubwa ya Watanzania ambao Mungu ametubariki tuweze kusonga mbele kwa pamoja tuachane na mawazo ya vitu vidogo vidogo, tuachane na kula *worms. (Makofi)*

Mheshimiwa fulani alisema tuko kwenye chupa hebu tutoke kwenye chupa tuwe na mawazo mapana ya pamoja tuweze kushirikiana, tuwalinde, tuwatunze wananchi wa Tanzania ambao wametupa dhamana ya kuwasemea. Tumekuja hapa kuwasemea, tuache itikadi zetu za kivyama tuangalie maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hotuba nikiwa na Wazungu huwa nagombana nao sana, lakini nikikaa na weusi hebu sema tulitafakari namna gani tunapangilia mambo yetu. Tukitembezana Wabunge wote hebu tuangalie *diary* zetu, ukimwona Mbunge *diary* yake imejaa miaka miwili ni mgogoro au miezi mitatu. Ukimwona Mtanzania *diary* imejaa labda Hakimu amejaza kesi, kwa sababu hatuwezi kupanga. Ziara za Mawaziri na zenyewe za kubahatisha hivyo hivyo, inawezekana mpaka za Rais hazijapangwa. Huyu Kaburu anayesema; *"An average black man does not plan his life beyond a year."* Sasa tupo weusi watupu hapa hebu tutafakari *can we plan, are we able to plan,* leo tuna *plan* kununua vitu chakavu, yaani mmekaa tunashauriana kweli tunapanga mambo ya msingi ya kuendeleza Taifa letu. Ninawaomba ndugu zangu kipengele hiki kwa ujumla wetu tukikatae na tunapokikataa ni kwa faida ya Tanzania na Taifa letu. Tuwa-*challenge* wale wanaoleta Miswada hii walete Miswada yenye mshiko, Miswada yenye faida kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba nikushukuru na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako ingawa wakati mwingine ili mchango uwe mzuri sana unakuwa *specific* unakuwa *forecast* unasema kuna kitu fulani na kitu fulani. Sasa ukisema tu chakavu, chakavu kama vile vyote, haya lakini ndio siasa ya vyama vingi. Tunaendelea sasa nitamwita Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** *Bismillah, Rahman Rahim,* Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nakushukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mwenyezi Mungu vilevile kwa kunipa uhai na nguvu ya kuwepo hapa. Kwanza kabla sijaanza mchango wangu naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Tumethubutu, tumeweza na tutaendelea kuweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *PPRA* ni wajibu wa kikanuni ku-*declare interest* katika maneno yangu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Bodi, Mtendaji Mkuu na watendaji wake wote na wajumbe wote wa Bodi kwa kazi nzuri ya uadilifu, ya umakini, ya uhakika ndiyo eneo ambalo naweza kusema ndani ya nafsi yangu ni eneo ambalo sijalisikia linanuka rushwa hata siku moja ni Kitengo hiki cha *PPRA.* Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii inafanya kazi kubwa sana kuokoa na kudhibiti manunuzi yasiyokuwa na tija. Tatizo kubwa tunapoipa nguvu *PPRA* hatutaipa uwezo kama hatuipangii Bajeti inayostahili kufanya kazi zake za ukaguzi kama inavyostahili kwa mujibu wa Sheria hii kama itapitishwa kesho na kwa majukumu ambayo wanataka kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii bila kupewa Bajeti inayostahili kupewa haitaweza kuajiri wafanyakazi wanaotakiwa kuajiriwa kusimamia Sheria hii, haitaweza kukarabati au kumalizia jengo lake ambalo taasisi hii inahifadhi taarifa na *documents very very sensitive,* Taasisi hii haitaweza kufungua ofisi zake za kanda kama haitaweza kupewa Bajeti inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu kipya kwenye Sheria hii ya leo ya kuifanya *PPRA* iweze kuitisha *tender* ambayo inalalamikiwa, kuitisha *tender* hizi zinagharama. Mahitaji ya *PPRA* ni wafanyakazi 142, lakini leo wafanyakazi waliopo ni 51 tu. Kuna upungufu zaidi ya wafanyakazi 90. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri upo hapa na wewe ndiyo taasisi yako, ujaribu kutazama ni namna gani ya kuiwezesha taasisi hii ili iweze kutimiza majukumu yake. Tumeona *CAG* anavyopewa pesa, taasisi hii huwa inagundua mapungufu kabla hata *CAG* hayajayaona. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri ulitizame suala hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zinazokaguliwa na *PPRA* ni 390, lakini taasisi zilizokaguliwa ni 330 tu kwa miaka minne, kwa maana taasisi hizi zinatakiwa zikaguliwe kila muda ili sasa *PPRA* iweze kujua ni nani ambaye anayechafua au ambaye anafanya kazi bila kufuata taratibu za kisheria. Taasisi hii iliomba ipewe shilingi bilioni 10 ili iweze kufanya kazi zake, pesa ilizopewa ni bilioni mbili na milioni mia moja. Tunaipa majukumu ya kuangalia matumizi au manunuzi ya Serikali ya zaidi ya shilingi trilioni tano kwa bilioni mbili na milioni mia moja. Hawataweza kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu. Kwenye ukaguzi wa mwaka jana taasisi zilizokaguliwa kukiuka taratibu za manunuzi taasisi 204 karibu zote zimekutwa zina upungufu. Sasa leo tunapitisha Sheria na meno mapya watafanyaje kazi yao kama hawawezeshwi katika rasilimali fedha na kwa mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri alione na aweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema ripoti ya *PPRA* iletwe Bungeni, inapoletwa Bungeni haijadiliwi na Kamati yoyote ya Bunge. Kwa hiyo, haya ni mapungufu ya Kanuni za Bunge kutokujadili ripoti ya *PPRA* ambayo ina umuhimu kama ripoti ya *CAG* na ripoti zingine zinazokaguliwa na Kamati za *POAC* na *LAAC* ambazo ni Kamati za Bunge. Taasisi hii inafanya kazi kubwa sana ya kuokoa mali za umma na hivi karibuni itaonyesha baadhi ya taaisi zinazojiingiza katika *tender* ambazo hazina tija katika taasisi zao *simply* kwa sababu ya fikra potofu ya kujiingizia pesa nje ya utaratibu unaotakiwa na hivi karibuni tutakuwa na *shame list* za Halmashauri zote zilizofanya vibaya, taasisi zote zilizofanya vibaya na kuwaweka hadharani viongozi wa taasisi ambazo zinahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya mimi kwa vile ni Mjumbe sitataka kuingia mjadala huu wa mali chakavu au mali safi lakini kuwe na busara katika kutatua tatizo hili, tutizame *the way forward.* Unaponunua ambacho kimetumika na kimefanyiwa *due diligence* ya uhakika. Tatizo wanaloliona Wabunge humu ndani kuwa inawezekana watu wakatumia mwanya huu kununua vitu vibovu katika nchi yetu, hilo halitakubalika na hakuna mtu yeyote atakayelikubali. *(Makofi)*

Lakini kukiwa na umakini wa kutizama mitambo iliyotumika miaka mitano iliyopita, sisi hatuhitaji teknolojia ya kuendesha treni kilomita 300 kwa saa. Tunahitaji watu wetu wafike Kigoma, waende salama na warudi salama. Kwa hiyo, busara zitumike kutizama ni maeneo gani ambayo Bunge na Serikali zinaweza kufikia muafaka wa kupata njia ya kupenyea ili sasa tusijikute tunaingia kwenye giza kama tulivyoingia hivi karibuni. Inawezekana kuna baadhi ya watu wanafikiri kwamba

kununua mali chakavu labda kuna kamisheni. Kuna wafanyakazi wengine wako *very honest*, kuna taasisi za Serikali watu wanafanya kazi kwa uadilifu na wanapoona kuna tatizo kwa sababu kwenye giza uchumi wa nchi utalala. Hatuwezi kununua mtambo mpya kwa sababu mtambo mpya unaweza ukahitaji miaka miwili. Lakini kama nilivyosema kama tulikuwa tuna mipango mibovu haya ndiyo yatatukuta njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka kutoa ushauri, lazima tuwe na *plan* na tu-*plan* vizuri sana, mimi pale Ilala sina suala la stakabadhi ghalani. Sisi tuna vijana pale kazi zao zinahitaji umeme, tuna *welders*, tuna vinyozi, tuna mama lishe ambao wanahitaji umeme na kama kuna njia ya kupata umeme basi Serikali itafakari itumie busara isinunue mitambo itakuja kuiabisha Serikali. Lakini mitambo ambayo imetumika na ambayo inaweza kufaa. Kama hii ya *Dowans,* hii mitambo imeletwa nchini si mitambo mipya. Tumelumbana humu ndani, tumeitia nchi kwenye giza miezi sita watu wamekosa ajira, vinyozi mjini hawana kazi, *welders* hawana kazi. Wengine wanafikiri umeme labda ni *air condition* au *TV* au wengine ambao wana uwezo wa kununua majenereta, si kila mtu ana uwezo wa kuwa na jenereta. Kuna watu wengi sana maskini wanateseka kwa sababu ya tatizo la umeme. Tuwe na mipango sahihi, tuwe na mipango ya kuhakikisha kuwa tunakwenda mbele *and if we want a future, we should brake with the past. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe mmoja wa wachangiaji katika mjadala huu ambao ni muhimu sana na nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Sheria hii ya manunuzi na kama walivyotangulia wenzangu kusema kwamba manunuzi katika nchi hii yanatumia karibu asilimia 80 ya Bajeti nzima ambayo imetengwa kila mwaka. Kwa hiyo, inadhihirisha kabisa ni kwa namna gani Sheria hii ilikuwa ni muhimu ili tuweze kudhibiti mianya yote ambayo inafanya zile asilimia 80 zisitumike vizuri. Kwa hiyo, naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona mimi tatizo si Sheria hii. Sheria imetengenezwa vizuri. Sheria imezingatia vitu vingi ambavyo vimewekwa vizuri. Tatizo ni namna gani ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii, hapa ndipo penye hoja na nitatoa mfano. Halmashauri ndiyo zinazopewa fedha nyingi sana kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo. Lakini Halmashauri zetu zimejikuta zikipata matatizo kwa sababu ya fedha hizi za maendeleo zinapofika kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, Halmashauri inatangaza *tender*, inapata wazabuni, kwa gharama za vifaa vya ujenzi vya wakati ule inapotangazwa. Lakini fedha zinakuja kuingia baadae baada ya miezi sita au wakati mwingine zinachelewa mwaka mzima. Kwa hiyo, fedha zinapokuja tayari gharama za ujenzi zimeshabadilika. Wote ni mashahidi saruji inapanda kila siku, bati zinapanda kila siku, kwa hiyo, mkandarasi ame-*tender* kazi kwa kiasi kadhaa cha fedha kwa bei kadhaa ya saruji au bati lakini anapokuja kupata zile fedha tayari bei zile zimebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ndipo panaanza kupotea ubora wa kazi inayofanywa na yule mkandarasi. Kwa hiyo, changamoto kubwa ya Serikali hapa ili kuifanya Sheria hii iweze kufanya kazi vizuri ni kuhakikisha inapeleka fedha kwenye Halmashauri kwa wakati muafaka na haraka iwezekanavyo ili ziweze kufanya kazi zinazotakiwa kwa kipindi kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shughuli za barabara ambazo hazilingani kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri hasa ukizingatia hali ya hewa. Tunazo Wilaya kama za Makete ambazo mvua inanyesha miezi nane mfululizo, kwa hiyo inabakiwa na miezi minne ya kazi ndiyo ambayo unaweza ukajenga barabara. Lakini katika miezi hiyo minne fedha hazijaja bado na kandarasi zimeshatangazwa na watu wamesha-*tender,* wameshapewa kazi fedha hazijafika bado. Fedha zitakapofika ni wakati ambao mvua zinanyesha, kwa hiyo, mkandarasi yule atajenga barabara kwa kiwango cha chini kwa sababu anajenga wakati wa mvua na kama tutaamua kwenye Halmashauri kwamba basi asuburi kwenye ile miezi minne zinakuja hoja za wakaguzi kwamba kwa nini fedha zimekaa muda wote huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ili kuwezesha Sheria hii ifanye kazi zake vizuri la kwanza iharakishe fedha kufika kwenye Halmashauri ili iweze kuendana na bei ambazo zimepangwa za wakati ule za bidhaa zilizopo. Lakini la pili itofautishe mazingira ya Halmashauri na Halmashauri na pale inapoonekana Halmashauri kwamba muda wake wa kufanya kazi ni mdogo basi wapewe kipaumbele cha kuharakishiwa fedha ili waweze kujenga hizo barabara kwa wakati ambao inawezekana, si wakati wa mvua. Hiyo ni hoja yangu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo bado nayo ni changamoto kwenye utekelezaji wa Sheria hii ni namna gani *PPRA* wamejipanga na ni namna gani *PPRA* wamewezeshwa. Kwa sababu tunafahamu kwamba *PPRA* makao yake makuu yapo Dar es Salaam, hakuna matawi kwenye Halmashauri, tuaambiwa kwamba yapo kwenye Kanda lakini manunuzi makubwa yanafanywa kwenye Halmashauri na hawa *PPRA* hawapo kule. Kwa hiyo, kama yanatokea makosa yote inakuwa ni vigumu sana kuyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba hawa *PPRA* ndiyo wanaweza wakigundua kwamba manunuzi yamekiukwa wanaweza wakasitisha ile *tender* isifanyike. Sasa watagundua saa ngapi kama wao wapo Dar es Salaam na manunuzi yamefanyika kule Makete au mahala pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninashauri kwamba katika changamoto hii ya pili, tuhakikishe wenzetu wa *PPRA* wanajengewa uwezo ili waweze kusambaa na kuwa na mtandao kama wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(PCCB)* ambayo wapo kila Wilaya na inakuwa rahisi kufuatilia mambo yote ambayo yanakuwa yamekiuka Sheria na pengine ningependekeza kwamba kwa kuwa fedha nyingi sana zinatoka kwenye Halmashauri. Serikali inaonaje kwamba kwa kuwa sasa hivi haina mtandao wa *PPRA* kwenye Halmashauri watumie mtandao wa *PCCB* kwa kuanzisha kitengo cha manunuzi ya umma ili hao sasa ndiyo wawe karibu na Halmashauri kufuatilia manunuzi yanayofanyika na baadae kama itaonekana kwamba tayari *PPRA* wameshajengewa uwezo wa kutosha *then* wanaweza wakaondoa kile kitengo cha *PPCB* wakawa na vitengo vyao katika Halmashauri. Hii itasaidia kudhibiti manunuzi ambayo si mazuri kwenye Halmashauri. Hayo ni mapendekezo, tutumie mtandao wa *PCCB* ambao pia umeimarika katika kila Wilaya tuweke kitengo cha manunuzi ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu nimefarijika sana na hatua ya Serikali ya kuona kwamba upo umuhimu sasa wa Madiwani kushirikishwa kwenye azma nzima ya kuona mikataba inayoingiwa na Halmashauri yake kuhusu manunuzi au *tender* mbalimbali. Kwa kupitia kwenye Kamati ya Fedha.

Mimi hili naliunga mkono vizuri sana kwa sababu mara nyingi tutapata nafasi ya kuangalia zile *BoQ* zikoje na tutaona nani amepewa na kama kuna upendeleo itakuwa rahisi kusema pale moja kwa moja kama kuna makosa na kumshauri Mwenyekiti wetu kwamba hii haitakiwi isainiwe na hii inatakiwa isainiwe. Mimi nadhani hili ni la kuungwa mkono vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hili ambalo limeongelewa na Wabunge. Mimi nataka Waheshimiwa Wabunge tuitendee haki Serikali yetu. Kwa nini nasema vile? Sheria hii kilichoandikwa humu ndani hakijaandikwa ununuzi wa vitu chakavu. Humu imeandikwa ununuzi wa vitu vilivyotumika na imetaja hivyo vitu kwamba ni ndege, mashine za reli na hizi meli, vitu vilivyotumika.

Ndugu zangu kitu kilichotumika, ukishalinunua gari toka viwandani ukiendasha kilomita kumi tayari ni *used car*, utakapokwenda kuuza hutaliuza kama gari jipya. Kwa hiyo, unaweza ukanunua ndege ambayo imetembea kilomita 8,000 tu; ile tayari ni *used* lakini inafanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sisi wote ni mashahidi hapa. Suala la kununua kitu ambacho ni *used* ni uwezo wako ulionao. Hununui kitu kilichotumika kwa kupenda, ni kutokana na uwezo ulionao wewe. Ndiyo maana sisi hapa tulipopewa fedha za magari wengi tumeshindwa kununua magari mapya, tumenunua yaliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa gari lililotumika haliui mtu kama ndege inaua mtu. Mimi nadhani twende na ukweli kuitendea haki Serikali yetu kwamba imesema inataka kununua vitu vilivyotumika. Kinachotakiwa hapa ni kuangalia uhalali kwamba kimetumika kiasi gani na je, bado kinafanya kazi au vipi.

Lakini vilevile tuangalie sababu zinazotupelekea kwa nini tununue kile kitu na ndiyo maana waka-*specify* wakaweka vitu vitatu kwamba tutanunua vitu hivi kwa sababu moja, mbili tatu. Kwa hiyo, nataka niwaombe *issue* iwe kukubaliana kwamba kama leo sisi tunaamua hatukubaliani kununua vitu vilivyotumika tukubaliane hivyo. Lakini tusiseme kwamba Serikali imesema inataka kununua vitu chakavu. Hii si sahihi, hatuitendei haki Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nataka nitoe angalizo kwa wenzangu, unapomkosoa mwenzako hebu jikosoe wewe kwanza. Kwa sababu hapa tunavaa kiatu cha mtumba, suruali mtumba, koti mtumba. Hebu tujirekebishe sisi kwanza ndiyo twende huko. Kwa hiyo, mimi nashauri sisemi kwamba Wabunge waunge mkono au wasiunge nataka tuitendee haki Serikali kwamba yenyewe inasema tununue vitu vilivyotumika sio kwamba ni chakavu vya kutupa hapana. Kwa hiyo huo ndiyo mchango wangu kwamba tutaamua lakini hoja inabaki pale pale kwamba ni kwa nini tunafikia uamuzi wa kununua kitu kilichotumika. *That is what should be main important point*. Lakini vinginevyo tutakuwa hatuitendei haki Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimeangalia Muswada huu kwamba kutakuwa na kitengo kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi, kitengo ambacho kitakuwa ni cha mambo ya *policy,* naunga mkono. Lakini vilevile napenda sana waangalie hizi sifa za yule *Chief Executive* atakayekuwa anasimamia kile kitengo kwamba awe na miaka kumi. Mimi naamini kwamba sasa hivi tunao vijana wenye uwezo ambao watakuwa wamefanya miaka mitano, mikaka mitatu ame-*prove* kazi nzuri nao wafikiriwe.

Kwa hiyo, yule anayefanya maamuzi ya kuteua *Chief Executive* wa *PPRA* na *Executive* wa *Policy Department* aangalie kwa upana zaidi kwamba wapo vijana ambao wanafanya kazi zao vizuri ili waweze nao kufikiriwa na si miaka kumi tu ndiyo weweze kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kuunga hoja mkono na nawashukuru sana wenzangu waliotangulia kuchangia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia maeneo machache kwenye Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niipongeze sana Kamati ya Fedha na Uchumi kwa jitihada kubwa sana ambazo imefanya katika kuuboresha Muswada huu na kuja kwenye sura ambayo umekuja leo. Napenda niwapongeze sana, najua Muswada huu umekataliwa karibu mara mbili kwenye ngazi ya Kamati na hii inaonekana wenzetu walifanya kazi kubwa kwa niaba ya Wabunge na Bunge na ndiyo sababu nachukua nafasi hii kuipongeza sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie, kwanza nianze na ukurasa wa sita kwenye Muswada hapa na naanza na sehemu ile ya *application*. Nimeshindwa kuelewa kwa nini kwenye eneo la *application*, ukienda *subsection (2)* mpaka (*4)*, zinazungumzia kwamba Jeshi na lenyewe manunuzi yake yatazingatia sheria hii. Sasa ambacho kimenishangaza hapa, ni kwa nini eneo hili liko kwenye eneo la *application* na kwa nini haliko ndani ya Muswada wenyewe kwenye kipengele maalum! Najua kwenye Sheria ya Mwaka 2004 hakipo hapa. Sasa kama tumeamua kuingiza kwamba na Jeshi lazima taratibu zake za manunuzi ziwe *governed* na sheria, basi naomba sehemu hii iondolewe, iwekwe ndani ya Muswada, siyo sehemu ya *application*. Sasa, kama Waziri ana sababu za msingi za kwa nini ameiweka hapo, basi atalieleza Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende *subsection* (9) kwenye Muswada na huu ni ukurasa wa 20. Ukienda ukurasa wa 20, kuna kipengele (i) ambacho kina vipengele vitatu, (i) – (iii) ambavyo kwa ruhusa yako Mwenyekiti, naomba nivirejee. Pale ukurasa wa 20 inasomeka:-

(i) *"Procurement audits during the tender preparatory process;"*

(ii) *Contract audits in the course of execution of an awarded tender; and*

(iii) *Performance audit after the completion of the contract in respect of any procurement as may be required.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo ni muhimu sana ambalo *PPRA* inalifanyia kazi na Kamati za Bunge zile zinazosimamia masuala ya Fedha, zinafanya kazi inayofanana na hiyo. Lakini, wenzetu *PPRA* wana utalaam mkubwa zaidi pengine kuliko *Oversight Committees* za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, iwe ni lazima kwa *PPRA* baada ya kufanya kazi zote hizi tatu ambazo zinafika mpaka mwisho, kuona namna ambavyo taratibu hizi za *tender* zimekwenda, maana wanakwenda mpaka kwenye *performance audit*, basi Bunge na *Oversight Committees* zipewe taarifa hizo ili ziweze kusaidia, kwa maana kwamba, zile *Oversight Committees* na zenyewe ziweze kusimamia na kushauri Serikali vizuri kwenye eneo linalohusiana na manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende ukurasa wa 35 kwenye Muswada. Ukurasa wa 35 na kwa taarifa ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri hapa asubuhi, inasema kwamba, tutaweka kanuni kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 ambazo zitawezesha Waheshimiwa Madiwani na hasa Kamati ya Fedha na Uchumi kuweza kusimamia suala zima la zabuni katika Halmashauri. Lakini kwa maana ya kwamba Mwenyekiti asiwe na madaraka peke yake ya kusaini mikataba hiyo. Baada ya mikataba kukamilika, iende kwenye Kamati hiyo, Kamati yote ijiridhishe na baadaye ndiyo Mwenyekiti asaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo wenzangu wengi wamezungumza, ushauri wangu katika eneo hilo ni kwamba mikataba hii mingi pamoja na *BoQs* zote zinakuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Sasa, tunajua Katiba yetu inaturuhusu wote tunaojua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza kuomba Udiwani. Sasa, siyo lazima nijue lugha zote mbili na kama najua Kiswahili, lakini unaniletea mikataba ambayo imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, maana yake unasema niweze kumshauri pia Mwenyekiti asaini kitu ambacho na mimi sina uhakika nacho sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nishauri, mikataba na *BoQs* zote zitakazosainiwa katika ngazi za Halmashauri, ziandikwe kwa lugha ambayo Waheshimiwa Madiwani wetu wanajua. Siyo mbaya kama ikiwepo *version* ya Kiswahili na *version* ya Kiingereza, anayeweza kusoma Kiingereza asome, anayeweza kusoma Kiswahili asome, ili mradi ajiridhishe kwamba kitu tunachosaini ni sahihi. Maana tunaweza tukaacha hivi hivi, watu wakaenda pale, tumelipana pesa, tunasema Mwenyekiti, hiyo iko sahihi bwana, saini, na Mwenyekiti akaisaini. Itakuwa madhumuni ya sheria hii tunayoipitia, hayana maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo pia nataka nishauri; sheria hii tunayopitisha, inabidi Sheria ya Fedha ya mwaka 1982 pamoja na Kanuni zake itabidi zirekebishwe. Sasa, najua tunapopitisha sheria hii, bado Sheria ya mwaka 1982 ile ya Fedha ya Serikali za Mitaa, itakuwa haijafanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, katika eneo hili nataka nishauri pia Serikali ilete Sheria ya Fedha ya mwaka 1982 na yenyewe iweze kubadilishwa. Wakati Waziri anaandaa Kanuni kwa ajili ya Sheria hii, basi na Sheria ya Fedha ya mwaka 1982 pamoja na Kanuni zake ziweze kubadilishwa ili sheria hii inapoanza, basi na Waheshimiwa Madiwani kule wawe na nguvu pia ya kuweza kusimamia hiyo mikataba vizuri. Vinginevyo, tunaweza tukapitisha leo, Waziri akatunga Kanuni, Sheria ya Fedha ya mwaka 1982 haijapitiwa na Kanuni zake hazijatungwa, Madiwani wale watakuwa bado hawawezi kusimamia mikataba, maana inaweza ikachukua muda mrefu sana. Hilo ni eneo muhimu ambalo nafikiri Serikali inapaswa kulifanyia kazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilisisitize ni *section 50* kwenye Muswada ambayo iko ukurasa wa 47. Ninachotaka kusisitiza hapa ni suala la *procurement of common used items and services*. Nilikuwa nazungumza na watalaam wa masuala ya *procurement*, nikasema, nilivyokuwa naliona kwamba kama tukiiachia *GPSA* ndiyo iamue kwa nchi nzima kwa ajili ya bidhaa ambazo zinatumika sana, itakuwa kama taasisi moja inahodhi

madaraka kwa nchi nzima. Lakini, kwa taarifa nilizozipata, kama ndiyo hivyo inavyofanyika kwamba *GPSA* kama bidhaa hizo zitanunuliwa Mbeya, basi watakwenda kule Mbeya na watambue baadhi ya maduka au taasisi zinazotoa huduma, basi taasisi zilizoko Mbeya zichukue huduma zile kule kule. Kama hilo litafanyika hivyo, itakuwa sahihi. Lakini, kama *GPSA* ndiyo itakayoingia kwenye mkataba na wazabuni, mathalan kutoka Dar es salaam uwaambie wapeleke bidhaa huko Mikoani, hiyo inaweza isiwe na tija sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *clause 66* ambayo imezungumzwa na Wabunge wengi sana. Nadhani Serikali ingekuwa wazi zaidi. Maana tunapozungumzia suala la kununua vifaa ambavyo vilishatumika, lazima tuseme kwamba tunataka tuvinunue kwa madhumuni gani. Maana ninavyojua, Serikali kimsingi haifanyi biashara. Tunasisitiza kwamba tunataka tununue vichwa vya treni, tunataka tununue ndege, tununue na meli. Nikawa najiuliza, hivi Serikali inafanya biashara ya meli? Maana kama tunataka meli hizi zinunuliwe kwa ajili ya matumizi ya Jeshi, ni vizuri tuseme, maana Jeshi ni la kwetu na tunahitaji tuwe na ulinzi wa uhakika. Maana tukificha sana, ndiyo sababu Wabunge wengi wanaweza wakawa hawaelewi hapa. Maana kama ni suala la kununua mathalan vifaru kwa ajili ya Jeshi, ni jambo ambalo linaweza likaeleweka. Lakini, kama tunataka tununue meli kwa ajili ya abiria kama wenzangu walivyosema, ambazo zimetumika, hili nadhani haliwezi kukubalika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaja na maelezo mazuri. Mimi katika eneo hili sisemi naliunga mkono mpaka Waziri atakapokuja na maelezo mazuri ya kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge kwa nini eneo hili lipite. Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Dokta Mgimwa, ametoa tafsiri ya vifaa chakavu na vifaa ambavyo vimetumika. Lakini kimsingi ukitaka kuangalia, vifaa ambavyo vimetumika na vifaa chakavu, kimsingi bado vyote vinaweza kuwa na athari ile ile, ndiyo sababu nasema Mheshimiwa Waziri ni vizuri akaja na maelezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mwisho na hili liko ukurasa wa 82. Ukurasa wa 82 naona kifungu cha 101 kama vile kinajikanganya kidogo. Naomba kwa ruhusa yako nikisome kabla kengele haijapigwa. Kinasema:-

*(1) "A tenderer or procuring entity aggrieved by the decision by the Appeals Authority may, within fourteen days of the date of delivery of such decision, apply to the High Court for judicial review."*

*(2) "Where the application is before the High Court for judicial review, the Appeals Authority may be represented by an advocate."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili eneo, *assuming* kwamba hii *procuring entity* unayoisema ni Taasisi ya Serikali. Taasisi ya Serikali imekuwa *aggrieved* na uamuzi wa *Appeals Authority* ambayo pia ni Taasisi ya Serikali. Sasa taasisi moja ya Serikali ambayo imekuwa *aggrieved* inakwenda Mahakamani *for judicial review*. Naona kama Serikali itakuwa inataka kujichanganya yenyewe, kujipeleka yenyewe kwa ajili ya *judicial review*. Nataka nipendekeze na kama nikiona inafaa pia naweza nikaleta *amendments*, kwamba kama kuna chombo ambacho kimekuwa *aggrieved* na hakijaridhika na uamuzi wa *Appeals Authority*, ni vizuri kikaenda kwa *AG* moja kwa moja, maana huyu ndiye Mshauri Mkuu wa Sheria wa Serikali kuliko kwenda kwenye *judicial review* ambayo nadhani ni Mahakamani. Naomba na eneo hilo Mheshimiwa Waziri aje na maelezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niseme mambo mawili kwa haraka haraka. La kwanza, katika hayo ya haraka haraka ni matumizi ya *force account* kwenye maeneo ambayo hayana matumizi makubwa ya fedha ili kuwa na matumizi mazuri ya fedha za Serikali. Kuna miradi midogo midogo ambayo inahitaji milioni 10, milioni 20, bado tunafanya kwa *tenderers* ambapo ukiangalia gharama zake ni kubwa kuliko kama tukitumia *force account*, na miradi hii mingi tunaiona kwenye Mamlaka za Halmashauri za Miji au Wilaya. Naomba Mheshimiwa Waziri alisisitize hili kwenye Kanuni ili kazi ambazo zinaweza zikafanywa kwa kutumia utaratibu wa *force account*, basi ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba pia kuwe na utaratibu maalum ambao utahakikisha kwamba bei ambazo zinatumika ndizo zinazotumika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja, ila kasoro kifungu cha 66 mpaka maelezo ya Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ameniwezesha leo hii tukiwa katika mjadala wa Muswada huu kupata fursa japo ya kuchangia kwa uchache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza machache. Nadhani wenzangu wamezungumza vya kutosha katika Muswada huu. Kwanza, ukiangalia Muswada huu, naomba tuwaelimishe Watanzania. Muswada huu ukiupitia, unakuonesha kwamba, kuna vifungu visivyopungua 108. Katika Muswada huu kuna vifungu visivyopungua 108. Kwa hiyo, kwanza, nataka Watanzania waelewe kwamba watendaji na baadhi ya watu wamefanya kazi kubwa sana pamoja na Kamati imefanya kazi kubwa sana kukokotoa Muswada huu mpaka umefika hapa Bungeni. Maana inawezekana Watanzania wakajua huenda pengine kuna kipengele kimoja tu cha manunuzi ya vifaa chakavu basi. Kwa hiyo, hili ningependa kwanza lifahamike kwa umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ningependa kupongeza Muswada huu kwa sababu maeneo mengi yamegusa maslahi ya jinsi gani mustakabali wa nchi yetu unatakiwa kwenda. Kwanza, ukiangalia katika suala zima la manunuzi, asilimia kubwa ya pesa za Serikali zote zinakwenda katika manunuzi. Nina imani, malalamiko makubwa sana yaliyokuwa yanatokea katika Halmashauri zetu na Serikali Kuu, ni kutokana na suala zima la manunuzi ambalo lilikuwa haliendi sawa sawa. Kupitia Muswada huu, napongeza sana kipengele ambacho kinaainisha kwamba jinsi gani Madiwani watakuwa na mamlaka ya kuhakikisha kwamba yale manunuzi na wao wanaweza kuyapitia katika Kamati zao za Fedha. Hili ni jambo kubwa sana ambalo pale awali hao Madiwani walikuwa hawana fursa hiyo au uwezo wa kuhoji wala hawakujua ni sehemu gani wanaweza kupitia kuhoji. Matokeo yake Watendaji walitumia madaraka yao vibaya sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika sehemu hii napenda sana kuishukuru Serikali na Kamati ya Fedha ya Bunge kuliona hili la kwamba, lazima Madiwani washirikishwe katika eneo hili. Tunashukuru sana. Nadhani suala hili litaleta heshima, lakini siyo heshima peke yake, vile vile na kuhakikisha kwamba pesa za Serikali kila mtu anaweza kuzisimamia kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukubwa wa Muswada huu, umebebwa katika kipengele namba 66, katika ununuzi wa vifaa vilivyotumika. Nadhani hapa, kama Watanzania wote tuwe na lugha moja. Mimi kabila langu ni Mzaramo. Kuna lugha moja inasema kwamba *"zilongwa mbali, zitendwa mbali"* kwamba linalozungumzwa likawa tofauti na linalofanywa likawa tofauti. Hii ndiyo maana ya mashaka ya Wabunge wengi sana waliokuwa humu leo, kuna mashaka makubwa. Lengo kubwa ni kuiwezesha Serikali kuweza kupata mitambo mbalimbali ambayo itaweza kusaidia. Lakini, kwa bahati mbaya tuliyokuwa tunakumbwa nayo, baadhi yetu hatuna uadilifu. Hili ndilo tatizo kubwa sana ambalo linatukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Wabunge wote, hata wale waliokuwa wanapinga humu ndani, naamini Wabunge wote ukiangalia humu, kila Mbunge ana gari *used*. Jamani tuwe wakweli. Hata magari yetu tunayotembelea, tukienda kuulizana nje pale, tunaona kila mtu ana gari *used* humu. Lakini, tatizo kubwa ni nini? Tatizo kubwa ni kwamba, Je, katika Muswada huu tukiupitisha, hawa watu tunaowapa mamlaka haya, wataweza kufanya uadilifu kwa Taifa hili? Hiyo ndiyo changamoto kubwa sana tuliyonayo! Muswada huu unaweza kupita kwa nia nzuri sana kwamba tunapopata shida, mitambo chakavu iweze kununuliwa kwa ajili kulisaidia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya baadhi ya watu watatumia kipengele hicho hicho, vijana wanasema kwamba *"wataipiga vizuri Serikali"*. Maana wengine wasiokuwa waadilifu, watatumia huo mwanya muafaka kuhakikisha kwamba wanatumia vizuri pesa za

Serikali katika hali nzima ya ufisadi ambao sisi kama Wabunge hatutaridhika katika suala hilo hata siku moja. Ndiyo maana nasema katika kipengele hiki, Mheshimiwa Waziri baadaye atoe ufafanuzi wa kina kwamba, sisi Wabunge hatutoridhia hata siku moja, tunapitisha Muswada huu na sheria, baadaye watendaji wa Serikali wanakuja kuwaingiza…kwa sababu kama kile kipengele kinasema kwamba Rais a-*approve*. Nasema siyo sahihi hata kidogo. Kuna watu ambao watataka *"kumwingiza mkenge"* Mheshimiwa Rais. Kitanunuliwa kitu ambacho baada ya mwezi mmoja au miwili kitakuwa hakifanyi kazi na Rais atakuwa *answerable* katika hilo. Sisi hatutoridhika na hatutokubali hata siku moja Rais wetu kuingizwa katika mtego kama huo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba, Taifa limekuwa na watu wasiokuwa waadilifu. Hilo ndilo tatizo kubwa sana, ndiyo maana utata unapatikana hapa. Laiti kama watu wangekuwa waadilifu, tunasimama katika njia moja, nadhani hata kipengele hicho watu wote tungejadili kwa pamoja. Kwa sababu sisi wote tumenunua magari *used* humu ndani. Hata rafiki yangu Peter Msigwa inawezekana na yeye ana gari lililotumika. Huu ni ukweli kabisa usiofichika, lakini tatizo kubwa, je, watu ni waadilifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapitisha hili kwa umakini na kwa uadilifu na kwa imani ya kutosha lakini watu humu ndiyo wataanza kujenga maghorofa kwa pesa hizo za Serikali. Nchi yetu tutaiuza kwa kipengele hicho hicho na sisi wote tutaonekana kwamba hatuna maana hata kidogo na hatutakubali kama Bunge hili la Kumi, Wabunge makini waingizwe mkenge na sisi tuseme kwamba jambo hili Wabunge walilipitisha, sisi hatutaridhika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele hicho nadhani tutakuwa na mjadala mpana hapa, kama sisi Wabunge, tupo hapa kwa ajili ya kulinda maslahi ya wananchi wa Watanzania, je tumejipanga vipi katika kipengele hicho? Kwa maana kwamba kuna *commitment* gani endapo uadilifu utakuwa umevunjwa? Watu watawajibika vipi hata ikiwezekana tutumie sheria za China. Hili ni jambo ambalo liko wazi, kila mtu hapa anakemea katika kipengele hiki kwa sababu anaguswa kwa kuangalia maslahi ya nchi hii kwa kuwa wananchi wote wametuamini sisi ndiyo tunaweza kuwalinda, ikiwezekana na mimi kesho nitaleta *Amendment* katika sehemu ya kusema Rais ahusike pale, mimi nasema Rais asihusike pale kwa sababu kuna watu wana ajenda ndani ya *briefcase,* ambazo ajenda hizo wanataka kumuingiza Rais, kum-*implicate* katika matumizi mabaya ya pesa za Serikali, hilo halitawezekana hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki kilikuwa na nia nzuri sana, lakini katika utekelezaji wake ndiyo kuna tatizo. Hili ni lazima tuelezane wazi na tuambiane kwamba madaraka ni dhamana na madaraka ni kuulizwa katika hili. Hapa tunapitisha kwa sherehe kubwa zaidi au tunajadili, lakini kila kitu kina maana yake mbele ya safari. Kama tutakuwa na nia nzuri wote kama Wabunge na watendaji wote, kipengele hiki kisingekuwa na mashaka, lakini tatizo kubwa ni kwamba, ukigongwa na nyoka basi hata ujani ukikugusa ni lazima unastuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, simlaumu mtu yeyote anayekataa kipengele hiki na simlaumu Waziri aliyeleta eneo hilo ni kwamba ameleta kwa ajili ya maslahi ya nchi, lakini na sisi tunaliangalia kwa upana zaidi ni jinsi gani tunakwenda sambamba, matatizo yetu tuliyoyapata ni sehemu ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ukiangalia kwa undani zaidi tutafanyaje kujikwamua hapa tulipo, kwamba ni lazima watendaji wetu tuwe na *commitment* ya mipango thabiti, ni wapi tunakwenda katika Taifa hili. Hili ni jambo la msingi kweli kweli, ni lazima tulifanye kwa pamoja kwamba watendaji je, watatupeleka maeneo sahihi? Hili ndilo tatizo letu kubwa ambalo linatukabili mpaka mjadala huu unakuwa mzito kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nongwa na Waziri, nina imani katika hoja hii uliyoleta ni hoja muafaka kwa ajili ya kulikomboa Taifa letu pale tunapopata matatizo kwa mfano, tulipokuwa tunakabiliwa na tatizo la umeme tungekuwa na kipengele cha kuweza kununua mitambo ambayo imetumika maana yake tungeweza kupata mitambo, tatizo je, hiyo mitambo itakayokwenda kununuliwa itakuwa ni *scraper* au imetumika kidogo tu? Hili ndilo tatizo ambalo limekuwa kubwa sana katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Waziri ukija hapa ututolee ufafanuzi wa kina na Watanzania wote waweze kupata elimu ya kutosha. Lakini nadhani katika Muswada huu sehemu zote zipo sahihi zaidi na kikubwa kama nilivyosema awali ni kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao ukija kuangalia maeneo mengi karibuni Wabunge wote wanakubaliana karibu asilimia 98 ya Muswada huu isipokuwa kipengele hicho ndiyo kina changamoto kubwa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nimesema sina maneno mengi ya kusema, ni hilo tu nilitaka kuchangia hapo, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa sababu nimeweka mchango wangu katika mustakabali wa Taifa hili. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Jaffo. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, simuoni, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola na baadaye Murtaza Ali Mangungu. Mheshimiwa Mgalu tafadhali!

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika sheria hii ya Manunuzi iliyowasilishwa asubuhi hii na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbali ambayo waliona yana utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu katika sheria hii, naomba tujielekeze kwenye mapungufu makubwa yanayojitokeza kutokana na matumizi ya pesa kwenye ngazi mbalimbali za Serikali. Sisi sote ni mashuhuda wa mapungufu hayo katika ripoti za *CAG*, tumekuwa tukijionea mara kwa mara matumizi yasiyozingatia mpango wa manunuzi, matumizi ambayo hayajaidhinishwa na Bodi ya Zabuni, matumizi ambayo hayazingatii njia za ushindani, lakini nadhani tunatunga sheria mpya ya kuweza kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo ninaloliona siyo sheria, Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na nadhani hata wafadhili wengi wanaiunga mkono, sheria ilikuwa madhubuti. Tatizo ninaloliona ni *enforcement* ya sheria kwa sababu kila mwaka upungufu huu unajitokeza. Sasa sheria hii nimeipitia, sijaona kwamba ni nini cha ziada ambacho kimeongezeka ili matatizo yanayojitokeza kwenye Halmashauri zetu, kwenye Serikali Kuu na kwenye Mashirika ya Umma yaweze kupungua. Kwa sababu Sheria ukiipitia hizo wanazosema *Tender Board* ilikuwepo pia, matakwa ni yale yale, majukumu ya *Accounting Officer* ni yale yale, *Evaluation Team* majukumu yake ni yale yale, *Procurement Management Unit* ilitamkwa kwenye sheria iliyopita, lakini pamoja na yote hayo bado mapungufu yalikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunatunga sheria mpya baada ya kulitathmini na baada ya kujiuliza kwa nini kila mwaka tunapokea taarifa ambazo zinaonesha kabisa asilimia 55 za *procurement entities* hazifanyi *compliance* na sheria. Kwa hiyo, pamoja na kwamba naipongeza Serikali kwa kukubali maoni ya Kamati na maoni ya Wadau mbalimbali, lakini jambo la msingi liwe ni *enforcement* ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu asubuhi wamezungumza kwamba tunapitia, mimi nipo katika Kamati ya *LAAC,* tunaona ni namna gani matumizi ya pesa yanavyokwenda ndivyo sivyo hasa kwenye manunuzi. Tunaona ni namna gani bei, maana yake sisi sote pia ni wanunuzi, tunaona ni namna gani bei zinavyokuwa ni za juu zaidi kuliko bei ambazo ziko kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani Serikali ingeainisha kabisa ni namna gani sheria hii itasaidia kupambana na changamoto hizo ili tujiridhishe. Lakini wakati upungufu huu kama nilivyosema umeainishwa sijaona pengine labda kwenye kanuni ni adhabu gani ambazo zitaainishwa zaidi ili kuona wale ambao wanavunja sheria kwa makusudi mazima wanachukuliwa hatua gani kali ambazo Sheria ya mwaka 2004 hazikuainishwa na sasa hivi sheria hii ndiyo imeainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda pengine nichangie majukumu ya *Accounting Officer*, kama walivyosema wenzangu wengine kwamba huyu *Accounting Officer* amepewa majukumu mengi sana, anateua *Tender Board*, anateua *Evaluation Team* anafanya kazi nyingi, mwishoni ana-*approve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira ambayo wamesema wenzangu kwamba uaminifu wetu una mashaka, nadhani Serikali ingeingilia kati ili kuona itafanyaje kutafuta *check and balance.* Nashukuru upande wa Halmashauri wamewashirikisha Kamati ya Fedha, sisi tuliliona hilo, Wenyeviti wetu wanapewa mikataba ambayo imefanyiwa kazi na watendaji, kwa mfano juzi tumeona Kinondoni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sogeza *mic* yako vizuri.

**MHE. SUBIRA KHAMIS MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Manispaa ya Kinondoni wameingia mkataba na kampuni moja kujenga *apartment* huko *Osterbay Villa* ule mkataba ni wa maisha, Kinondoni wanapata asilimia 25 ndiye mwenye kiwanja, ndiye mmiliki, lakini yule mwekezaji anapata asilimia 75 na ni milele na milele. Sisi tumeona pale kuna upungufu katika mkataba na kwa kuwa alisaini Naibu Meya lakini huyo Naibu Meya amesaini kwa kushauriwa na Watendaji. Lakini Mkataba ule ungepitia kwenye Kamati ya Fedha na Mipango ni lazima wangetokea Madiwani ambao wangetilia mashaka inakuwaje? Kwamba sisi ndiyo wenye mali, sisi ndiyo wenye kiwanja, Mwekezaji amekuja tu tumpe mamlaka ya kupata asilimia 75 milele na milele, hii haiwezekani! Hatujawahi kuona mkataba wa namna hiyo, lakini imetokea na haiwezekani kuuvunja, mkataba ule umeingiwa na watendaji wapo na hamna aliyewajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maoni yangu nadhani pengine Serikali ingeongeza zaidi adhabu za kutoa kwa wale ambao watakwenda kinyume na sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa kuchangia kama walivyosema wenzangu ni hili la *Accounting Officer* kuomba kibali endapo manunuzi hayo yamevuka bajeti. Kwa kweli hoja hizi za manunuzi yaliyokwenda nje ya bajeti zipo na mara kwa mara zinatokea, lakini ipo kwenye sheria. Kifungu Na. 35(4) imetamka siku kumi na nne (14). Hivi tujiulize Halmashauri zote 133 na zinaongezeka zingine kwa *Pay Master General* ndani ya siku kumi na nne (14) inawezekana kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sheria haijasema kwenye Halmashauri kuna pesa zinatokana na vyanzo vyake *(own source)* ambazo zinatumika kwenye manunuzi, je, hapa *Accounting Officer* anafanyaje sheria haijasema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani iwe *strict prohibited* kwamba *Accounting Officer* yeyote haruhusiwi kufanya manunuzi yanayovuka nje ya bajeti kama kweli tumemtaka awe na *Annual Procurement Plan*, kama kweli tumemtaka awe na *Evaluation Team,* kwa nini afanye manunuzi nje ya bajeti? Kwa sababu unapopanga bajeti na kama sheria inavyotaka sasa hivi ilivyopendekezwa na Kamati kwamba mpango wa manunuzi uende sambamba na uandaaji wa bajeti, kwa hiyo ndani ya kipindi kile naamini wakati mambo haya yanakwenda sambamba ni lazima atakuwa na uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hii *approve* ya siku 14 ya *Pay Master General* ambaye ni Katibu Mkuu Hazina muda huu hautoshi, tutakuwa tunajidanganya na hizi hoja zitajitokeza mara kwa mara. Lakini jambo lingine kama nilivyosema kama Watendaji wetu wakiamua kujitoa kwa dhati, pengine tusingekuwa na haja ya kuwa na sheria kama hizi, kwa sababu sheria hizi zinafanya manunuzi yawe ya gharama.

Kukaa hii *Evaluation Team* ni posho, kukaa Bodi ya Zabuni ni posho, hao *PMU* nayo itabidi wakae ili kupanga hayo manunuzi na hapo ni posho. Kwa hiyo, utakuta kitu cha milioni ishirini gharama zake zinaweza kuongezeka mpaka milioni tano. Lakini kama tungekuwa wote tumejitoa na kuwa waadilifu nadhani hizi *process* zote hazikuwa na ulazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mmoja pia amesema mambo ya *Force Account*, nadhani Waziri kwenye Kanuni hilo aliweke kwa kuwa maeneo mengi tumeona kwa mfano tumetembelea Mvomero, nyumba ya Mkurugenzi inajengwa kwa milioni mia nne wala siyo ghorofa wala siyo nini! Hata wewe mwenyewe Mtanzania ukipewa milioni mia nne huwezi kujenga nyumba ya namna ile, kwa hiyo, mambo ya tenda kwamba *specification* zipo mamlaka za Serikali nazo hazisaidii. Kuna *TBA* wanaleta hizo *BOQ* yote hayo wanafuata sheria lakini kwa gharama kubwa sana. Hivi leo tumwuulize Mtanzania wa kawaida unapewa shilingi milioni mia nne utajenga nyumba ya vyumba vitatu? Lakini ame-*comply* na sheria lakini nyumba ni milioni mia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda kusema kama kweli tuna dhamira ya dhati, kuna mambo pengine hayana hata haja ya kufanya ushindani, mtu ukiwa na dhamira unaweza ukalifanya hilo jambo kwa hela kidogo na kwa *quality* inayotakiwa bila ya kuwa na haja ya kushindanisha. Kwa sababu unaposhindanisha na wale wanataka faida kubwa na pia *tender board* hizi watu siyo malaika, wanavujisha taarifa, wanatengeneza zile *BOQ,* wanawapa wanawa-*lead* kwamba jamani tenda iko kiasi fulani mwenzio ka-*tender* hiki na wewe fanya hivi. Kwa sababu ni lazima uwe na *estimate* zako kama *procuring entity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba watendaji kama kweli sheria ilikuwa na matatizo sawa, lakini Serikali imeziona hizo changamoto, wadau mbalimbali wamechangia, sasa tunawataka watuoneshe kweli kwamba sheria ile mwaka 2004 ilikuwa na matatizo. Lakini kwa kweli matatizo makubwa labda yalikuwa ni muda mrefu siku 105, lakini mambo mengi yamerudiwa ni yale yale. Lakini pia labda kwenye Kanuni nayo itamke wazi matumizi ya hizi *agency* zetu. Hawa *MSD* wanauza dawa lakini tukipita Halmashauri bei zao ni tofauti wamenunua kwa *private dealers* wanakwambia hazikuwepo, sijui *out of stock*, hawana uthibitisho wowote, kwa hiyo bado tatizo lipo.

Tunaweza tukatoa kanuni kwamba wanunue kwenye *agency* zetu lakini utekelezaji wa hizo kanuni haupo kwa sababu wanaongea na watu wa *MSD* au mtu anakwenda anamgongea *out of stock* anakwenda kununua kwa bei anazozijua yeye. Kwa hiyo, matatizo makubwa kama alivyosema Mbunge mwenzangu aliyepita punde ni uaminifu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu manunuzi ya vitu vilivyotumika, natambua kwamba ni kweli tunatumia vitu *used* na sina mashaka na hivi vitu ambavyo vimetajwa, lakini bado naungana na wale waliosema tusimshirikishe Rais kwenye manunuzi haya, kwamba *approval* itoke kwenye *cabinet,* hapana. Kama hii *procuring entity* hiyo hiyo iendelee ipeleke labda kama ni *PPRA* iingilie kati kwenye kuridhia manunuzi haya ambayo tunasema labda ni *used* au kuweka *mechanism* nyingine yoyote ili kuwe na *check and balance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwamba, ni kweli kwa wakati mwingine hatuwezi kusema kila kitu tutaweza kununua vitu vipya siyo rahisi, lakini ni uaminifu, uzalendo na kwamba tutafute *mechanism* juu ya nani hasa atakayeweza kujiridhisha kwamba hii *evaluation team* imefanya sawasawa, hii kweli ni *used* lakini inatufaa katika mazingira yetu na *factors* mbalimbali zizingatiwe kabla hatujafikia maamuzi ya kusema kwamba tununue bidhaa za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, katika ukurasa wa 58, *emergency procurement*, kwa kweli siungi mkono kwamba, *Accounting Officer* peke yake, hapa tunaowalalamikia ni *Accounting Officers* na ndiyo hao ambao wametufikisha hapa mpaka tunabadilisha sheria kuona kwamba ile ilikuwa na upungufu, leo yeye peke yake kama binadamu aamue kwamba hii ni *emergency* na hii siyo *emergency*, nadhani hapa siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pengine kwenye ngazi ya Halmashauri ipitie kwenye Kamati ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuruna naunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa Taifa letu. Ingawa

tumepewa leo Muswada huu lakini tumetumia muda kuusoma vizuri, tumejaribu kuangalia vile vipengele ambavyo ni muhimu kwa Taifa letu. Kwa ujumla napenda nipongeze kwamba, Kamati iliyoshughulikia na kuangalia kwa undani imejaribu kutoa maoni ambayo yanalingana na hali halisi ya nchi yetu. Vile vile, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kuangalia maeneo yale ambayo ni muhimu ambayo tunaweza tukayafanya kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo nimelifurahia sana kwa mfano, Madiwani kushirikishwa katika ununuzi ni suala la muhimu sana katika Halmashauri zetu. Tumeona kuna mikataba mingi sana ambayo inaingiwa katika Halmashauri zetu kwa mfano, mikataba ya ujenzi wa barabara, unaweza ukaona wananchi wanataka kumwuuliza Diwani na Diwani anasema yeye hajui mkaulize Watendaji. Lakini kama Madiwani watakuwa wanashirikishwa kwenye tenda za mikataba tutakuwa tumeondoa tatizo kubwa sana ili kuondoa lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hata Madiwani wakiulizwa maswali ya tenda katika Halmashauri wanashindwa kujibu, lakini wakishirikishwa hiyo itasaidia sana. Katika kipengele hicho, napenda kupongeza kabisa kuingiza katika hii sera ya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kujikita, sasa huku napata wasiwasi kidogo kwa sababu kuna *terms* mbili zinatumika hapa, kuna vitu chakavu na vitu *used*, hapa ndiyo sisi tunachanganyikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali inaweka sheria kwamba tutanunua vitu chakavu hapo, sitaunga mkono, lakini kama tunakuwa *specifically* tunasema *used* na *used for how long*? Ni lazima tu-*specify* hapo. Kwa sababu tunaweza tukasema tunanunua vitu *used,* matokeo yake watu wakageuka badala ya kununua *used,* wananunua vitu vilivyokufa kabisa (*scraps*) hapo italeta matatizo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kipengele namba 66 hakija-*specify* kwamba *used how*? Waziri wa Fedha angeeleza vizuri, kwa mfano, unanunua ndege imetumika labda mwaka mmoja, hiyo ni *used* au imetumika miezi sita, pia tunasema *used*. Lakini unanunua ndege ambayo imetumika miaka 20, unaileta hapa, hiyo siyo *used,* hiyo ni *scraps* tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo inabidi Watanzania tuelewe vizuri hizi *terms* mbili ambazo tumezitumia hapa kwa sababu sasa hivi watu wameshachanganyikiwa tayari, tunafikiri sasa hivi tunakwenda kununua *scraps* ambazo wenzetu wamezishatumia wanataka ku-*dump* kwetu. Sasa hata *inflation* utaona sasa itakuwa maajabu hata uchumi hapo utakuwaje, kwa sababu ku-*maintain* uchumi wa nchi yoyote ile lazima uweke *restriction* kwenye *importation* na kama unaweka *importation* ya vitu ambavyo vimechakaa nje ukaingiza kwetu basi tayari tumekufa. Sasa sielewi hapa, mlikuwa mna maana ipi lakini nasema hivi kama tunalenga vitu *used* ambavyo kwenye *normal sense* naunga mkono, lakini kama ni *used* zile *scraps* sitaunga mkono hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimeliona, tukiangalia katika Halmashauri hata katika *Central Government* unaweza ukaona manunuzi yanafanyika pale bila kufuata utaratibu kwa mfano, unaweza kukuta mtu amenunua labda gari, anasema kwamba *documents* hazipo, lakini akiambiwa azitafute, baada ya miezi mitatu utasikia *documents* wameshazipata na *price* inakuwa tofauti. Sasa hii ndio inatuchanganya, ambacho kitu kinachotakiwa hapa wenzangu wameshaongea tayari, sisi tunakabiliwa na suala la uaminifu kwamba katika utendaji wetu hatuna uaminifu katika manunuzi na Taifa hili linaingia gharama kubwa sana katika manunuzi.

Sasa naiomba Serikali, Muswada huu tunaupitisha leo, lakini tuhakikishe kwamba tunafuata sheria. Sheria za manunuzi inabidi zisimamiwe vizuri. Kama hatutasimamia zile sheria ndio hapo tutakwenda kununua vitu ambavyo havifai. Tutanunua vitu ambavyo vimekuwa *expired*. Sasa hivi bahati mbaya tume-*highlight,* tumesema kwamba tunataka tununue meli iliyotumika, tununue ndege iliyotumika, tununue treni zilizotumika. Sasa hapa hata wale wenzetu wanaotumia vitu hivi wameshasikia kwamba sasa hivi zile *scraps* ambazo wameshazitupa huko wanaanza kupaka rangi ili waseme wanatuuzia sisi huku, lazima tuwe makini sana kwa sababu wao

wanafanya biashara, hakuna Taifa ambalo halifanyi biashara hata siku moja. Kwa hiyo, wakisikia Watanzania tayari tumeweka kwenye sheria vitu vilivyotumika wanaanza ku-*modify* kupaka rangi na sisi tayari tunakwenda kuangalia, tunasema hii inafaa, hapo tutakuwa tumeshaumia tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe kitengo cha ununuzi tuna watu makini ambao wanakwenda kuangalia ili waone je, hivi vitu kweli tunaweza tukanunua? Sisi tuna tatizo kwenye umakini hapa, unaweza kusema mtu makini akaangalie analeta mitambo ya ajabu ajabu halafu baadaye tunaanza kusema mtu awekwe ndani. Sasa ndugu zangu, naona tuhakikishe uongozi unaoshughulikia masuala ya manunuzi lazima ujiridhishe kwamba hatua yoyote, wakileta vitu ambavyo havifai, vikafanya kazi miezi miwili, wako *responsible* kuwekwa ndani, hiyo lazima uidhinishe. Bila kufanya hivyo tutaletewa vitu vya ajabu sana hapa. Sheria haina matatizo, sheria zipo, hata sheria za zamani wala hazina matatizo, ukiona mtu amesema sheria zetu zina matatizo labda yeye ana matatizo, sheria ni utekelezaji na utekelezaji wetu sisi ni mbovu, ni hapo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tungekuwa tunajadili masuala ya utekelezaji, usimamiaji mzuri wala masuala mengine ya umaskini hayatakuwepo. Halafu usije ukasema sisi Tanzania tunashindwa kununua vitu ambavyo vinafaa kwa sababu ya umaskini. Hili suala la umaskini huwa linanisumbua sana kichwani kwa sababu tuna madini tayari, umaskini uko wapi? Madini yako pale, yale madini ilitakiwa ifikiwe muafaka sisi tuwe tunachimba wenyewe na kuuza wenyewe. Sasa wale wawekezaji wanakupangia sasa hivi hata masharti magumu yanakuja sasa sijui tutafanyaje. Maana kuna masharti mengine hata kutamka hapa hatuwezi na hatupendi kuyasikia na watasema kama hamnunui vile vyuma vilivyochakaa, ndege zilizochakaa basi lile sharti linarudi, hapa mtafanyaje? Watapakapaka rangi, watasema sisi Waingereza tunasema, lazima mnunue, kama hamtaki kununua sharti liko pale pale, sasa sijui hapa itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuwe makini sana tunapofanya maamuzi. *Term* iliyotumika kwamba *used, term* hiyo haina shida, shida ni sisi wenyewe, hapo ndio penye shida. Kwa sababu macho yetu inaelekea hayawezi kuangalia kipi ni *used*, kipi ambacho kimechakaa na hakifai kutumika. Tunaona hata madawa mengine yanakuja wanasema haya madawa yamepitwa na wakati. Sasa unaanza kushangaa haya madawa yaliingiaje kama yamepitwa na wakati, hawakuona? Sasa hilo ni tatizo. Tunaletewa hapa utasikia kuna vitu vingine vinachomwa huko sijui vinafanyaje, vinaingizwa bila mpangilio, watu wanasema vitu *fake*, sasa huu u-*fake* huwa najiuliza hatuuoni kuanzia kule kule? Kama tumeshindwa kuona vile vitu ambavyo ni vipya (*brand new)* kabisa, ambavyo havina matatizo, je, hivi *used* tutaona? Hili ndio suala la kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine tumekuja kuyaona Dar es Salaam, sasa je, vile *used* ambavyo vimetumika na viko sijui kwenye *yard* gani tutaona kweli hiki kinaweza kikakaa hata zaidi ya miaka 20. Hapo tutaingia katika matatizo. Bahati mbaya sana vitu ambavyo tumevilenga yaani kikipata hitilafu chombo kimoja tu watu wamekufa. Kwa mfano, fikiria ndege, kweli umepanda ndege *used,* halafu ikaleta matatizo huko angani, utafanyaje? Nafuu ungesema *used car* kwa sababu hiyo hata ikikorofisha utagundua, lakini ndege huwezi ukagundua, utagundua umeshapoteza maisha ya watu. Ukija katika treni unasema sijui unaleta vichwa ambavyo vimechakaa, utashangaa kichwa kingine kinaachana na injini huko kinaanza safari ya kwake, utaanza kushangaa kinaua watu, imeshatokea. Tunatoa *recommendation,* unasema ilikuwa *used*, itawakuaje hapo, itakuwa aibu. (*Makofi*)

Sasa ndugu zangu Wabunge nafikiria kwa sababu Watanzania wanatutegemea sana, itakuja kutokea aibu tukinunua kitu *used,* halafu kikaua Watanzania wengi na wananchi wakasema, Wabunge tuliowachagua ndio walipitisha kitu ambacho kimechakaa, hapo tutapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumalizia kipengele hiki namba 66, watu ambao wataji-*commit* kuidhinisha, halafu nadhani kuna wenzangu waliochangia wamesema kwamba, Rais kwenye kipengele hiki asiidhinishe, hata mimi naunga mkono kwa sababu najua kitaleta matatizo hapa. Sasa kwa nini tumuingize Rais kwenye matatizo makubwa? Nafuu tuwape watendaji ili tuwashike vizuri maana tutawasimamia. Wewe ukienda kununua kitu ambacho

hakifai, kikatumika miezi miwili, miezi mitatu tunasema sheria zichukue mkondo wake. Lakini tukimweka mkubwa pale, utafanyaje? Hali itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichangie hivyo lakini naiomba Serikali iwe makini sana katika kufanya maamuzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya mambo chakavu. Kimsingi nafikiri Waheshimiwa Wabunge, tungelikuwa tunajikita na kueleza ile *provision* inasema nini, tukiwa tunasema tu chakavu kama vile Muswada huu umeletwa kwa ajili ya kuelezea manunuzi ya vitu chakavu. Sasa naomba wale ambao bado mna nafasi na kwa sababu tunaendelea basi muwe *specific* ili Serikali iweze kupata ushauri huo vizuri zaidi. Kwa sababu ukisoma vizuri katika hiyo *provision* inasema: "*Where the public interest demands",* yaani si jambo la kawaida na pale inapotokeza kweli kuna ulazima sana. Sasa tusiseme hali hiyo ikaonekana kama Muswada wote huu umeletwa kwa ajili ya manunuzi ya vitu chakavu. Naomba tu, ili tuweze kutoa msaada mzuri kwa Serikali na ili hoja yao iwe nzuri, basi tuwe *very specific* katika kutoa mawazo yetu. Ahsante sana.

**MHE. SLYVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika *agenda* inayoendelea. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa kuja na Muswada huu. Naamini Muswada huu tutakapoupitisha ndio utakuwa msimamizi wa masuala yote ya manunuzi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa vile sote tunakubaliana kwamba manunuzi huchukua asilimia kumi ya pato la Taifa na kwa bajeti tuliyoipitisha maana yake tunazungumzia trilioni 1.3, ni hela nyingi sana. Ushauri wangu katika suala hili, tunapitisha Muswada na baadaye utakuwa Sheria ya Ununuzi, naomba sana Serikali yetu iwe makini kwa sababu bajeti ya trilioni 1.3 si kitu kidogo, fedha hizi ni nyingi. Kwa hiyo, kwanza naomba uzalendo uwe mbele yetu kwa maana kwamba, Watanzania hawa ambao wametuweka humu ndani, tuhakikishe tunawatendea haki na watendaji ambao wamepata dhamana hizi wawe makini na waongozwe na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Muswada wa Ununuzi maana yake tuna–*procure* zile *services* kwa mfano, *consultancy*, kwenye taaluma hizi kama tunahitaji watafiti au ushauri elekezi mara nyingi nimeona uzoefu ni kwamba, tunapenda sana kuchukua taasisi za nje. Sasa ushauri wangu pale ambapo Watanzania wanaweza kufanya kazi hizi kwa vile pia huchukua fedha nyingi sana, nakumbuka *research* kadhaa nyuma mtaalam ameletwa analipwa dola 5000 kwa siku, lakini kazi hiyo angeweza kufanya Mtanzania. Mtaalam kazi yake ana-*polish*, Kiingereza, si *issue* hapa, sisi ni Waswahili kwa vile watalaam wetu wazalendo, nazungumzia kwenye Kifungu cha 4(3) ambacho kinazungumza mambo ya *consultancy* na mambo mengine, tuwape kipaumbele watalaam wazalendo kwa sababu hii pia ni *incentive* kwao kwani Taifa limetumia muda mwingi sana kuwasomesha, sasa utalaam wao uonekane hapa. Wazungu tuwaache na mambo yao, labda pale inapobidi yaani tumepungukiwa utaalam huo ndio tuelekee ku-*outsource* utalaam wao. Vinginevyo *consultancy* hizi zisitoke nje wakati wazalendo tunao. Hivi leo tunapozungumza na nilimsikia Naibu Waziri wa Elimu leo asubuhi akisema tunavyo Vyuo Vikuu 40, naamini watalaam watakuwa ni wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia ni hili ambalo limezungumzwa sana hapa la kununua inapobidi vitu vinunuliwe. Lakini sielewi Serikali inapojielekeza kwenye masuala ya vitu ambavyo vimetumika. Nadhani Wabunge wengine wametoa mfano, tuna magari *used*, magari *used* kwa sababu ya *individual* hiyo ni *preference* yako, lakini kwa *Government* naomba Serikali iliepuke suala hili. Iliepuke kwa sababu tunaamini kitu ambacho ni *used* mara nyingi hata teknolojia yake imepita, unaponunua kitu ambacho ni *used, spare parts* zake ziko wapi? Kwa hiyo, katika kuwatendea haki Watanzania hata kama limetumika hilo nenola inapobidi, lakini hapana jamani. Naomba neno hili tuliondoe, tuwatendee haki Watanzania hakuna inapobidi, inabidi wapi? Maisha yao ni muhimu sana. Sisi hapa likitokea la kutokea kwa mfano, unanunua kitu *used and then* zile *mark* na *costs* zake zinakuwa zaidi ya kile kipya, utatumia zaidi na Mzee Mwinyi alisema dezo ni ghali, tusipende vitu vya dezo kwa sababu vitatugharimu mara kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu chini ya Kiongozi wetu mpendwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, tusikubali hivi vitu ambavyo tunasema ikibidi, hakuna cha kubidi hapa, maisha ya Tanzania ni muhimu zaidi. Nakumbuka tuliponunua ndege ya Rais tulisema kwa ajili ya Rais wetu, hawezi kusafiri kwa meli kwenda Ulaya, kwa gharama yoyote tutanunua, basi hivi vitu ambavyo tunahisi ni muhimu tuvinunueni kwa gharama yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nishauri wenzangu yale ambayo tunahisi ni ya maslahi, basi tushikane mkono wote bila kuangalia itikadi zetu, tusikilizane hapa ndani. Lengo letu ni moja ku-*deliver* huduma kwa Watanzania. Sisi watunga sheria, tukitunga sheria kwa kukubaliana hapa ambazo zinapotosha baadaye tutakuja kutafuta mchawi ni nani. Sasa ukitafuta mchawi wakati umeshaumiza watu, sisi juzi tumeona kwetu kule Unguja, Meli imezama, meli ile ilikuwa imetumika miaka mingi sana, sasa hivi kila kona ya Zanzibar ni majonzi, ni msiba mkubwa. Sasa je, tungekuwa tuna meli ambayo tuna hakika ni mpya, haya yasingetokea na maisha yaliyopotea hayana fidia. Tuna mifano mingi sana huko nyuma, kwa hiyo, tunaomba tujifunze kwa matukio ambayo yametokea hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu Muswada huu hauzungumzii kununua tu lakini pia ku-*dispose,* niseme kwamba, tunapouza vitu ambavyo vimetumika vya *public* ifanywe tathmini ya makini. Kwa sababu kuuza *at a given price* kitu ambacho kina hali ya ubora, basi naomba wanaohusika wawe na uzalendo, tusiuze tu kwa sababu tunahisi kwamba hiki unambarikia rafiki yako au jamaa yako, lakini ni kitu ambacho kilikuwa bado kina *life span* ya kutumika na kusaidia maendeleo ya nchi yetu. Sasa hili pia la kuuza vitu vyetu, vitu vya *public*, vitu vya Serikali, naomba pia tuliangalie kwa makini, tusiangalie tu kununua kwa sababu kuna kununua na kuuza vitu vya Serikali au vitu vya *public* ambavyo baada ya kipindi fulani vinakuwa havifai kwa sababu ya *maintenance costs* zake, basi tuwe makini pia kwenye ku-*dispose* hivi vitu vya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie ile *book value* yake siyo kwa sababu kuna rafiki yangu ana kampuni yake vinaweza vikasaidia *then* tunavitoa hapana, hizi *public goods* ni *public funds* zimetumika kuvi-*acquire*. Hapa tunazungumzia kununua, lakini pia tuzungumzie namna ya kuviuza vinapokuwa vimeshamaliza muda wake. Wale ambao watashindwa kuwa waadilifu kuna sehemu moja imezungumzia habari ya *penalties,* sasa kutakuwa na adhabu kali, tena watangazwe tuwajue hawa ambao wamehusika katika kuuza vitu vya umma kwa bei ya kutupwa au bei poa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya hivi tunajengea imani kwa Serikali, lakini zaidi Chama chetu ambacho kinaongoza nchi hii. Tunataka Chama chetu kiendelee kutawala lakini kitatawala baada ya kuwa kinawahudumia ipasavyo Watanzania, vinginevyo tuko kwenye vyama vingi, tutakuja kupigwa mweleka na tusingependa itokee labda baada ya miaka 50. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaweza kufanikiwa kama Muswada huu tutaujadili kwa makini. Muswada huu utatuletea imani na utarudisha matumaini kwa Watanzania, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu lijadili masuala haya na Serikali yetu iwe sikivu pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wanapiga kelele sana, basi isikilize. Lakini kama itasimamia na *it is irreversible,* ita-*cost* kwa sababu baada ya miaka hii minne, mwaka 2015 tutakuja kuwa *evaluated* tumetoa huduma gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilipenda nizungumzie hapa habari ya *procurement*, habari ya ku-*dispose public goods*, habari ya uadilifu na hata katika taasisi za ulinzi tunapongeza sana. Lakini tuna mifano pia kwamba, vifaa vya kijeshi vinanunuliwa ambavyo viko katika *poor quality,* lakini kwa sababu vinatumika kwa ajili ya kulinda maisha ya Watanzania na jeshi letu lazima liwe na vifaa vya kisasa, lakini kutokana na usiri ambao tunausema kwamba si vizuri sana kuelezea mambo ya ulinzi kwa hadhara kubwa, naomba sasa hawa ambao wana wajibu huu wazingatie uzalendo. Tuna mifano katika nchi za Afrika, Zambia wakati wa Marehemu Chiluba kanunua ndege nyingi sana ambazo zilikuwa *under quality* na tunakumbuka kwenye mkutano ule uliofanyika Arusha wa wafanyabiashara, Helikopta ilikuwa inafanya *patrol*, ika-*fell*, bila shaka ilikuwa ina matatizo toka inanunuliwa. Siyo Helikopta ile tu, viko vitu vingi. Sasa naomba pia

kwenye taasisi hizi za ulinzi wahusika wawe waadilifu sana kama walivyojitolea maisha yao kulinda Watanzania, basi na wanapofanya *procurement* katika vifaa vya kijeshi wawe wazalendo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kukushukuru sana. (*Makofi*)

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Ibara ya 68(7) kuomba Mwongozo wako kwa sababu kabla ya Mheshimiwa Sylvester kuanza kuzungumza, ulisimama hapa na ukatoa maelekezo, lakini ulikuwa umetoa maelekezo kama mara ya pili, lakini hiyo ya tatu ukawa umesimama, unajaribu kuwaambia Wabunge ambao watachangia, wajaribu kuwa *specific* na unajaribu kusema kwamba Wabunge wote wanachangia *as if issue* peke yake ni hii ya 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naogopa kwamba, hayo maelekezo unayotoa, unayatoa *as if* unataka ku-*limit* mchango na mawazo ya Wabunge wanavyochangia hapa. Kwa sababu *issue* iliyopo kwenye hii Ibara ya 68 na umeisoma hapo kidogo kwamba tunaposema: "*Where the public interest's demands.*" Sasa *issue* kubwa ya Wabunge hapa ni kwamba *who is going to determine* hii *public interest of that particular time* na mambo kama haya yameshatokea na Wabunge wana *interest* kubwa hapa kwa sababu kuna matatizo, hivi ndivyo vitu vinavyotoa *loophole,* matokeo yake tunafanya manunuzi ambayo sio kwa *interest* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama maelekezo unayotoa kweli yana nia njema, lakini na-*feel* kama yanataka ku-*limit* jinsi gani tunatakiwa kuchangia humu ndani.

**MWENYEKITI**: Hii kali maana najitolea Mwongozo mwenyewe sasa. Labda nitoe tu ufafanuzi wa kile nilichokisema kwa sababu siwezi kujitolea Mwongozo, ingawa umeingia kwa *entry* hiyo ya Mwongozo. Dhamira yangu ilikuwa ni kujaribu kufanya kikao, ukiwa Mwenyekiti unakipa kitu unachokisimamia *test*, *I just wanted to give the test* ya kitu ambacho mimi ndiyo Mwenyekiti. Kwa sababu ningependa sana kupata mijadala ambayo ina afya, kwa mfano, ulichokisema sasa kwamba hii *where it becomes for the public interest* inakuaje, yaani nataka ladha hiyo, nikasema pengine ni vizuri mkawa *so specific* katika hili m-*actuate* vizuri. Kwa hiyo, dhamira yangu ilikuwa ni hiyo ambayo unaitaka ya kusema kwa uwazi zaidi sio kwa maana ya ku-*limit*. Tuendelee.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Serukamba na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Idd Azzan, simuoni, Mheshimiwa Jitu Soni. Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii niweze kuchangia Muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa kweli, *procurement* inachukua nafasi kubwa sana katika kuongoza nchi na ukisoma madhumuni na sababu za Muswada huu, yako madhumuni karibu kumi na unaona kila moja lina nafasi yake katika kuleta maendeleo. Unachokiona kwenye Muswada huu, wamejaribu kujibu kila aina ya mazingira tuliyonayo leo, ukisoma yale madhumuni, utaona kila jambo unataka kutibu jambo gani. Labda uniruhusu maana kule mwisho angalau wameandika kwa Kiswahili ili tuweze kuelewana vizuri. Anasema Muswada umegawika sehemu kumi zinazofafanua mambo mbalimbali yanayopendekezwa katika sheria hii.

Sehemu ya kwanza ni majina, sehemu ya pili, Divisheni ya Sera ya Ununuzi wa Umma. Sehemu ya tatu, kuanzishwa kwa Mamlaka. Sehemu ya nne, inaweka masharti ya kuanzisha vyombo vya kushughulikia masuala ya ununuzi wa umma. Sehemu ya tano pia kuna misingi ya ununuzi wa umma na mambo mengine yanayoweka masharti kwa Mamlaka zenye dhamana. Sehemu ya sita, inapendekeza masharti na vigezo vya kuchagua njia ya ununuzi. Sehemu ya saba, inapendekeza kuweka utaratibu wa kufanya ununuzi chini ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Sehemu ya nane inapendekeza kuweka masharti yanayokataza watumishi wa umma kujiusisha na vitendo vya rushwa. Sehemu ya tisa, inapendekeza kuweka masharti ya kusuluhisha migogoro ya zabuni. Unaweza ukaona sheria hii inakuja kujibu mambo mengi sana ambayo huwa yanatokea kwa wale ambao wamefanya manunuzi au wamewahi kufanya kazi kwenye *procurement unit* na kwa kweli niipongeze Serikali kwa kuleta sheria hii na niwapongeze hata Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kuipitia vizuri sheria hii. (*Makofi*)

Unaweza kuona Kamati ya Fedha na Uchumi hawakuwa na haraka kwenye kuleta sheria hii, wamechukua muda na kwa kweli wamefanya kazi ya kutosha. Ukiangalia, labda nianze katika mambo machache. La kwanza, katika sheria hii kuna mahali ambapo inabidi kwenda kwenye Baraza la Mawaziri ili waweze kuridhia baadhi ya mambo, hii siikubali. Nadhani umefika wakati tuanze kuwa *responsible*, *organisation* inayohusika iwe *responsible* na manunuzi yake, tukianza kila kitu nataka hiki nitakiandikia kiende kwenye Baraza la Mawaziri, maana yake ni moja tu, kila mtu anaondoka kuwa *responsible*. Kwa hiyo, likiharibika ni Baraza la Mawaziri liliamua. Ningetaka manunuzi haya kama yanafanywa na *Department A* waende mpaka mwisho, kama kuna jambo hawaelewani vizuri, waende kwenye Mamlaka ya *PPRA* ili itoe maelekezo ili kesho likiharibika jambo tunaye wa kumuuliza. Lakini ukianza kusema jambo hili liende kwenye Baraza la Mawaziri, unapanua wigo na kwa kweli moja ya matatizo yetu tunayo-*face* katika nchi hii, hakuna ambaye anataka kuamua mwenyewe maana yake tutakaa vikao, tutapeleka kwenye Baraza la Mawaziri, sasa unamshika nani ikishakuwa Baraza lote la Mawaziri maana yake tutamshika Rais? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba sana, tunapotengeneza sheria hii tuseme kila wanaofanya manunuzi wawe *responsible* na manunuzi yao ili kesho tuwe na wa kumuuliza. Wakimaliza manunuzi wanakuambia, *the best practice* ukishamaliza manunuzi unafanya *post-mortem,* unaanza toka siku ya kwanza umetangaza, umeandaa zile *documents*, umefanya *evaluation*, sijui umefanya *negotiation*, ume-*award* mpaka mtu umempa *contract,* kwa hiyo unaangalia, je katika hii *audit trend* nimekosea wapi? Ili hata kesho ikitokea *tender* nyingine ya namna hiyo utajua wapi mlikosea na muweze kusahihisha kwa sababu *experience* inasaidia katika kufanya vitu viwe vizuri zaidi. Kwa hiyo, ninachosema, tuanze kuweka *responsibility* na kila mtu awe *responsible* kwa mambo ambayo ameamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *lowest evaluated bidder*. Hii *idea* inanisumbua sana, kwenye miradi hii unaweza ukaamua ukasema mradi huu tunatangaza, lakini tutafanya *pre-qualification*, ukishafanya *pre-qualification* maana yake nini? Utawachambua, utasema wamebaki hawa wanne, nadhani hawa ni wazuri, mnakwenda mnaanza na *technical part of i*t, unasema katika hawa watatu waliobaki, *technical* wamepita viwango, kwa hiyo, sasa tunakwenda kufungua upande wa fedha. Kwenye fedha unasema ni *lowest evaluated*, kwamba aliyeweka hela kidogo huyu ndiye tunampa, *fine* amepita kwenye hii *area*. Madhara yake tumeyaona mara nyingi sana, amekuwa *lowest evaluated bidder* ana-*end up* hajamaliza mkataba. Ukiangalia ile ya *engineer's estimate* ya kwenu mliyoiandaa, inaonesha kwamba, kazi hii nadhani nitaifanya kwa shilingi tano, nyie wenyewe mmekaa kwa sababu mnajua, anakuja mtu anasema kazi hii ataifanya kwa shilingi tatu na nusu na nyie mnakubali, kesho asipofanikiwa mnamlaumu nani? Kwa hiyo, nadhani umefika wakati, hii *area* nayo tuiangalie vizuri sana, habari ya *lowest evaluated bidder,* hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 nilikwenda *International Law Institute* (*ILI*) kusoma *procurement* katika miradi ya *World Bank,* zile nchi zilizoendelea, hakuna habari tena ya *lowest evaluated bidder*, wao wanachoangalia, anaangalia bajeti ya kazi hii ni kiasi gani, anawatafuta tena wao wanakwenda hadi *single sourcing*, anatafuta watu ambao ni *expert* kwenye hiyo *area*, anawaambia leteni *evaluation* yenu, anaangalia je wana- *meet* na nilichoandaa? *By doing that* uta- *acquire issue* ya *quality*, lakini ukienda kwenye *lowest evaluated bidder, quality* inakuwa *jeopardised* na matokeo yake, tuna *end up* na *variations* nyingi sana. Kwa hiyo, nadhani umefika wakati na kwa kweli suala la *procurement* linahitaji *trust* zaidi kuliko sheria. Wako watu wanaongea hapa, hii ndiyo njia ya wizi, nasema hivi kwenye *procurement trust* ndiyo *number one*, tusipo *deal* na suala la kujenga *trust*, atakuja mtu, atafuata sheria hii *A to Z* na bado anawapiga. Mkienda kumkagua hakuna utakapomkuta hata sehemu moja, kwa sababu vitu hivi wanaofanya ni binadam, *these things are technical*. Yule aliyeandaa *bidding document* anachukua anawapa

watu watatu, wale watu wanakuja wakileta *document* yao, *word by word* unamkamata wapi na *price* wanapanga, wanakwambia *price* yetu hii hapa, usishuke chini ya hiki, akifika anapewa kazi, hawezi ku-*perform* na watu wametengeneza utaratibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema zaidi kwenye *procurement* ni suala la *trust* zaidi na lazima tuijenge kwenye *society* na umefika wakati tuone mahali hii ni nchi yetu na hapa ni kwetu, tuifanyie kazi vizuri, tupate *the best, out of it*. Tupate *value of our money*, lazima tuanze kuileta hii elimu kwa sana ili watu waondoke huko. Ndiyo maana katika nchi zilizoendelea, nilimuuliza *Professor,* kwa nini nyie mnakwenda *straight*, kwa nini sisi twende kwenye kutangaza? Akasema huko kwenu *trust* hakuna. Kwa hiyo, *we are trying* kuweka *process* ambayo itazuia vitu vya hovyo na naona kwenye sheria hii hilo limekuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ununuzi wa vitu *used*. Ukisikiliza hapa Bungeni, ninachojifunza hapa cha kwanza, wala hatukukielewa hiki kitu. *Nowhere* kwenye Muswada huu wamesema kununua *scrap*, hakuna, asimame mtu aniambie, wapi tumesema tutanunua *scrap*, *unless* sijui Kiingereza, walichosema ni kununua vitu *used*, lakini kwenye mazingira ambayo yatakuwa ni ya lazima sana, ambayo unadhani kuna *interest*. Wako watu wanasema ukinunua *used* unaua watu, nitawapa mfano, Kigoma kuna Meli inaitwa *MV* Liemba, meli ile imenunuliwa mwaka 1905, juzi juzi hapa baada ya uhuru tukanunua meli mpya kabisa ya Mwongozi, imekufa, Liemba bado ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu hapa tuongee vitu hivi tukijua, zamani wakati tuna *East African Airways* walikuwa wananua ndege zilizotumika za *British Airways* na zinafanya kazi, tumesahau historia, tunachosema tutumie vitu *used* katika mazingira ambayo yanawezekana. Kwa mfano kwenye ndege, jamani, ndege ikishanunuliwa leo, ikaanza kutumika, ndege ukishafanya *checks* ni *almost* hiyo tayari ni *new* ndege, *I mean this is how this business is going on in the world*, biashara hii inafanyika hivyo. Watu, wanasema sisi tuna hela nyingi sana, tununue mpya, hatuwezi tusidanganyane. Bado tuna matatizo kama nchi, hatujamaliza barabara, maji na kadhalika, jamani tuwe wakweli. Lakini hapa kuna mtu mmoja ametania hapa, amesema Wabunge karibu asilimia 95, tumenunua magari *used,* mbona hatujafa? Maana lazima tuanzie kwetu wenyewe, wanasema *charity begins at home.* Kama tunaitaka Serikali inunue vitu vipya, Serikali hii tajiri tuanze wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, naiomba Serikali iwe makini tu kwenye kununua vitu vya namna hii. Kwa mfano, leo unaongelea reli ya kati, reli hii ya kati, aina ya reli hii hamna duniani wanaotumia reli hii, aina ya mabehewa haya hayapo duniani, ukisema unakwenda kununua mapya unanunua wapi? Wenzetu wameshaondoka huko, ndiyo maana tunaiomba Serikali iende kwende *standard gauge,* ambayo tunaweza tukaenda kwingine duniani na tukapata. Kwa hiyo, kwa sasa hali tuliyonayo, hatuna uchaguzi, lazima tununue vitu hivi ili na watu hawa wa Kigoma, Tabora na Mwanza, wapate *service*, hili hatuwezi kuliepuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu amesema hapa, nchi hii imekaa gizani eti kwa sababu tumeambiwa tusinunue *Dowans*, ukiuliza *Dowans* alitwambia Dokta Rashid nilikuwepo kwenye Kamati ya *POAC*, mtambo mmoja wa *megawatts* 40 ulikuwa umetumika siku 30, mitambo ile mingine *megawatts* zilizobaki, imetumika miaka miwili na nusu, tumesema na lakini yeye akaenda mbali, akatafuta watu kutoka Ujerumani kuja kuangalia *worthiness* ya zile *machines*, wanasema mkizinunua leo mtafanya *major overall* baada ya miaka 20. Watu wakasema zimetumika, hatuwezi kununua, nchi bora iingie gizani, *yes we did,* tumeingia gizani, tumepata hasara, uchumi umeporomoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo kazi ya sisi wanasiasa tunataka kuiongoza nchi namna hii. Tafadhalini sana tuwe wakweli kwa nafsi zetu, lakini leo amekuja mzungu, kwa mashine hizo hizo anatuuzia umeme na tunanunua na majumbani kwetu hakuna ambaye ame-*boycott* kutumia umeme huo. Niambieni ni nani nyumbani kwake amesema umeme huu kwa sababu unatoka kwa huyu, ambao ni *used* siutaki, naomba m-*disconnect* kwangu, nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Mmarekani hapa akasema *this is the best machines*, zinatumia gesi, mnahangaika na *environment, this is the best country*, mnashangilia hivi. Jamani

tuiache Serikali na naamini watu wa Serikali jamani tusidhani ni wajinga hivyo, tusidhani wataalam wa nchi hii ni wajinga hivyo, tusidhani sisi ni wazalendo kuliko watu wengine. *(Makofi)*

Hii tabia inayoanzwa kujengwa humu ndani utadhani humu ndani ndiyo kuna wazalendo peke yake, tukianza kuchunguzana hapa, nani anabaki? Tuambiane ukweli hapa. Ninachosema ni kwamba, Serikali ifuate taratibu, tuhakikishe sheria hii kwenye manunuzi ya dharura, kweli iwe ni dharura isiwe ni dharura ya kudanganyana, kwenye manunuzi ya hivyo vitu *used*, kweli kuwe kuna sababu ya kununua. Leo unakwenda unataka kununua vifaa vya jeshi, sisi ni *third world*, ukisema unataka uende ukanunue vile vifaa wanavyoendesha nchi kama Marekani, *you are wrong*, hatuwezi tusidanganyane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiambiane hapa sisi matajiri sana, nani kasema! Kwa hiyo, ninachotaka kusema, tusome sheria hii vizuri sana. Tukiisoma sheria hii vizuri sana, sheria ni nzuri na nampongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta sheria hii, *in fact* imechelewa. Sheria hii imefanyaje? Imechelewa. Naomba wafanyakazi wetu, watendaji wetu wawe na uzalendo. Kwa sababu kwenye *procurement* kama hakuna uzalendo, *we are wasting our time*, hata ungeweka sheria nzuri namna gani. Narudia jamani, bado nina hakika ukinunua kitu, kwa mfano, leo unaweza ukanunua gari mpya, unatoka nyumbani kwako unafika barabarani unapata ajali, utakavyokwenda kuiuza ama wanavyokuja kufanya *evaluation* sio gari mpya tena hiyo, *that is a used car*, hata kama imekwenda kilometa kumi. Sasa tusianze kufanya kazi hapa ya kudhani watu, kila mtu anasema hapa, nchi gani hii inanunua vitu *scrap*, nani kasema *scrap*? Tusiwadanganye Watanzania ambao hawajausoma Muswada huu, tunachosema tena ni kwa mazingira na bahati nzuri Waziri amekuwa *specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Ndiyo, Mheshimiwa Silinde taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8). Mzungumzaji aliyepita amesema hakuna mahali ambapo imeandikwa, sasa ningependa nimsaidie. Kwenye hii sheria, angalia kifungu cha 66 (1) na (2), soma vizuri, kinasema: "(1)*Where the public interest demands tha railway machinery, civilian or military ships and civilian or military aircraft that has been used be procured, the procuring entity may, upon approval by the Cabinet and the Authority, proceed with normal or emergency procurement.*

*(2) Where the procurement referred to under subsection (1) is to be done under emergency procurement, the procedure stipulated under section 65 shall, with necessary modification, apply".*

Kwa hiyo, hiyo ni moja. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amekuja vile vile amei-*state* ukurasa wa saba, ameelezea kwenye sehemu ya sita, ndiyo vitu vilivyotumika hivyo hivyo. Sehemu ya tano anasema kuruhusu Serikali kufanya ununuzi wa vifaa maalum vilivyotumika ambavyo gharama yake ni kubwa. Kitu chochote kilichotumika ni *used.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde toa hiyo taarifa, toa tu hiyo taarifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa ya *used*, tusitafsiri *used* kinyume na ukweli, kilichotumika sio uhalisia, kilichotumika ni *used* ndiyo ukweli na uhalisia.

**MWENYEKITI:** Labda nikuweke vizuri kabla sijampa nafasi mpokea taarifa, kwa sababu hukuomba mwongozo au hukusema kuhusu utaratibu kwa maana ya, hapa kuna maneno mawili ambayo yanachanganya, neno *used* na *scraped*. Sasa kwa Kiswahili tuna neno kilichotumika na chakavu, sasa hapa taarifa unayompa iliyo kwenye *section* 66 inasema *used* kwa maana ya Kiswahili ni nini? Iliyotumika na sio *scrapped* kwa maana ya chakavu, sasa Mheshimiwa Peter Serukamba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Silinde namheshimu sana lakini anapotaka kudanganya umma, sio vizuri sana. Sasa hii siwezi kuipokea, *used* ni iliyotumika, *scrapped* ni chakavu, *unless*, halafu kuna nyingine naweza nikamwongezea *recondition*, lakini hapa tunaongelea *used machines*. Kwa hiyo, hiyo taarifa yake siwezi kuipokea. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa nafasi nilizo nazo naona nitapata wachangiaji wengine wawili. Sasa nimwite Mheshimiwa Soni na baadaye Mheshimiwa Albert Ntabaliba atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Mheshimiwa Soni!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuipongeza Serikali kwa kuuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Kwa sababu Sheria iliyokuwepo ya mwaka 2004 kwa kweli ndiyo imetufikisha mahali nchi hii ilipo leo hii. Ilikuwa na upungufu, lakini naamini kwamba Muswada huu ambao tunategemea kuupitisha na tunaamini kwamba utatupeleka huko tunakotegemea kwenda. Pia naipongeza Kamati kwa kazi nzuri walioifanya kwa kuishawishi Serikali na wamefanya kazi kwa makini sana, naamini kwamba haya yote ambayo wametuletea wameyapitia vizuri sana na naamini yataleta manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Serikali pamoja na Kamati kwa kuweka kipengele kile cha Madiwani. Kwa sababu asilimia kubwa ya manunuzi katika ngazi zetu za Halmashauri na ndiyo mahali ambapo inagusa Watanzania wote na ndiyo iko huko ngazi ya chini katika ngazi ya Halmashauri. Wao wakiwa tayari watahusika moja kwa moja katika manunuzi na pia katika kutwaa vile vifaa vya Serikali ambavyo tayari vimepitwa na muda au havitakiwi kutumika tena. Naamini tutaweza kupata manufaa makubwa sana. Lakini nasisitiza Serikali ikubali na iwekwe katika Sheria katika masuala ya kutumia *Force Account.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mifano mingi ambapo kutokana na ile Sheria ya mwaka 2004 tulishindwa kabisa kupata manufaa kwa sababu mfano tulipewa shilingi milioni 18 kwa kujenga darasa kwa kupitia MMES. Lakini ilishindikana kabisa kubadilisha ile Sheria wanasema kwamba *Procurement Act* hairuhusu*,* Ilikuwa sababu nyingi na baadaye tenda zilitolewa watu walijenga hayo madarasa kwa milioni 18 wakati tungeweza kujenga kwa kutumia *Force Account* darasa lile lile kwa *quality* ile ile kwa milioni 12 au 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba baadhi ya vipengele vingeangaliwa, leo hii tunasema tutumie tenda labda kwa *services* za *catering.* Labda katika maofisi yetu tunatoa chai, chakula na huduma ndogo ndogo. Leo hii mtu ambaye hajasajiliwa labda kwenye *process* hizo awe na leseni na vyeti, akiwa hana unakuta ananyimwa kutoa huduma ya chai. Yule anayetoa ile huduma ambaye ana leseni chai ya kawaida tu anaweza kuchaji shilingi 5,000/=, wakati mama ntilie au wale wajasiriamali wadogo wadogo wangeweza kutoa huduma ile ile tena yenye ubora zaidi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna vitu vidogo vidogo ambavyo tunahitaji kuvinunua ambavyo ni lazima vifuate *Procurement Act*. Unakuta gharama inakuwa ni kubwa mno kwa sababu vile vitu mpaka vipite kwenye *process*. Baadhi ya vitu vingeruhusiwa vitumike katika manunuzi ya kawaida ili bila kupita kwenye hii *tendering process,* naamini tungeweza kusaidia kupunguza gharama nyingi. Pia *documents* nyingi za hizi tenda zinakuwa ni siri hasa ukiangalia mambo ya barabara au mambo ya ujenzi. Madiwani kule wakati wanapodai, au ukitaka kuangalia *document* fulani inakuwa ni siri. Naomba iwekwe wazi kabisa kwamba *documents* hizi siyo siri. Iwe *accessible* kwa mtu yoyote yule wakati anapohitaji kuona, ili watu wajue kazi ambazo zimetolewa na kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bei zile ambazo wanapanga zisiwe ni siri, tenda ikishatolewa mwananchi yeyote yule iwe kiongozi au mwananchi wa kawaida awe na haki ya kujua kwamba kitu fulani tumenunua. Kwa mfano, kama ni mfuko wa *cement* umenunuliwa kwa bei gani, isisubiriwe mpaka Madiwani wapitishe taarifa zije kutoka baada ya miezi sita wakati mfuko wa *cement* unauzwa shilingi 15,000/= kama wameandika elfu 18,000 au 20,000, mwanzoni tu wakati hiyo tenda inatolewa, mtu angepewa ile tenda na bei zingetolewa tungeshajua kwamba hii haifai na ingeweza kusimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mambo ya uzalendo. Katika haya mambo yote tukisema hii ni sheria kama alivyosema msemaji aliyepita, hakuna mahali ambapo unaweza kumbana. Hata lile darasa la milioni 18 lililojengwa, utamshtaki nani? Kwa sababu amepitia vipengele vyote, hakuna mahali ambapo utaweza kumbana. Sisi kule imetokea, kuna kazi kwa mfano ya barabara, tenda imetolewa, barabara ni kilometa tatu, labda ni shilingi milioni tisa kwa kuchonga. Lakini kuna watu ambao wako majirani pale *TANAPA* na wafanyabiashara wengine, wana vifaa vya kutosha, anasema wekeni futi ili muweze kuchonga barabara. Ile barabara ya kilomita tatu tungeweza kuchonga hata kilomita 12. Lakini kwa ajili ya haya mambo ya *procurement* inashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye Kanuni pawe na mahali ambapo tukiomba kibali maalum, mahali ambapo wananchi na wadau wengine mbalimbali tunaweza kuchangia basi hiyo iweze kutumika ili kazi iweze kufanyika zaidi na nchi ipate manufaa na wananchi pia wapate manufaa. Pia suala la *lowest bidder* hilo sikubaliani nalo. Napendekeza kwamba, tuangalie *quality* mara nyingine tunachagua mtu ambaye *the lowest,* lakini mwisho wa siku unakuta kazi ile anashindwa, inabidi turudie na gharama inakuwa kubwa. Hata yeye anapo-*bid the lowest quality* na vifaa ambavyo atatumia pia vitakuwa havifanani. Lakini tuangalie bei iwe *reasonable* lakini *quality* ya kazi pia iwe *reasonable* na ambayo itadumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine napenda kuchangia kuhusu wakati ambapo vifaa vya Serikali ambapo sasa vinatakiwa viwe *disposed,* mara nyingi hivyo vifaa vinaweza kutumika. Nashukuru katika sehemu nyingi tulishindwa, lakini naipongeza *TRA,* kuna kipindi fenicha zao, ilikuwa zipigwe mnada lakini waliomba kibali tukaweza kupeleka vile vifaa, meza, viti na makabati katika shule zetu na leo hii zinaendelea kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, ningependekeza kama ni magari au vifaa vingine vya Serikali ambavyo sasa havitumiki, *priority* ya kwanza badala ya kuwa, hata na tenda kama zinaweza kurekebishwa kidogo zikatumika katika Taasisi zetu za Umma kwa mfano, kwenye shule, zahanati na taasisi zingine, basi wapewe *priority* kwa ile *book value* iliyopo, hiyo itatusaidia. Mara nyingi hayo manung'uniko yanayotokea kwamba gari kwa mfano linauzwa milioni tatu lakini baada ya muda ule gari ikiwa barabarani ina thamani tena ya milioni 20. Lakini *book value* ni milioni mbili. Kama taasisi za nchini kama shule, hospitali au *NGOs* ambazo zinafanya kazi za huduma za jamii, ziko tayari kununua kwa hizo milioni, basi ndiyo wapewe *priority* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala hili la kununua vifaa vipya na vifaa ambavyo ni *used.* Nasema hapa tutumie busara, mara nyingi hata unaponunua kifaa kipya, leo mtu aliyenunua *Cruiser* mpya na anayenunua *Mahindra* mpya au anayenunua gari ya Mchina mpya, kweli zinafanana? Hazifanani. Kwa hiyo, hata kwenye *used* unaweza kununua *used, quality* nzuri, lakini tatizo linakuja ni nani atathibitisha kwamba *quality* yake ni nzuri. *(Makofi)*

Lakini pia tunapopotosha uma kwamba leo hii ajali iliyotokea kwa mfano *MV Spice Islander* Zanzibar kwamba ni kwa ajili ni *used*, ndiyo maana ajali imetokea. Hata ingekuwa mpya umejaza watu 3,000 kwenye meli ya abiria 200 watakufa tu. Ndege inayobeba watu 60 ukapakia tani 10 na abiria 100 wataanguka tu watakufa. Kwa hiyo, zile taasisi ambazo zinatakiwa kucheki kwamba kama ni magari ya abiria, leo hii mabasi tukisema yasinunuliwe *used* naamini kwa mfano kwangu kule Babati itakuwa hakuna usafiri kabisa. Mabasi mapya yanatembea katika baadhi ya barabara tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabasi mengi ambayo yanabeba abiria kule kwetu ni *used cars* ambazo zimeletwa, zimetengenezwa ilimradi *quality* iwe nzuri. Isipokuwa tufuate zile kanuni, sheria na utaratibu. Naamini kama lengo ni hili badala ya kuwa *Cabinet* ipitishe, napendekeza kwamba, kama ni manunuzi ya dharura basi iletwe hapa Bungeni, Bunge hili liridhie. Sisi turidhie badala ya *Cabinet* tusiilaumu Serikali, sisi wote tukiridhika kwamba hicho chombo kinatakiwa kununuliwa, naamini manung'uniko hayatakuwepo na malengo ya Serikali tutayafikia. Kwa hiyo, badala ya *Cabinet* napendekeza iwe ni Bunge hili. Hicho kitu ambacho kinatakiwa kununuliwa kiletwe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie suala la uzalendo. Haya manung'uniko yote yanatokea ni kutokana na watu kutokuwa na uzalendo na nchi yao na kutokuwa na uzalendo na maeneo yao. Tusibaki kulalamika, hata tungeleta sheria ya aina gani, lakini watu ambao watakaoitekeleza hii Sheria hawa ambao tunategemea kuwakabidhi hii kazi ya *procurement,* kama watakuwa siyo waadilifu bado tutarudi hapa tutaendelea kuilaumu Serikali hii na tutaendelea kujilaumu sisi wenyewe. Lakini pia tungeweka sheria mbali na hii kwa wale ambao watakiuka sasa hivi hii sheria, akibainika isiwe ni kifungo kidogo tu, huyo mtu napendekeza afungwe chini ya hati ya *economy sabotage* yaani asitoke ndani kabisa. Yeye na mali zake zote zifilisiwe ili tuoneshe mfano. Tukishafanya hivyo naamini watu watafuata sheria na wataogopa kufanya mambo ambayo si halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nirudie suala la *Forced Account,* iwekwe wazi ili mahali ambapo wananchi na wadau wengine wanaweza kuchangia ile pesa kidogo ambayo tunayo tuweze kufanya kazi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja lakini tuiweke vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soni. Sasa naona muda bado ninao, umetuachia muda kidogo. Nimwite Mheshimiwa Ntabalila Albert Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo juu ya Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuuleta Muswada huu ndani ya Bunge letu ili tuweze kutoa mchango wetu wa namna ya kuuboresha. Vile vile niipongeze Kamati iliyotoa mapendekezo na kwa kuwa walisema kwamba, walishaurudisha huu Muswada mara mbili kwa kutoa maoni yao. Kwenye kifungu cha 66 sina matatizo sana. Naona kimejaribu kuonesha kwamba, *Cabinet* inaweza kuwajibika. *Cabinet* iweze kuwajibika kama kuna hayo manunuzi ya vitu chakavu au vitu vilivyotumika. Neno ni lile lile ni namna unavyoli-*twist* tu, lakini kimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nakiona kiendelee kuwa hivyo hivyo kwa sababu makosa yatakayofanyika ya manunuzi ya vitu hivi yabakie ndani ya Serikali. Bunge kama Bunge si kazi yetu kufanya manunuzi. Kazi yetu ni kutunga Sheria hii tunayoipitisha Sheria ya Ununuzi, basi Wizara na Serikali waweze ku-*execute* hayo manunuzi. Sasa vitu vichakavu au vitu vilivyotumika, ndege iliyotumika, kwa *concept* ya kawaida Watanzania wanaelewa, lakini ukiwaambia kwamba wanakwenda kupanda ndege iliyotumika, watu wanaanza kuiogopa. Kwa hiyo, ningependa kusema tu kwamba, *slightly* kwa kuwa Serikali itakuwa imeamua, Watanzania leo ungewauliza kwamba je, mngependa kupanda ndege, Serikali tununue ndege iliyotumika au ambayo haijatumika, Watanzania wangekwambia kwamba, ni ndege ambayo haijatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuendelea sana, ni busara ya Serikali na Serikali tunaiamini, nafikiri inafanya kazi vizuri. Hivyo vyombo ambayo vitanunuliwa kwa kweli ni kwa maisha ya Watanzania, Watanzania wanahitaji usalama wa maisha yao. Hapo siendi ndani sana. Lakini la pili, nimefanya kazi ya manunuzi kwa miaka 11 kabla ya kuingia Bungeni, ndiyo ilikuwa kazi yangu. Naelewa na sitaki kuingia ndani. Lakini ninachosema ni kwamba, *procurement* yoyote ile haiendi na Sheria lakini nafikiri zaidi ni ile *moral*, unaamini kwamba, unachokifanya ni cha dhati. Sasa ile *trust* kama wenzangu walivyosema, ni kitu kikubwa sana kwenye manunuzi. Mnaweza mkawa mmekaa kikao na wote mmekubaliana na mkakuta Sheria zote mmezifuata, lakini vile vile na nchi mmeiumiza. Kwa hiyo, siyo kitu kizuri sana nafikiri *trust* ndiyo tuiweke mbele kuliko sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zetu tumekuwa nazo lakini hazina meno, ndiyo tatizo la nchi hii. Sheria za nchi hii zimekosa meno, hatuoni Waziri wa Fedha, hatuoni vyombo vikishughulika na watu wakichukuliwa hatua kwa *misconduct* ya manunuzi. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo nafikiri tusogee mbele kidogo tuoneshe Watanzania kwamba jamani tunasimamia hivi vitu, tunakaa humu Bungeni, tunatunga sheria, watu wanaharibu, hakuna anayechukuliwa hatua. Watu wanahamishwa kutoka hapa kwenda hapa kwamba ndiyo ufanisi wa Serikali au ndiyo ufanisi wa Wizara. Sasa nafikiri siyo kitu kizuri. Tufike mahali *Cabinet* yetu ifanye kazi, ifanye kazi Watanzania waiamini. Itafikia mahali watakuja ku-*raise* hii *Cabinet* tuipe *marks* ngapi? Utakuja

kushangaa itakuja kupewa *marks* ndogo kwa sababu ya maamuzi, watu wanaharibu, wanahamishiwa maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Sheria hii sioni mahali ambapo, kwa sababu hii ni sheria yetu, sioni mahali ambapo panaonesha patakuwa na upendeleo kwa Watanzania. Lazima ifike mahali tuoneshe kwamba ndani ya Sheria hii manunuzi ya kiasi fulani mahali fulani yanaweza yakafanywa na Watanzania. Siyo lazima iwe ni *International Bid,* kunaweza kuwa na *Local Bid* ambayo ndani ya Sheria hii siioni ikituonesha na ikituelekeza kwamba wale wanao-*deal* na manunuzi sasa waweze kuona kwamba hapa *builders* wawe Watanzania na watu wa nje. Sasa ni vizuri, hata kama tukiifanya kuwa ni *internal tender*, Watanzania hatutaweza na ningeshauri kwamba tuwe na hiyo *provision.* Tuna hii asilimia kumi mnayoichaji *TRA* pale kwa kuleta magari mabovu au yaliyotumika. Sasa hivi tunachajiwa asilimia kumi kwa kuleta gari lililokaa zaidi ya miaka kumi. Je, tutakapoleta meli ambayo imezidi miaka kumi, itachajiwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napongeza kwamba Madiwani kuhusika lakini isiwe ndiyo chanzo cha migogoro ya manunuzi kwenye Halmashauri zetu. Wanaweza wakahusika ikawa *in chaos* kwa nchi nzima, mambo hayaendi. Kwa hiyo, nacho ni kitu muhimu na cha kuangalia ili mambo yaweze kwenda. Lakini kikubwa zaidi mimi siwezi kusema mengi, *commitment* ya Wizara inayohusika ichukue hatua kwa wale wanaofanya vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema mengi, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Huyu ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo na kwa kesho wachangiaji wetu watakuwa, ataanza Mheshimiwa Rosweeter Kasikila na baadaye Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na wengine na nadhani wachangiaji karibu wote mlioomba kwa mujibu wa orodha iliyopo sasa mtapata nafasi. Kama itaongezeka kesho hatujui.

Ninalo tangazo moja. Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa vile vitabu vya rasimu ya Sera ya Elimu vilivyogawiwa Bungeni ndivyo vitakavyotumika siku ya Semina tarehe 13 Novemba, 2011. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa mvisome, ikiwa ni kama sehemu ya maandalizi kwa ajili ya semina hiyo. Baada ya tangazo hilo, sina la zaidi. Naomba nichukue nafasi hii kuahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.36 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 11 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*